# ATHARI ZA MTAGUSANO KATI YA JAMII NA EKOLOJIA KATIKA USHAIRI WA KITHAKA WA MBERIA: *BARA JINGINE* NA *RANGI YA ANGA*

**NA**

**MUGWE JOHN MWANIKI**

**C50/ 80397/ 2015**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2018**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine chochote.

……………………………. ……………………….

**Mugwe John Mwaniki** **Tarehe**

**Mtahiniwa**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi tulioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia Idara ya Kiswahili.

………………………. ………………………….

**Prof. Rayya Timammy** **Tarehe**

……………………….. ………………………….

**Ms. Mary Ndung'u** **Tarehe**

# TABARUKU

Tasnifu hii namtabarukia mama yangu Bi. Lucy Wanjiru kwa kunisomesha na kunipa nasaha ambayo imenisaidia maishani mwangu.

Namtabarukia vile vile mke wangu mpenzi Mary Muthoni na mwanangu Austin Mburu. Kwa hakika mumekuwa mhimili muhimu katika masomo yangu.

## SHUKRANI

Kwanza ningependa kutoa shukrani za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siha njema wakati niliokuwa nikisoma na kuandika tasnifu hii. Pia nawashukuru wasimamizi wangu Prof. Rayya Timammy na Ms. Mary Ndung'u kwa kuniongoza na kunishauri wakati wa kuandika tasnifu hii. Nawashukuru kwa kutenga muda wenu kila mara nilipohitaji kuelekezwa. Vile vile ningependa kuwashukuru wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili ambao mihadhara yao imenijenga kiusomi. Shukrani maalum ziwaendee wahadhiri wafuatao: Prof. Iribe Mwangi, Prof. John Habwe, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Mwenda Mbatiah, Dkt. Jefwa, Dkt. Zaja, Dkt. Mbuthia na Dkt. Jerono.

Pia napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa familia yangu na hasa mke wangu Bi. Mary Muthoni. Nakushukuru sana kwa uvumilivu wako na kunitia moyo katika kipindi hiki nilichokuwa nikishughulikia tasnifu hii. Pia namshukuru ndugu yangu Michael Munga kwa kunitia moyo kwamba nijitahidi na Mwenyezi Mungu ataniwezesha kumaliza masomo yangu.

## IKISIRI

Tasnifu hii inahusu uchunguzi wa athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia katika diwani ya *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014). Tumelenga kuchunguza athari za mtagusano baina ya jamii na mazingira. Ili kufaulisha lengo hili tumejikita katika mazingira ya kijiografia kama vile misitu, mito, bahari na kadhalika na kuonyesha jinsi yanavyoathiriwa na mwingiliano baina ya wanajamii. Vilevile tumebainisha jinsi masuala ya kijamii kama vile ufuska, ndoa za mapema, ubaguzi wa kijinsia na teknolojia ya kisasa yanavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii. Pia tumebainisha masuala ya kiuchumi na kisiasa kama vile ukosefu wa kazi, ufisadi, uongozi mbaya miongoni mwa mengine yanavyoingiliana na kuathiri mfumo wa ekolojia jamii. Ili kufanikisha haya yote tumeongozwa na Nadharia ya Uhalisia ilioasisiwa na Lukacs mwaka wa 1963. Nadharia hii inadai kuwa msimulizi wa kazi ya fasihi sharti aeleze masuala ya kweli na yanayoweza kuaminika na kuthibitika katika jamii anamoishi. Nadharia hii imetuelekeza katika kubainisha mambo yanayoathiri mfumo wa ekolojia katika hali halisi ya maisha. Pia tumeongozwa na Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia ilioasisiwa na Bronfenbrenner mwaka wa 1989. Nadharia hii inadai kuwa maisha ya jamii huathiriwa na watu na viumbe vingine vinayoizunguka. Nadharia hii imetuelekeza katika kubainisha jinsi mahusiano na maingiliano ya jamii yanavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii.

## YALIYOMO


UNGAMO ........ i
TABARUKU ........ ii
SHUKRANI ........ iii
IKISIRI ........ iv
YALIYOMO ........ v
ORODHA YA VIFUPISHO ........ viii
UFAFANUZI WA DHANA ........ ix
SURA YA KWANZA ........ 1
UTANGULIZI ........ 1
1.0 Usuli wa Mada ........ 1
1.1 Tatizo la Utafiti ........ 3
1.2 Madhumuni ya Utafiti ........ 4
1.3 Maswali ya Utafiti ........ 4
1.4 Sababu za Kuchagua Mada ........ 4
1.5 Upeo na Mipaka ........ 5
1.6 Msingi wa Kinadharia ........ 6
1.6.1 Nadharia ya Uhalisia ........ 6
1.6.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Uhalisia na Michango yake ........ 8
1.6.2 Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia ........ 9
1.6.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia na Michango yake ........ 10
1.7.0 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ........ 11
1.7.1 Ushairi na Fasihi kwa Jumla ........ 12
1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga* ........ 19
1.8.0 Mbinu za Utafiti ........ 22
1.8.2 Ukusanyaji wa Data ........ 23
1.8.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Matokeo ........ 23
1.8.4 Hitimisho ........ 24
SURA YA PILI ........ 25
ATHARI ZA MTAGUSANO KATI YA JAMII NA MAZINGIRA ........ 25
2.0 Utangulizi ........ 25

2.1 Uharibifu wa Misitu ........ 25
2.2 Hali ya Hewa na Ongezeko la Joto ........ 30
2.3 Uchafuzi wa Mito na Mabwawa ........ 33
2.4 Milima na Mabonde ........ 37
2.5 Uhifadhi wa Bahari na Maziwa ........ 39
2.6 Mmomonyoko wa Udongo ........ 41
2.7 Hitimisho ........ 47
SURA YA TATU ........ 48
ATHARI ZA MASUALA YA KIJAMII KWENYE MFUMO WA EKOLOJIA JAMII ........ 48
3.0 Utangulizi ........ 48
3.1 Ufuska ........ 48
3.2 Dawa za Kulevya ........ 50
3.3 Mimba na Ndoa za Mapema ........ 52
3.4 Ubaguzi wa Kijinsia ........ 57
3.5 Ukeketaji wa Mtoto wa Kike ........ 60
3.6 Teknolojia ya Kisasa ........ 62
3.7 Hitimisho ........ 63
SURA YA NNE ........ 64
ATHARI ZA MASUALA YA KIUCHUMI NA KISIASA KWENYE MFUMO WA EKOLOJIA JAMII ........ 64
4.0 Utangulizi ........ 64
4.1 Ukosefu wa Kazi ........ 64
4.2 Ufisadi ........ 67
4.3 Hali ya Umasikini ........ 68
4.4 Uongozi Mbaya ........ 72
4.5 Hitimisho ........ 77
SURA YA TANO ........ 78
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 78
5.0 Utangulizi ........ 78
5.1 Matokeo ya Utafiti ........ 78
5.2 Mapendekezo ya Utafiti ........ 81

5.3 Hitimisho ........ 82
MAREJELEO ........ 83

## ORODHA YA VIFUPISHO

**Mh-** Mhariri

**NEMA-** National Environment Management Authority

**TY** – Tafsiri Yangu

**UK-** Ukurasa

## UFAFANUZI WA DHANA

**Ekolojia-** Ni taaluma inayochunguza mahusiano baina ya viumbe na mazingira.

**Ekolojia jamii –** Ni taaluma inayoangazia mahusiano baina ya binadamu na mazingira na hasa utegemeano baina ya binadamu na taasisi mbalimbali.

**Mtagusano –** Ni dhana inayorejelea maingiliano na mahusiano baina ya kitu kimoja na kingine.
**Tabia nchi –** Ni dhana inayorejelea mabadiliko ya hali ya anga kutokana na ongezeko la hali ya joto duniani.

**Ufeministi wa Kiekolojia –** Ni mkabala wa kifeministi unaoonyesha mahusiano kati ya wanawake na mazingira na mchango wao katika kuyahifadhi.

# SURA YA KWANZA
# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli wa Mada

Katika karne ya ishirini na moja, maisha ya binadamu yamebadilika kwa kiwango kikubwa. Hii ni kwa sababu binadamu anaendelea kujihusisha na harakati za uvumbuzi wa teknolojia mpya. Uvumbuzi huu umeathiri mfumo wa ekolojia. Pia kutokana na suala la utandawazi mifumo mbalimbali ya kijamii kama vile: ndoa, elimu, malezi, biashara, utamaduni, uchumi, siasa imeathiriwa suala ambalo limeathiri mahusiano na utangamano baina ya wanadamu. Hali hii hutokea kwa sababu jinsi ambavyo teknolojia inavyoendelea kubadilika na kuvumbuliwa ndivyo navyo ekolojia inabadilika na kuathiri maisha ya binadamu.

Katika utafiti huu, tumechunguza athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia katika diwani za Kithaka wa Mberia: *Bara Jingine* (2001) na *Rangi ya Anga* (2014). Gromov (2006) anasema kuwa, Mberia ni miongoni mwa washairi wachache na maarufu nchini Kenya, ambao wanatunga mashairi ya kisasa. Nakubaliana na kauli hii ya Gromov kwani Mberia ni miongoni mwa waandishi maarufu wa ushairi na ambaye ametoa mchango faafu katika kukuza na kuendeleza mashairi huru. Bertoncini (2010), anaunga mkono kauli hii ya Gromov anaposema kuwa Mberia ni mmojawapo wa washairi maarufu nchini Kenya ambao wameipa jamii mtazamo na mwelekeo mpya. Kulingana na Bertoncini, mashairi yake kwa jumla yanazungumzia kuhusu masuala ambayo yanawakumba wanajamii katika maisha yao ya kawaida. Kauli hii ya Bertoncini ni ya kweli kwa sababu mashairi ya Mberia yanaangazia masuala kama vile: siasa, dhuluma za kiuchumi na kijamii na pia uchafuzi na uharibifu wa mazingira kama vile uharibifu wa misitu, hewa na mito. Katika kazi zake, anaonekana akikashifu uongozi wa kiimla, dhuluma zinazofanyiwa wanawake kama vile kubakwa kwa wasichana wa shule, ndoa za mapema na hata ukahaba ambao unasababishwa na umasikini. Pia anaonyesha athari zinazosababishwa na binadamu anapoharibu ekolojia.

Ongarora (2017) anasema kuwa baadhi ya mashairi ya Mberia yanazungumzia kuhusu jinsi binadamu anavyochangia katika uharibifu wa mazingira na kwa upande mwingine kuna yale mashairi ambayo yanazungumzia kuhusu haja ya kutunza mazingira. Anaendelea kusema kuwa uharibifu wa mazingira ni tishio kwa binadamu na hata wanyama wengine ambao wanamzingira.

Uchafuzi na uharibifu wa mazingira hutokea kupitia kwa uchafuzi wa maji na hewa, ukataji ovyo wa miti, mmomonyoko wa udongo na ufugaji wa wanyama wengi kiholela miongoni mwa njia nyingine. Masuala haya yote ambayo Mberia anayaangazia, yanajitokeza wazi wazi katika diwani za *Bara Jingine (*2001) na *Rangi ya Anga* (2014).

Ekolojia ni taaluma inayochunguza kuhusu mifumo na dhima ya maumbile ya kiasilia. Dhima ya mifumo ya ekolojia huathiriwa na jinsi binadamu anavyohusiana na mazingira yake (Odum, 1971). Kauli hii ya Odum inaoana na Krebs (1978) anayesema kuwa ekolojia ni taaluma ya kisayansi ambayo inahusu uchunguzi wa mwingiliano na mahusiano kati ya binadamu na binadamu mwenzake, wanyama na mimea. Kulingana na wataalamu hawa wawili ni kuwa ekolojia ni taaluma inayochunguza mahusiano na maingiliano baina ya jamii na mazingira yake. Mazingira haya yaweza kuwa ya kijiografia kama vile: misitu, mito, mabadiliko ya hali ya anga na kadhalika. Pia yaweza kuwa mazingira ya kijamii kwa mfano, shule, familia ujirani, utamaduni na kadhalika.

Kutokana na uharibifu wa mazingira katika karne ya ishirini na moja, binadamu anastahili kuibuka na mbinu mpya za kuangazia mazingira ya kiasili na jinsi ambavyo anastahili kuingiliana nayo (Claser, 2002). Binadamu anapoendelea kuhitilafiana na mazingira yake, huathiri maendeleo yake ya kiuchumi, kijamii na kisiasa ambayo huibuka kila siku. Huku kuhitilafiana kwa binadamu na mazingira yake kukiongezeka husababisha baadhi ya matatizo kujidhihirisha wazi. Baadhi ya matatizo haya ni kama vile: kufifia kwa mali asili, mabadiliko ya hewa na kuzorota kwa mifumo ya kiuchumi na kijamii. Binadamu kwa mfano, anapoharibu misitu na chemichemi za maji, huweza kusababisha mmomonyoko wa ardhi ambao huweza kuathiri jamii kiuchumi na kijamii. Hii ni kwa sababu jamii nyingi hutegemea ardhi kwa kilimo ili kuweza, kwa mfano kukabiliana na janga la njaa. Mabadiliko ya hali ya hewa huweza kuathiri jamii kwa kusababisha kuzorota kwa afya ya binadamu na hata wanyama. Mabadiliko haya pia huweza kuathiri baadhi ya mimea ambayo binadamu na wanyama hutegemea kama chakula.

Jinsi binadamu anavyoendelea kuingiliana na mazingira yake ndivyo anavyoendelea kuyaharibu. Hii ni kwa sababu binadamu hujibunia mazingira yake tofauti na yale ya kiasili. Uharibifu huu huishia kuwa wa kihistoria na kitamaduni hali ambayo huathiri maisha ya kawaida ya wanajamii. Binadamu anafanya hivi kupitia mifumo mipya ya kiteknolojia. Suala hili la binadamu kuharibu mazingira lilianza katika mapinduzi ya kwanza ya viwanda na kuendelea hadi sasa, huku

likichangiwa zaidi na utafiti ambao unaendeshwa kupitia kwa teknolojia mpya ambayo inavumbuliwa na binadamu kila uchao (Crutzen, 2008). Mfumo wa ekolojia jamii huchangia jinsi binadamu huuona ulimwengu kwa ujumla na jinsi mfumo wa ulimwengu unavyoingiliana na sayansi. Ili binadamu aweze kufikia uwiano kati yake na mazingira anamoishi lazima ajielewe na kujitambua (TY). Kwa hivyo ni wazi kuwa watafiti wanaojishughulisha na mfumo huu wa ekolojia jamii, huangazia mwingiliano kati ya binadamu na mazingira yake. Msingi mkuu wa nadharia hii ni kuonyesha jinsi ambavyo maisha ya binadamu hubadilika kutokana na mabadiliko ya kimazingira anamoishi. Mabadiliko haya yaweza kuwa ya kijamii au kijiografia.

Fasihi humfanya mtu kiumbe razini na aelewe mazingira anamoishi (Njogu na Chimerah, 1999). Kwa vile fasihi inafungamanishwa na maisha ya binadamu, basi msanii hupata msukumo na mshawasha wa kutunga kazi yoyote ya kifasihi, kutokana na matukio na mabadiliko ambayo yanaikumba jamii katika mazingira anamoishi. Kulingana na wasomi hawa ni wazi kuwa si rahisi kutenganisha fasihi na mifumo ya kiekolojia ambayo inaikumba jamii. Hii ni kwa sababu fasihi ni kioo cha jamii na husawiri jamii kulingana na mabadiliko inayopitia. Mwanasanaa yeyote basi hana budi kutumia fasihi kuangazia mazingira anamotoka na kuyaboresha kwa manufaa ya jamii kwa jumla.

## 1.1 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu ulinuia kuchunguza na kubainisha athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia katika diwani ya *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (2014). Katika utafiti huu tulichochewa na ukweli kwamba kuna kazi za fasihi ya Kiswahili ambazo zimeandikwa kuhusiana na ekolojia. Vilevile tumenuia kubaini athari za mtagusano kati ya jamii na mazingira. Hii ni kwa sababu binadamu haishi katika ombwe tupu bali hutangamana na kuingiliana na mazingira anamoishi. Pia utafiti huu umenuia kubainisha masuala ya kijamii yanayoathiri mfumo wa ekolojia jamii kwani binadamu huingiliana na kutegemeana katika maisha yao ya kila siku. Hatimaye tumenuia kuangazia athari za masuala ya kisiasa na kiuchumi kwenye mfumo wa ekolojia jamii.

## 1.2 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti wetu umeongozwa na madhumuni yafuatayo:

1. Kuchunguza athari za mtagusano kati ya jamii na mazingira kupitia utambulishaji na uwasilishaji wa mandhari katika *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga.*
2. Kubainisha athari za masuala ya kijamii kwenye mfumo wa ekolojia jamii kupitia uwasilishaji wa maudhui katika *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga.*
3. Kuchunguza athari za masuala ya kisiasa na kiuchumi kwenye mfumo wa ekolojia jamii kupitia uwasilishaji wa maudhui katika *Bara Jingine na Rangi ya Anga*.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

1. Je, kuna athari kutokana na mtagusano kati ya jamii na mazingira katika *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga?*
2. Je, ni masuala yepi ya kijamii yanayoathiri mfumo wa ekolojia jamii katika *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga?*
3. Je, ni masuala yepi ya kisiasa na kiuchumi yanayoathiri mfumo wa ekolojia jamii katika *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga?*

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Fasihi hufungamanishwa na maisha ya binadamu na msanii hupata msukumo na mshawasha wa kutunga kazi yoyote ya fasihi kutokana na matukio na mabadiliko ambayo yanaikumba jamii katika mazingira anamoishi, (Njogu na Chimerah, 1999). Kwa hivyo mada hii tumeiteua kwa sababu ekolojia ni suala muhimu sana katika maisha ya kawaida ya binadamu ambayo hubadilikabadilika kulingana na kipindi fulani cha wakati na mazingira anamoishi. Hata kama dhana hii imezungumziwa hapo awali na baadhi ya wahakiki, sababu yetu mahususi ya kuiteua ni kutaka kufahamu ni zipi athari za mtagusano kati ya jamii na mazingira. Pia tumechochewa na hamu ya kutaka kuchunguza ni vipi mfumo wa ekolojia jamii unavyoathiriwa, kupitia uwasilishaji wa masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni kuwa, Mberia anaangazia masuala mazito yanayoathiri ekolojia kama vile uharibifu wa misitu, ardhi, mito, hewa, bahari na maziwa miongoni mwa mengine. Masuala mengine anayoyazungumzia ni kama vile: malezi, ndoa, elimu, biashara, utamaduni na kadhalika. Mambo haya hayatendeki tu katika jamii anamotoka mwandishi bali

katika ulimwengu mzima kwa jumla. Masuala haya pia yanaathiri binadamu katika shughuli zake za kila siku. Binadamu pia huwa haishi katika ombwe tupu bali huingiliana na kutagusana na viumbe na vitu vingine ambavyo vinamzingira. Isitoshe, maisha ya binadamu hubadilikabadilika kila kuchapo kwa sababu ya uvumbuzi mpya wa kiteknolojia. Uvumbuzi huu umeathiri ekolojia, suala ambalo limechangia kubadilika kwa maisha ya binadamu. Teknolojia hii pia imechangia kuendelea na kuenea kwa viwanda ambavyo vinazalisha rasilimali, suala ambalo linaathiri mazingira anamoishi binadamu na hivyo basi kuleta mikinzano kati yake na wanyama ambao wanayategemea mazingira yaya haya ambayo binadamu anayategemea na kuishi. Utafiti huu utasaidia kuleta uwiano mwema kati ya binadamu na mazingira yake.

Jambo jingine ambalo lilitutia ari ya kufanya uchunguzi huu ni kwamba, tafiti ambazo zimefanywa hapo awali kuhusu ushairi wa Mberia, nyingi zinaangazia fani na maudhui. Lakini suala la ekolojia na jinsi linavyojitokeza katika ushairi wa Mberia linastahili kuchunguzwa kwani linahusu vizazi vyote. Ntarangwi (2004) anasema ya kwamba kazi ya fasihi inafaa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida wa kweli na halisi. Anaendelea kusema kuwa msanii anapaswa kuandika kuhusu watu katika hali halisi ya maisha. Ili kufanikisha uandishi wake, mtunzi anapaswa kuonyesha wahusika, matukio na mandhari yanayokubalika na kuaminika katika jamii ya wakati wake. Kauli hii ya Ntarangwi imetusaidia katika kubainisha masuala ya ekolojia ambayo yanajitokeza katika *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga* na jinsi ambavyo yanaathiri mifumo mbalimbali ya kijamii.

### 1.5 Upeo na Mipaka

Utafiti wetu umejikita katika uchunguzi wa athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia katika *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014). Katika utafiti huu tumeangazia athari za mtagusano kati ya jamii na mazingira na jinsi mwingiliano huu unavyoathiri maisha ya binadamu na viumbe vingine. Ili kufanikisha lengo hili tumejikita katika mazingira ya kijiografia pekee. Vilevile tulinuia kubainisha jinsi masuala ya kijamii yanavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii. Hatimaye tumeangazia namna masuala ya kiuchumi na kisiasa yanavyoathiri mchakato mzima wa ekolojia jamii. Ili kufaulisha haya tumejikita katika kipengele cha maudhui pekee. Katika utafiti huu hatujazungumzia kuhusu matumizi yoyote ya lugha ila pasipo budi bila kupoteza malengo yetu. Ili kutimiza malengo haya tumeteua mashairi kumi na sita kwa jumla. Kumi na manne kutoka *Bara Jingine* na mawili kutoka *Rangi ya Anga* ambayo yamegawanywa

katika sehemu mbalimbali. Vilevile utafiti huu umeongozwa na mihimili ya Nadharia ya Uhalisia na Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia.

## 1.6 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia mbili ambazo ni Nadharia ya Uhalisia na Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia. Nadharia hizi tumeziteua kwa sababu zimetuwezesha kutimiza madhumuni yetu ya utafiti. Nadharia ya Uhalisia imetusaidia katika kuchunguza athari za mtagusano wa jamii na mazingira. Hii ni kwa sababu Lucas (1963) anasema kuwa uhalisia huchunguza undani wa picha na mandhari yanayoonekana ya kihalisia na kugundua sheria za mabadiliko zinazosababisha hali hii. Kulingana na mtaalamu huyu ni wajibu wa msanii kuelewa mazingira anamoishi kama kitu changamano kinachobadilika. Kwa hivyo ni wazi kuwa mtazamo huu wa kihalisia unatilia mkazo kuwa yanayoangaziwa katika kazi ya kifasihi lazima yathibitike katika ulimwengu halisi. Nadharia hii ilitufaa kwani ekolojia inahusisha mandhari ambayo yanamzunguka binadamu na jinsi anavyoingiliana nayo. Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia imetuwezesha kuchunguza jinsi ekolojia jamii inavyoathiriwa na masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hii ni kwa sababu Bronfenbrenner (2005) anasema kuwa maendeleo ya binadamu ya kiuchumi, kisiasa, kijamii, kiutamaduni na kiteknolojia huathiriwa na jinsi ambavyo anaingiliana na kutangamana na mazingira anamoishi. Binadamu akihitilafiana na mazingira anamoishi, huweza kuathiri mifumo yake ya kijamii kama vile: ndoa, malezi, elimu, biashara, siasa na kadhalika. Nadharia hii imetusaidia kuchunguza jinsi ekolojia inavyoathiriwa kupitia mabadiliko ya mifumo hii.

### 1.6.1 Nadharia ya Uhalisia

Nadharia hii iliasisiwa katika karne ya kumi na tisa, kuelezea tapo la kipindi maalum cha kihistoria katika fasihi ya Ulaya. Dhana hii ilianza kutumika katika nchi ya Ufaransa kabla ya kusambaa katika nchi ya Uingereza, Urusi na hatimaye Marekani. Mmoja kati ya wataalamu wanaohusishwa na tapo hili la uhalisia ni Lukacs (1963) ambaye anaamini kuwa usawiri wa uhalisia sharti uangazie picha inayoonekana ya uhalisi na kubainisha kanuni za mabadiliko ya kihistoria zinazosababisha hali fulani. Mtaalamu huyu anadai kuwa mtunzi wa kazi fulani ya fasihi ana jukumu la kuelewa ulimwengu kama kitu changamano na kinachobadilika kulingana na wakati. Anaendelea kusema kuwa mwandishi wa kihalisia hujaribu kuonyesha mtazamo wake

huku akitumia mandhari ambayo yanamzingira. Mwandishi husawiri wahusika kulingana na sifa zao au hali ya mazingira ambayo inawazunguka na ukweli wa mhusika na mambo ambayo anayafanya hujitokeza tu kwa kuangazia jinsi mhusika huyo anavyoingiliana na mandhari yake. Kulingana na Lukacs ni dhahiri kwamba ni wajibu wa mwandishi kufichua msukumo unaosababisha mabadiliko haya ya kihistoria katika jamii na vilevile ni wajibu wake kutoa suluhisho la matatizo ambayo yanaikumba jamii katika kipindi cha wakati wake. Lukacs (1963) anashikilia kuwa jamii hubadilikabadilika kulingana na wakati na pia matatizo ambayo huikumba jamii hutofautiana katika vipindi maalum vya wakati.

Dhana ya uhalisia iliwekewa misingi na mwanafalsafa kwa jina Hegel (1971). Alitumia dhana hii kurejelea kazi ya fasihi ambayo inaonyesha ulimwengu ambapo wahusika wanatekeleza mambo kutokana na msukumo wa hali halisi ya maisha wanamoishi. Kulingana na Hegel (1971) msingi wa nadharia hii ni usimulizi ambao unajikita katika kusimulia matukio kama yanavyoonekana katika ulimwengu halisi na sharti matukio haya yajikite katika ukweli. Anaendelea kusema kuwa ukweli hauwezi kuwepo ikiwa hakuna mandhari ambayo yanaonekana kwani huwa yana umuhimu mkubwa katika kuelezea uhalisia. Anasisitiza kuwa ukweli huhitaji uwazi na ni kile tu ambacho kinafahamika katika maisha ya binadamu.

Hegel (1971) anauona ulimwengu mzima kama unaoeleweka kwa kuelezea na kusimulia mawazo ya kweli ambayo yanapatikana katika ulimwengu wa kihalisia. Anaiona kazi ya kifasihi kama isiyo ya kiasilia bali inayotokana na shughuli za kibinadamu ambazo hufanywa kila siku. Hivyo basi uhalisia unasisitiza na kutilia mkazo uwasilishaji wa matukio ya kweli na kama yanavyotokea katika jamii anamoishi mtunzi wa kazi za kifasihi. Waandishi wanaochukua mtazamo huu wa uandishi, wanastahili kuchora taswira za mandhari, maudhui na wahusika kama zinavyoonekana katika jamii anamoishi. Hii ni kwa sababu fasihi ni kioo cha jamii na ndiposa mwandishi anatilia mkazo wahusika, mandhari na maudhui yanayopatikana katika maisha ya kawaida ya jamii anamoishi. Wamitila (2002), anasema kuwa uhalisia ni mkondo unaosisitiza usawiri wa matukio au maisha katika fasihi kama yalivyo katika maisha ya kila siku. Kauli hii ya Wamitila inashabihiana na kauli ya Mohamed (1995) anayesema kuwa, uhalisia sharti uwe na wingi wa ukweli. Hata hivyo, ukweli anaosisitiza Mohamed, ni ukweli wenye kumaanisha hali ya uyakinifu na matukio yanayokubalika kimantiki. Hivyo basi, kulingana na wasomi hawa wawili uhalisia sharti uzungumzie kuhusu ukweli wa matukio ambayo yanawakumba wanajamii

katika maisha yao ya kawaida. Wamitila (2003) anaunga mkono mawazo ya Hegel (1971) kwamba msimulizi husimulia mambo ya kweli yanayopatikana katika ulimwengu wa kihalisia anaposema kuwa kigezo cha kimsingi katika uhalisia ni hali ya kujifunga kwenye wahusika wa kawaida au wanaoweza kupatikana katika jamii halisi na wanavyoingiliana na mandhari na mazingira yao ya kawaida.

Mawazo ya Ntarangwi (2004) yanaoana na ya Wamitila (2003) anaposema kuwa, nadharia hii inahusu usawiri wa mambo ya kihalisia katika fasihi. Mwandishi wa kihalisia huamini mambo ya ukweli ambayo yanaweza kuonekana na kuthibitishwa. Ntarangwi anashikilia kuwa msanii anapaswa kuandika kuhusu masuala ambayo yanawahusu watu katika hali halisi za maisha. Hivyo basi uhalisia sharti ujikite katika matukio ambayo yanaweza kuthibitika katika jamii. Naye Mcdougal (2009) anasema kuwa uhalisia katika fasihi unarejelea uandishi ambao unaonyesha maisha ya ukweli ambayo yamesawiriwa kwa usahihi na kwa undani. Mcdougal anaendelea kusema kuwa uhalisia hujishughulisha na masuala ambayo yanaikumba jamii katika kipindi fulani cha wakati. Masuala haya huwa ni ya kijamii kama vile: athari za teknolojia ya kisasa na athari za watu kuhamia mijini. Anaendelea kusema kuwa waandishi wa kihalisia huangazia migogoro na mivutano ya kitabaka katika jamii kama vile uongozi na ndoa. Kutokana na wataalamu hawa tunaweza kudai kuwa, fasihi huwa ni zao la jamii na huibuka kutokana na mazingira anamoishi binadamu. Hivyo basi, sharti fasihi iweze kuakisi mambo ambayo yanaikumba jamii katika maisha yao ya kawaida kwani fasihi ni kioo cha jamii na husawiri jinsi jamii ilivyo katika uyakinifu na ukamilifu wake.

#### 1.6.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Uhalisia na Michango yake

Msimulizi husimulia kuhusu masuala ambayo yanawahusu watu katika hali halisi ya maisha. Kwa mfano katika diwani *Bara Jingine* (Mberia, 2001: 55) katika shairi ‘Jinamizi’, mtunzi anaonyesha jinsi watu wanavyochangia katika shughuli za ukataji wa miti ili wapate mbao na ardhi ya kulima. Matokeo yake ni kuacha ardhi ikiwa wazi na wakati wa mvua mchanga wote unabebwa hali inayochangia mmomonyoko wa udongo. Mhimili huu umetuongoza katika kubainisha madhara mengine yanayohusishwa na uharibifu wa mazingira katika *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga.*

Msanii huwasilisha maisha ya jamii kwa uwazi na usahihi. Mtunzi huwasilisha mambo ambayo yanaonekana katika jamii anamoishi. Kwa mfano katika diwani *Bara Jingine* (Mberia, 2001: 63) katika shairi 'Mimi Mto Nairobi' msimulizi anaonyesha jinsi wakazi wa Nairobi wanavyouharibu mto Nairobi kwa kutupa mafuta, makopo, tairi na takataka. Binadamu anafanya hivi licha ya kuwa ndiye anayefaidika na maji haya. Pia anaharibu ekolojia kwani kuna mimea na wanyama wengine ambao wanategemea maji ya mto huu. Mhimili huu umetusaidia katika kubainisha athari za mtagusano kati ya jamii na mazingira katika *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga.*

Mwandishi anastahili kusawiri wahusika, matukio na mandhari yanayokubalika na kuaminika katika jamii ya wakati wake. Kwa mfano katika diwani *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014: 35) shairi 'Wanda' msimulizi anaonyesha athari za mafuriko baada ya binadamu kuhitilafiana na ekolojia. kwa mfano ukataji wa miti na ufugaji wa wanyama wengi. Mafuriko haya yanaathiri maisha ya binadamu na wanyama wengine na jinsi ufugaji wa wanyama wengi kiholela unavyoathiri ardhi na kusababisha mmomonyoko wa udongo. Mhimili huu umetuelekeza katika kuangazia na kubainisha matukio ambayo yanaathiri mfumo wa ekolojia katika *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga.*

Mtunzi hutumia mandhari ya kawaida ambayo husawiri usahihi na utamaduni wa jamii anamoishi na kuangazia matatizo yanayoikumba jamii kila siku na kupendekeza njia ya kuyatatua. Kwa mfano, mabadiliko ya hali ya anga ambayo huweza yakaathiri mifugo na mimea. Kwa mfano katika shairi *Rangi ya Anga* ( Mberia, 2014: 12) mtunzi anaonyesha jinsi haki za watoto wa kike zinavyokiukwa kwa mfano, ukeketwaji, ndoa za mapema, ubakaji na kadhalika. Mhimili huu umetuongoza katika kubainisha jinsi mabadiliko ya kitamaduni yanavyoathiri mifumo ya ekolojia jamii katika diwani za *Bara Jingine* na Rangi *ya Anga*.

### 1.6.2 Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia

Nadharia hii inahusishwa na mwanasaikolojia Bronfenbrenner (1917-2005) aliyezaliwa nchini Marekani lakini mwenye asili ya Kirusi. Msomi huyu anajulikana sana kwa kuweka misingi katika Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia. Bronfenbrenner (1989) anasema kuwa Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia ni mtazamo unaotumika kuelezea maendeleo ya binadamu ambayo yanahusisha utafiti wa kisayansi kuhusu mwingiliano kati ya binadamu na mazingira anamoishi.

(TY). Kwa hivyo mfumo huu wa ekolojia huonyesha uhusiano, upatano na mwingiliano kati ya binadamu na binadamu mwenzake, wanyama na hata mimea katika mazingira fulani maalum. Kulingana na nadharia hii, binadamu ndiye hujenga mandhari ambayo huchangia katika maendeleo yake ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, tofauti na viumbe vingine vyote. Hii ni kwa sababu binadamu ni kiumbe razini na matendo yake huathiri viumbe na vitu vyote ambavyo vimemzingira kwa mfano, mito, milima, uchafuzi wa hali ya hewa na utamaduni wa jamii, hali ambazo hufanya maisha ya binadamu yaathiriwe. Bronfenbrenner (1989) anaendelea kusema kuwa maisha ya binadamu yamebadilika kutokana na jinsi ambavyo amepiga hatua mbele kiteknolojia kwa muda wa miongo miwili iliyopita. Teknolojia hii imeongezea maarifa ambayo tayari yapo na kugundua maarifa mengine ambayo hayakuwa yanajulikana hapo awali. Maarifa haya mapya ya kiteknolojia yameweza kubadilisha mifumo ya kijamii kwa kiasi kikubwa. Nadharia hii inashikilia kuwa mabadiliko mengi ya kijamii, kiuchumi na hata kisiasa ambayo yametokea katika mfumo huu wa kiutandawazi yameathiri mazingira anamoishi binadamu hali ambayo imebadilisha maisha yake.

Bronfenbrenner na wenzake (1994) wanasema kuwa nadharia hii ya Mfumo wa Ekolojia hubadilikabadilika kulingana na jinsi binadamu anavyopiga hatua za kimaendeleo. Hii ni kwa sababu maendeleo ya binadamu katika uwanja wa kiteknolojia husababisha mabadiliko ya kimazingira na mifumo ya kijamii. Mabadiliko haya huathiri kizazi kimoja hadi kingine. Hivyo basi baada ya jamii kugundua kwamba mchakato wa maendeleo unaathiri mabadiliko ya kimazingira na mifumo ya kijamii ni muhimu sera za kijamii ziwekwe ili kuweza kuyahifadhi mazingira inamoishi. Kutokana na mawazo haya ya Bronfenbrenner ni wazi kuwa mchakato wa maendeleo ya binadamu umechangiwa na mwingiliano kati ya binadamu na mazingira anamoishi. Maendeleo haya huathiriwa na vitu au viumbe ambavyo vinamzingira binadamu kwa mfano, wazazi, marafiki, utamaduni, shule na kadhalika.

#### 1.6.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia na Michango yake

Mihimili ya nadharia hii huonyesha jinsi binadamu anastahili kuhusiana na kuingiliana na mandhari yake na mchango wa mandhari haya katika kuboresha maendeleo yake ili aweze kujiepusha kwa mfano na magonjwa ambayo yanaweza kumkumba kutokana na uchafuzi wa mazingira. Kwa mfano katika diwani *Bara Jingine* (Mberia, 2001: 55) katika shairi ‘Jinamizi’ mwandishi anaonyesha jinsi binadamu anavyoathirika kutokana na magonjwa mbalimbali kama

vile kipindupindu yanayosababishwa na mafuriko makubwa yanayotokea baada ya kukata miti na kufuga idadi kubwa ya wanyama. Mafuriko haya hata yanachangia vifo vya binadamu na wanyama. Mhimili huu umetusaidia katika kuchunguza jinsi mabadiliko ya ekolojia jamii yanavyoweza kuathiri maisha ya binadamu katika *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga.*

Nadharia hii huonyesha jinsi tabia na utamaduni wa kijamii huchangia katika kuathiri maendeleo ya kiuchumi na kijamii kutokana na mali asili na mifumo mipya ya kiteknolojia. Kwa mfano katika diwani *Bara Jingine* (Mberia, 2001: 43) katika shairi 'Wanabiashara Barabarani' mtunzi anaonyesha jinsi wanawake wanajiingiza katika ukahaba kwa sababu ya umaskini. Wanawake hawa huishia kudhulumiwa na wateja wao kwani hata huwa hawalipwi baada ya kuwahudumia. Jambo ambalo husababisha wanawake hawa kujiingiza katika biashara hii ya ukahaba ni hali ngumu ya kimaisha. Mhimili huu umetuwezesha kubainisha jinsi mifumo ya ekolojia jamii inavyobadilika kutokana na binadamu kuingiliana na tamaduni mbalimbali katika *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga*

Maendeleo katika jamii huathiriwa na vitu au viumbe ambavyo vinaizingira jamii kwa mfano: wazazi, marafiki, taasisi za elimu, utamaduni na kadhalika. Kwa mfano katika shairi *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014: 6) mtunzi anaonyesha jinsi wazazi wanavyowalazimisha watoto wao kukeketwa. Pia mtunzi anaonyesha jinsi mfumo wa kijamii unavyombagua mtoto wa kike. Kwa mfano tunaarifiwa kuwa mtoto wa kike hastahili kurithi mali yoyote katika jamii. Mhimili huu umetuwezesha kubainisha jinsi mfumo wa ekolojia jamii unavyoathiriwa na masuala mbalimbali ya kijamii.

### 1.7.0 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Ushairi ni utanzu ambao umeangaziwa na wasomi mbalimbali. Hata hivyo, kilichoangaziwa sana ni fani na maudhui. Kazi ya kuhusisha ushairi na mfumo wa ekolojia kwa uelewa wangu bado haijashughulikiwa na wahakiki wengi. Ni wazi kwamba wataalamu wengi wamezungumzia kuhusu ushairi na kutoa maoni yao ambayo yana manufaa mengi katika uchunguzi wowote wa ushairi. Katika sehemu hii tumeangazia mapito ya machapisho ambayo yameandikwa kuhusiana na mfumo wa ekolojia. Kwanza tumeangazia kuhusu ushairi na fasihi kwa jumla, kisha tumejifunga katika diwani za *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014). Vilevile tumeangazia yale ambayo yameandikwa kuhusiana na masuala ya kijamii, kisiasa na

kiuchumi ili kuweza kujenga mjadala wa utafiti wetu. Hii ni kwa sababu utafiti huu ulilenga kuonyesha athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia. Pia tulinuia kuonyesha athari za masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwenye mfumo wa ekolojia jamii.

### 1.7.1 Ushairi na Fasihi kwa Jumla

Harries (1962) anauona ushairi kama taaluma ambayo ni kamilifu katika kueleza ukweli wa maisha katika jamii husika. Raffel (1984) anatilia kauli hii mkazo kwa kusema kuwa, ukamilifu wa ushairi hutegemea mtindo anaoutumia mshairi katika kutunga kazi yake. Waandishi tofauti huweza kutofautiana kimtindo, wanapoandika kazi zao. Mawazo haya ya wasomi hawa wawili yametuwezesha kuchunguza jinsi binadamu anavyoingiliana na mfumo wa ekolojia na jinsi unavyojidhihirisha katika *Bara Jingine* ( Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* ( Mberia, 2014).

Ngari (1998) anaangazia jinsi Mberia anatetea haki za wanyonge na jinsi wafanyakazi wanadhulumiwa katika diwani ya *Mchezo wa Karata*. Ngari pia anaangazia jinsi tamathali za semi kama vile: tashbihi, takriri na maswali ya balagha zinavyoendeleza maudhui kuhusu matatizo yanayowakumba wanajamii katika jamii husika. Pia anaangazia jinsi Mberia anavyosawiri jamii, ambayo inamkandamiza mwananchi wa kawaida. Utafiti huu umetusaidia kuyafahamu mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii yanayoathiri mfumo wa ekolojia. Hata hivyo, utafiti wetu unatofautiana na wake, kwani hatukujikita katika mtindo, bali tumeangazia jinsi mfumo wa ekolojia unavyoathiriwa kutokana na mtagusano baina ya wanajamii kupitia utambulishaji wa mandhari na uwasilishaji wa maudhui katika *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga.* (Mberia, 2004). Pia hatujashughulikia matumizi ya lugha kama alivyofanya Ngari (1998).

King'ei na Kimoli (2001) wanadai kuwa ushairi ni zana mwafaka ambayo humwezesha mtunzi kufumbata hali ya maisha katika maneno machache yaliyofinyangwa kisanaa. Kwa hivyo mtunzi hutumia maneno machache yaliyofumbata ujumbe maalum ili kuangazia maisha ya binadamu. Kazi hii ya King'ei na Kimoli imetufaa katika kuchagua mashairi ambayo yanaakisi mabadiliko ya ekolojia kutokana na shughuli za kibinadamu katika diwani teule. Tofauti na uchunguzi wao utafiti wetu umejikita katika kuchunguza athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia kupitia utambulishaji wa mandhari na uwasilishaji wa maudhui ya kiuchumi, kijamii na kisiasa katika diwani za *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014)

Kobia (2007) anaonyesha jinsi viongozi waliochaguliwa na kupewa jukumu la kutunza mazingira wanavyoyaharibu kwa manufaa yao binafsi. Anaonyesha jinsi mawaziri ambao wana majukumu ya kuona kwamba miti hasa ya kiasili inalindwa na kutunzwa vyema kwa sababu ndio huwapa wanajamii hewa safi, kuvuta mvua na hata kuzuia mmomonyoko wa udongo ndio wako mstari wa mbele kuchangia katika uharibifu wa misitu. Viongozi hawa wanawaruhusu wananchi kuchoma makaa na kupasua mbao kisha wanawapa kitu kidogo. Hali hii inachangia ukataji wa miti ya kiasili suala ambalo linasababisha mito na maziwa kukauka na mvua kupungua. Matokeo yake ni kuwa ukame unaongezeka, mimea inakauka na mifugo inakosa malisho. Baadaye mifugo hawa wanaanza kuangamia mmoja mmoja nao wanajamii wanaanza kuangamia kwa sababu ya ukosefu wa chakula. Suala hili linaathiri jamii kiuchumi kwani wanabakia wakiwa maskini hohehahe na kuanza kuomba chakula katika nchi jirani.

Kobia (2007) anaendelea kuonyesha jinsi jamii inavyokumbwa na ukame baada ya kukata miti ovyoovyo. Tunaarifiwa kuwa mito inaendelea kukauka kwa sababu ya uhaba wa maji nao wanyama pamoja na binadamu wanaendelea kufa. Janga hili la ukame linaathiri mifumo ya kijamii kwani tunaarifiwa kuwa hata wanawake wanaanza kusengenyana kuwa waume zao wanashindwa kutekeleza wajibu wao wa ndoa. Kazi hii imetufaa kwani ilitupa mwanga kuhusu matatizo ambayo jamii hukumbana nayo baada ya kuhitilafiana na ekolojia. Pia imetusaidia katika kuangazia jinsi jamii huathirika kiuchumi baada ya kuharibu mazingira inamoishi. Kazi hii ni tofauti na yetu kwani utafiti wetu umejihusisha katika kuchunguza athari za mtagusano baina ya jamii na ekolojia kupitia utambulishaji na uwasilishaji wa mandhari na maudhui katika *Bara Jingine* (Mberia, 2001 ) na *Rangi ya Anga* ( Mberia, 2014).

Kezilahabi (2008) anazungumzia kuhusu athari ya mafuriko ambayo yanawakumba wanajamii katika diwani ya *Dhifa.* Anasema kuwa mafuriko haya yanasababisha hasara kubwa kwa wakulima ambao wanalima kwa bidii kisha mimea yao inaharibiwa na mafuriko. Maisha ya binadamu pia yanaathirika kwani tunaarifiwa kuwa nyumba kongwe zilizoko mabondeni na ambazo hazina nguvu ya kujisetiri zinabebwa na maji ya mafuriko. Mafuriko haya hata yanaangamiza wanajamii suala ambalo linasababisha wahamie maeneo salama. Pia yanasababisha miti ya umeme kuanguka hali ambayo inachangia nguvu za umeme kupotea na kuacha eneo zima likiwa giza. Hali hii ni hatari kwani miti hii ya umeme ikianguka inahatarisha maisha ya binadamu na hata wanyama wanaoishi maeneo haya. Baada ya mafuriko kunazuka

upepo mkali ambao unasababisha miti kuangukia nyumba za wakazi wa maeneo haya. Upepo huu unahatarisha maisha ya wanajamii kwani uvumapo hata huwa hawalali nyumbani mwao kwa kuhofia kuangamizwa. Kulingana na Kezilahabi (2008) ni kuwa mafuriko haya yanaathiri jamii kiuchumi kwani yanasababishia wenyeji hasara ambayo inaathiri hata vizazi vijavyo. Mafuriko haya pia yanaathiri mfumo wa ekolojia kwani yanasababisha kuanguka kwa miti mikongwe ambayo ni ya kiasili jambo ambalo linasababisha mmomonyoko wa ardhi na kuharibiwa kwa makazi ya baadhi ya wanyama. Kazi hii ya Kezilahabi imetusaidia katika kuangazia jinsi mifumo ya kijamii inavyoathiriwa kutokana na mabadiliko ya ekolojia jamii. Pia imetusaidia kubainisha jinsi jamii huathirika kiuchumi baada ya ekolojia kuharibiwa. Kazi yetu imetofautiana na hii ya Kezilahabi kwani sisi tumejikita katika diwani ya *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* ( Mberia, 2014).

Wamitila (2008) anazungumzia kuhusu jinsi meli zinazosafirisha mafuta zinavyochafua maji baharini. Mafuta haya yanaharibu ekolojia kwani yanapopenyeza majini yanaathiri wanyama ambao wanaishi humo. Pia mimea ambayo inapatikana baharini inakufa kwa sababu ya ukosefu wa hewa safi. Suala hili linaathiri jamii kiuchumi kwani baadhi ya wanajamii wanategemea maji haya ya baharini kujipatia riziki. Kwa mfano, wengi hujihusisha na kazi ya kuvua samaki ili waweze kujikimu kimaisha na ikiwa kazi yenyewe haipo basi wanajamii wanajihusisha na mambo mengine kama vile uhalifu na ukahaba ili waweze kujikimu kimaisha. Kutokana na kazi hii ya Wamitila ni wazi kuwa binadamu akihitilafiana na mazingira basi jamii huweza kuathirika kiuchumi na kijamii. Wamitila (2008) pia anaonyesha jinsi binadamu na wanyama wanavyoathirika kutokana na upungufu wa mvua hali inayosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi ulimwenguni. Mabadiliko haya yanasababishwa na watu kukata miti ya kiasili kiholela na kuchafua mazingira. Kazi hii ya Wamitila imetuwezesha kuchunguza jinsi mahusiano ya ekolojia yanavyoathiri mazingira. Kazi hii inatofautiana na yetu kwani sisi tumejikita katika diwani ya *Bara Jingine* ( Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014) tofauti na Wamitila ambaye anaeleza mawazo yake kwa muundo wa riwaya.

Kanyua (2013) anaonyesha jinsi mtindo unavyoendeleza maudhui katika tamthilia ya *Natala*. Katika uchunguzi wake, anaonyesha jinsi Mberia anavyotumia mbinu tofautitofauti za lugha katika ujenzi na uendelezaji wa ukombozi wa mwanamke katika jamii. Uchunguzi huu umetuwezesha kuelewa kazi za Mberia na masuala ya ekolojia jamii anayosimulia katika kazi

zake. Vilevile umetuwezesha kubainisha jinsi masuala ya kijamii yanavyoingiliana na kuathiri mfumo wa ekolojia jamii katika diwani za *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga*. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwani tumejikita katika diwani mbili za ushairi za Mberia. Pia Kanyua anaongozwa na Nadharia ya Ufeministi katika uchunguzi wake ilhali katika uchunguzi wetu tunaongozwa na mihimili ya Nadharia ya Uhalisia na Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia. Utafiti wetu pia haujajikita katika mtindo bali unajikita katika kuchunguza athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia kupitia uwasilishaji wa mandhari na uwasilishaji wa maudhui huku tukirejelea diwani za *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014).

Mwangi (2013) anaangazia uhalisia na uhalisia ajabu katika riwaya mpya za Kiswahili. Katika utafiti wake, anachunguza jinsi uhalisia na uhalisia ajabu unavyojidhihirisha kupitia kwa wahusika na mandhari. Mwangi katika utafiti wake anaonyesha mpaka uliopo kati ya uhalisia na uhalisia ajabu. Utafiti huu umetufaa katika kuamua mabadiliko ya kijamii ambayo yanaathiri mifumo ya ekolojia na yanaweza kuonekana na kuthibitika huku tukielekezwa na mihimili ya Nadharia ya Uhalisia. Tofauti kati ya utafiti wake na wetu ni kwamba, yeye anajikita katika utanzu wa riwaya, ilhali sisi tumejikita katika utanzu wa ushairi. Vilevile Mwangi anaongozwa na Nadharia ya Uhalisia na Uhalisia Ajabu katika kuchunguza vipengele vya mandhari na wahusika ilhali sisi tumeongozwa na Nadharia ya Uhalisia na Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia katika kuchunguza jinsi athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia katika *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014).

Waweru (2014) anaangazia fani katika tamthilia za Mberia. Katika utafiti wake, Waweru anajikita katika tamthilia tatu za Mberia: *Natala*, *Kifo Kisimani* na *Maua Kwenye Jua la Asubuhi*. Katika uchunguzi wake anaonyesha jinsi wahusika, matumizi ya lugha na mandhari yanavyotumika katika kusawiri maudhui ya kijamii na kiuchumi. Utafiti huu umetufaa hasa katika kuamua ni yepi masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Pia umetusaidia katika kufahamu ni vipi mfumo wa ekolojia jamii unavyoathiriwa na masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa katika *Bara Jingine* (Mberia, 2002) *na Rangi ya Anga*.(Mberia, 2014). Tofauti ya utafiti huu na wetu ni kwamba Waweru amejikita katika utanzu wa tamthilia ilhali sisi tunajikita katika utanzu wa ushairi huku tukirejelea diwani za *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga*. Pia tofauti na Waweru hatutashughulikia fani bali tunaangazia athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia katika *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014).

Nabeta na Ongutte (2014) wanasema kuwa kuna kazi za Kiswahili kama vile: *Nakuruto* (Momanyi, 2009) na *Kifo Kisimani* (Mberia, 2001) ambazo zinaangazia kuhusu mabadiliko ya hali ya anga na uharibifu wa ekolojia kwa jumla. Wanasema kwamba baadhi ya masuala ambayo yanaathiri mfumo wa ekolojia jamii ni pamoja na: uongozi mbaya, ukataji wa miti kiholela, unyakuzi wa ardhi yenye chemichemi za maji na nafasi ya mwanamke katika kuhifadhi mazingira. Kutokana na uharibifu huu wa ekolojia, jamii inashindwa kushughulikia kilimo, binadamu na wanyamapori wanakufa kwa sababu ya kiangazi suala ambalo linachangia wanadamu kuhamia katika mataifa ambayo hayajaathiriwa sana na mabadiliko ya tabia nchi. Wanaendelea kusema kuwa ili kuzuia kadhia hii ya uharibifu wa ekolojia viongozi wa kisiasa lazima waweke mikakati madhubuti ya kulinda ekolojia na kuelimisha umma kwa jumla kuhusu umuhimu wa kuhifadhi ekolojia. Wanadai kuwa masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi yanaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa kiasi kikubwa.

Isitoshe, wanaelezea jinsi ekolojia inavyoharibiwa katika riwaya *Bustani ya Edeni* (Mbogo, 2002). Wanaonyesha jinsi uharibifu wa mazingira unavyotokea katika sehemu za pwani katika nchi ya Tanzania. Vilevile wanabainisha matatizo yanayosababishwa na kiwanda cha Sagasaga, pale ambapo wafanyakazi wanaugua kwa sababu ya kufanya kazi bila glovu. Maji taka na kemikali zinazotoka katika kiwanda hiki zinaelekezwa katika mto Zamala na kuangamiza mimea na wanyama. Hali hii inaathiri wanajamii wanaotumia maji haya kwa kuoga, kunywa na hata kuosha nguo. Matokeo yake ni wakazi wa eneo hili kuambukizwa ugonjwa wa kansa kutokana na kemikali kali zinazotoka katika kiwanda hiki cha Sagasaga.

Vilevile wakirejelea tamthilia ya *Kifo Kisimani* (Mberia, 2001) wanaonyesha jinsi uongozi mbaya unavyochangia katika uharibifu wa mfumo wa ekolojia jamii. Wanasema kuwa Mberia anaonyesha jinsi viongozi walio mamlakani wanavyoharibu ekolojia kwa sababu ya manufaa yao wenyewe. Wanatumia raslimali zinazozalishwa na ekolojia ili waweze kusalia mamlakani. Kwa mfano, wananyakuwa ardhi ambayo imetengewa shughuli za umma kama vile viwanja vya kuchezea watoto. Wanaonyesha jinsi utawala mbaya wa Butangi unavyoathiri ekolojia. Viongozi wa kisiasa wanalima sehemu yoyote ile na kufuga idadi kubwa ya mifugo mahali popote pale bila kujali kanuni za kuhifadhi ardhi. Matokeo ya hali hii ni rutuba ya udongo kuharibiwa na wanajamii kukumbwa na janga la njaa na hatimaye kuangamia. Pia wananchi wanachangia katika ukataji wa miti kiholela, suala linalochangia kukauka kwa chemichemi za maji. Wasomi

hawa wanadai kuwa kukauka kwa mito na chemichemi za maji si suala la kiasili bali nikutokana na viongozi ambao hawajawajibika. Hili ni kweli kwa sababu maeneo kama vile msitu wa Mau nchini Kenya, serikali haichukui hatua kali katika kukabiliana na watu wanaoharibu ekolojia ya msitu huu. Taasisi za serikali ambazo zimepewa majukumu ya kutekeleza sera za kuhifadhi ekolojia zimekashifiwa kwa sababu ya kujihusisha na ufisadi na kuachilia wanajamii wauharibu msitu huu wa Mau kwa kuchoma makaa na kupasua mbao (Letiwa, 2018). Utafiti huu wa Nabeta na Ongutte umetusaidia katika kuelewa dhana ya mfumo wa ekolojia na jinsi unavyoathiriwa na wanajamii. Hata hivyo utafiti wetu unatofautiana na wao kwani wanajikita katika *Nakuruto* (Momanyi, 2009) *Kifo Kisimani* (Mberia, 2001) ilhali utafiti wetu umejikita katika diwani ya *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014).

Sabula (2014) ameangazia nafasi ya mwanamke katika uhifadhi wa mazingira katika riwaya ya *Nakuruto* (Momanyi, 2009) huku akijikita katika mtazamo wa ufeministi wa kiekolojia. Katika utafiti wake Sabula anaongozwa na mihimili ya nadharia ya Ufeministi wa Kiekolojia. Katika utafiti wake anaonyesha nafasi na mchango wa Ufeministi wa kiekolojia katika fasihi ya Kiswahili. Vilevile anaonyesha juhudi za Nakuruto kama mhusika wa kike katika hali ya kupigania uhifadhi wa mazingira. Isitoshe, katika ufafiti wake anaonyesha kuwa ufeministi wa kiekolojia una mchango mkubwa katika kuwazindua wanawake ili kuleta ukombozi wa mazingira. Ameonyesha jinsi mhusika Nakuruto anavyoelimisha jamii kuhusu athari za mabadiliko ya anga na jinsi wanavyoweza kujinasua kutokana na hali hii. Pia anaonyesha jinsi mwanamke anavyo dhulumiwa na kudhihakiwa anapojaribu kujihusisha na harakati za uhifadhi wa mazingira. Pia amebainisha jinsi masuala kama vile umasikini, kukauka kwa chemichemi za maji, maradhi na mauti yanavyosababishwa na uharibifu wa mazingira. Utafiti huu umetusaidia katika kubainisha aina za mazingira na jinsi yanavyoathiriwa na mtagusano kati ya jamii. Hata hivyo utafiti wetu ni tofauti na wake kwani anaongozwa na Nadharia ya Ufeministi wa Kiekolojia ilhali utafiti wetu umeongozwa na Nadharia ya Uhalisia na ya Mfumo wa Ekolojia. Vilevile tofauti na Sabula ambaye amejikita katika riwaya ya *Nakuruto* (Momanyi, 2009), utafiti wetu umejikita katika diwani *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014).

Mogeni (2015) anashughulikia fani na maudhui katika Gazeti la *Taifa Leo.* Kulingana na uchunguzi wake, ameweza kuonyesha matukio na masuala ambayo husababisha maisha ya binadamu kubadilikabadilika kila siku. Anaonyesha jinsi jamii inavyoathirika kisiasa, kiuchumi

na kijamii. Pia anaonyesha jinsi mifumo ya kiteknolojia inavyoathiri maisha ya binadamu huku akirejelea ushairi wa magazetini. Utafiti huu umetufaa katika kuangazia matukio na masuala ambayo yanaathiri mifumo ya ekolojia jamii kwa sababu ya mabadiliko ya kiteknolojia . Tofauti na Mogeni (2015) utafiti wetu haujajikita katika mashairi ya Gazeti la *Taifa Leo*, kama alivyofanya bali tumejikita katika *Bara Jingine* ( Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* ( Mberia, 2014) Pia tofauti na Mogeni (2015) ambaye aliongozwa na Nadharia ya Mtindo, utafiti wetu umeongozwa na Nadharia ya Uhalisia na ya Mfumo wa Ekolojia.

Nasimiyu (2016) anaangazia jinsi mazingira ya kijamii na kihistoria yanavyoathiri uwasilishaji wa maudhui katika diwani ya *Dhifa* (Kezilahabi, 2013). Katika utafiti wake, Nasimiyu anabainisha jinsi maudhui ya kisiasa na kijamii yanavyojitokeza katika mazingira ya kihistoria na kijamii huku akirejelea diwani ya *Dhifa*. Utafiti huu unajikita katika mandhari ya nchi ya Tanzania. Utafiti huu umetufaa katika kuelewa na kubainisha jinsi mabadiliko ya kijamii kama vile familia, elimu na utamaduni yanavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii. Pia umetusaidia katika kuelewa athari za mabadiliko ya ekolojia kwenye mifumo ya kijamii katika mataifa mengine. Nasimiyu anaongozwa na Nadharia ya Simiotiki katika utafiti wake ilhali utafiti wetu umeongozwa na Nadharia ya Uhalisia na Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia. Pia tofauti na Nasimiyu anayerejelea diwani ya *Dhifa*, sisi tumejikita katika diwani ya *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2004).

Kibaru (2016) anaangazia taashira ya mazingira katika diwani za *Sauti ya Dhiki* na *Msimu wa Tisa*. Katika utafiti wake, Kibaru anaangazia maudhui ya kijamii, kisiasa na kiuchumi na jinsi ambavyo mazingira yanaathiri jamii katika maisha yao ya kawaida. Kibaru anabainisha kwamba mazingira yana mchango mkubwa katika kuendeleza maudhui katika kazi husika. Utafiti huu umetusaidia katika kubainisha jinsi masuala ya kijamii, kiuchumi yanavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii. Katika utafiti wetu, tunarejelea diwani za *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014), tofauti na Kibaru ambaye amejikita katika diwani za *Sauti ya Dhiki* na *Msimu wa Tisa*. Pia tumeongozwa na Nadharia ya Uhalisia na Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia tofauti na Kibaru ambaye aliongozwa na Nadharia ya Simiotiki.

Warutere (2018) anasema kuwa ajenda muhimu katika nchi ya Kenya ambayo inastahili kupewa kipaumbele ni kuhusu utunzaji wa mazingira ambayo anayaona kama msingi wa kuwapa wanajamii chakula, usalama, afya na maendeleo ya kiuchumi. Anasema kuwa mojawapo ya

changamoto inayowakumba wakenya ni jinsi ya kuhifadhi misitu ambayo imeharibiwa miaka mingi iliyopita kutokana na usimamizi mbaya. Huku kauli ya ulimwengu ikiwa ni kupanda miti, Kenya inaendelea kukata miti ili kutimiza mahitaji ya kuni, makaa na kilimo. Mazingira ambayo yamehifadhiwa vyema huwapa wanajamii chakula, afya nzuri, makazi mazuri na hata ukuaji na ueneaji wa viwanda, suala ambalo huchangia katika kubuni nafasi za kazi na kuinua jamii kiuchumi. Ili kutimiza hali hii, serikali lazima iweke mikakati na sera mwafaka ili iweze kukabiliana na watu wanaokata miti kiholela. Ni wajibu pia wa serikali kuhamazisha umma kuhusu madhara ambayo yanaletwa na uharibifu wa mazingira. Umma sharti ufahamishwe kuhusu umuhimu wa miti ambayo huwapa gesi ya oksijeni, mvua na pia huzuia mmomonyoko wa udongo. Kazi hii ya Warutere (2018) ilitusaidia katika kuelewa jinsi wanajamii wanavyoathirika wakihitilafiana na ekolojia. Utafiti wetu unatofautiana na kazi hii kwani tunajikita katika diwani ya *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014).

### 1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga*

Nzuki (2003) anaangazia mwingiliano wa fani na maudhui katika ushairi wa Mberia. Nzuki, anajikita katika diwani mbili za Mberia: *Mchezo wa Karata* na *Bara Jingine*. Katika utafiti wake, Nzuki anaonyesha jinsi mtindo unavyoendeleza maudhui kama vile: siasa, mazingira, utamaduni na dhuluma za kimapenzi katika diwani hizi. Katika uchunguzi wake, Nzuki pia anaonyesha jinsi Mberia anavyotumia tamathali za semi kama vile: tashbihi, sitiari na kinaya kuendeleza ujumbe wake. Ili kufaulisha uchunguzi wake, Nzuki anaongozwa na Nadharia ya Kisosholojia katika kuangazia maudhui na Nadharia ya Kimuundo katika kuangazia mtindo. Utafiti huu umetusaidia katika kuangazia jinsi mfumo wa ekolojia jamii unavyoathiriwa na masuala ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hata hivyo, tofauti na uchunguzi wa Nzuki, utafiti wetu haujajikita katika mtindo na unaongozwa na Nadharia ya Uhalisia na Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia. Pia tunaangalia diwani ya *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014) ambayo hakuishughulikia.

Bertoncini (2010) anaangazia aina za maudhui yanayojitokeza katika ushairi wa Mberia katika diwani *Mchezo wa Karata* (1997) na *Bara Jingine* (2001) japo kwa muhtasari. Katika diwani *Mchezo wa Karata* (Mberia, 1997) Bertoncini anasema kuwa maudhui ya kisiasa na kijamii yanajitokeza kwa kiwango kikubwa. Ameonyesha mashairi yanayozungumzia kuhusu masuala ya kisiasa na kijamii. Vilevile katika diwani *Bara Jingine* (Mberia, 2001) Bertoncini ameyagawa

mashairi haya katika makundi matatu kimaudhui. Kuna yale yanayozungumzia kuhusu masuala ya kisiasa, kijamii na uhifadhi wa mazingira. Anaendelea kusema kwamba katika mashairi yanayozungumzia kuhusu masuala ya kijamii, Mberia anakashifu vitendo vya kidhuluma ambavyo wanatendewa wanawake. Vitendo hivi ni kama vile ubakaji wa wasichana wa shule suala ambalo huathiri maisha yao ya baadaye. Baadhi ya wasichana wanajihusisha na ukahaba kwa sababu ya umasikini. Bertoncini anaendelea kudai kuwa kuhusiana na mashairi yenye maudhui ya kisiasa, Mberia anaonekana akikashifu viongozi wanaotawala kwa njia ya udikteta na kujihusisha na ufisadi. Pia wanachangia katika vita vya kikabila ili waendelee kusalia mamlakani. Ili kufaulisha maudhui haya Bertoncini anaonyesha jinsi Mberia alivyotumia tamathali za lugha kwa upevu mkubwa. Utafiti huu wa Bertoncini umetusaidia katika kuamua ni mashairi yepi yanazungumzia kuhusu masuala ya kijamii na kisiasa. Hata hivyo tofauti na Bertoncini ambaye anaangazia diwani mbili za *Mchezo wa Karata* (Mberia, 1997) na *Bara Jingine* (Mberia, 2001), utafiti wetu umeangazia diwani mbili za Mberia *Bara Jingine* (2001) na *Rangi ya Anga* (2014) ambayo Bertoncini hakuangazia. Vilevile tofauti na Bertoncini ambaye ameangazia kuhusu matumizi ya tamathali za semi katika diwani hizi *Mchezo wa Karata* (Mberia, 1997) na *Bara Jingine* (Mberia, 2001), utafiti wetu umejikita katika uchunguzi wa athari ya mtagusano kati ya jamii na ekolojia katika *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014). Hatujagusia suala lolote kuhusiana na tamathali za lugha.

Gicuku (2011) anashughulikia jinsi maudhui ya ndoa yamesawiriwa katika ushairi wa Kezilahabi na Mberia. Anaonyesha jinsi watunzi hawa wanavyosawiri maudhui ya ndoa na changamoto ambazo zinaikumba asasi hii. Anaonyesha kuwa changamoto hizi zinasababishwa na mazingira ambamo binadamu anaishi. Pia anaonyesha kuwa misingi ya changamoto hizi, hutokana na mabadiliko ya mifumo ya kijamii. Utafiti huu umetufaa katika kuteua masuala ya kijamii na jinsi ambavyo yanaathiri mfumo wa ekolojia jamii. Tofauti yetu na utafiti wake ni kuwa yeye anajikita katika diwani ya *Kichomi* (Kezilahabi, 1974) , *Bara Jingine* ( Mberia, 2001) na *Msimu wa Tisa* (Mberia, 2007) ilhali utafiti wetu unajikita katika diwani ya *Bara Jingine* ( Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* ( Mberia, 2014). Pia tofauti na Gicuku anayeongozwa na nadharia ya Umuundo - Utekelezi sisi tunaongozwa na nadharia mbili ambazo ni Uhalisia na Mfumo wa Ekolojia.

Nyambura (2014) anashughulikia matumizi ya kinaya katika ushairi wa Mberia. Katika utafiti wake, anajikita katika diwani za *Bara Jingine*, (Mberia, 2001) *Redio na Mwezi* (Mberia, 2005) na *Msimu wa Tisa* (Mberia, 2007). Anaonyesha ni kwa nini Mberia anatumia kinaya katika diwani hizi. Pia anaonyesha jinsi Mberia ametumia kinaya katika kuendeleza maudhui mbalimbali. Utafiti huu umetusaidia kuielewa diwani ya *Bara Jingine* kwa kina na kubainisha baadhi ya masuala ya ekolojia jamii ambayo Mberia anayashughulikia katika diwani hii . Hii ni kutokana na sababu kuwa ametumia mandhari mbalimbali kusawiri mfumo wa ekolojia. Tofauti na utafiti wake ni kuwa utafiti wetu haujajikita katika matumizi ya kinaya katika diwani za Mberia bali unajikita katika kuangazia athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia kupitia utambulishaji wa mandhari na uwasilishaji wa maudhui katika diwani za *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014) ambayo Nyambura hakushughulikia katika utafiti wake.

Ongarora (2017) ameshughulikia maudhui katika ushairi wa Mberia. Katika utafiti huu anajikita katika diwani tano za Mberia: *Mchezo wa Karata* (1997), *Bara Jingine* (2001), *Redio na Mwezi* (2005), *Msimu wa Tisa* (2007) na *Rangi ya Anga* (2014). Katika uchunguzi huu Ongarora ameyagawanya mashairi haya ya Mberia kimaudhui. Amebainisha yale yanayosheheni maudhui ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na yanayohusu mazingira na masuala ya kihistoria. Kuhusiana na mashairi ambayo yanahusu siasa, Ongarora anasema kuwa Mberia anaonyesha namna nchi na wanasiasa wanavyoendesha shughuli za kisiasa. Suala hili ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Hii ndio kwa sababu Mberia katika mashairi yake anawashauri wananchi wawe makini sana hasa wanapowachagua viongozi wao. Katika mashairi haya yanayozungumzia kuhusu siasa, Mberia anakashifu uongozi mbaya kupitia kwa dhihaka na sitiari. Wakati huo huo anawahimiza wananchi wabadilishe hali ya kisiasa na jamii kwa jumla kupitia haki walizopewa na katiba kama wapiga kura.

Kuhusiana na masuala ya kiuchumi, Ongarora (2017) anasema kuwa Mberia anachora jamii iliyogawanywa katika matabaka kwa misingi ya utajiri, nguvu za kisiasa na elimu. Tabaka la juu lina fedha, uwezo na njia za kudhibiti nyenzo za kuzalisha mali. Watu wa tabaka la juu wanang'ang'ania kubaki mamlakani nao wa tabaka la kati wanakazana kupanda daraja la kiuchumi ili kuwafikia walio katika daraja la juu. Watu wa daraja la chini ambao hujumuisha maskini wanaajiriwa katika ofisi za serikali, makampuni ya kibinafsi na katika makazi ya matajiri. Wachochole hawa wanapokazania kutimiza mahitaji yao ya kimsingi wanadhulumiwa

na watu wa tabaka la juu na kati. Kwa upande mwingine nchi ambazo zimeendelea kiuchumi zinadhulumu nchi za ulimwengu wa tatu.

Kuhusiana na masuala ya kijamii Ongarora anasema kuwa Mberia anaangazia masuala anuai ambayo yanaathiri jamii. Anaangazia uigaji wa utamaduni wa kigeni ambao unaweza kuwa na athari hasi na chanya. Baadhi ya athari hasi ni kuwa vijana wanaathirika kwa kutazama filamu za ponografia na kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja. Pia anaonyesha jinsi Mberia anavyokashifu tamaduni ambazo zimepitwa na wakati kwa mfano, ukeketaji wa wasichana. Baada ya kukeketwa wasichana hawa wanaozwa kwa matajiri ili kuwanusuru wazazi wao kutokana na lindi la umasikini. Hatima ya wasichana hawa ni kuacha masomo na kuishia kuajiriwa kama wafanya kazi wa nyumbani. Isitoshe, anaonyesha jinsi wanawake wanavyonyimwa haki za kurithi ardhi. Wanapigwa na kudhihakiwa hasa kwa sababu ya kutojifungua watoto wa kiume. Hali hii inawanyima wanawake haki zao za kimsingi. Kwa hivyo anazikashifu tamaduni ambazo zinambagua mtoto wa kike na kukosa kumpa nafasi sawa na mwenzake wa kiume.

Vilevile Ongarora anasema kuwa Mberia katika diwani zake anasisitiza umuhimu wa kuhifadhi mazingira. Anaonyesha jinsi wanajamii wanavyoharibu mazingira kama vile misitu, chemichemi za maji, mimea na wanyama kwa jumla. Anaendelea kusema kuwa baadhi ya mashairi ya Mberia yanaangazia jinsi shughuli za kijamii kama vile: ukulima katika sehemu za miinuko na ufugaji wa idadi kubwa ya mifugo zinavyaathiri ekolojia.

Utafiti huu Ongarora umetusaidia katika kubainisha na kuchagua mashairi ambayo yanazungumzia masuala kisiasa, kiuchumi, kijamii na kimazingira. Hata hivyo tofauti na Ongarora utafiti wetu unaangazia athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia. Vilevile tumejikita katika diwa mbili za Mberia *Bara Jingine* (2001) na *Rangi ya Anga* (2014) tofauti na Ongarora ambaye ameangazia diwani tano za Mberia. Isitoshe, Ongarora ameongozwa na Nadharia ya Baada ya Ukoloni ilhali utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya Uhalisia na ya Mfumo wa Ekolojia.

### 1.8.0 Mbinu za Utafiti

Kombo na Tromp (2006) wanasema kuwa mbinu za utafiti zinarejelea namna utafiti utakavyoendeshwa na jinsi utakavyofanyika. Mbinu zinazotumika katika utafiti ndizo huweka

msingi wa data itakayokusanywa na kuchanganuliwa. Sehemu hii inaangazia: uteuzi wa sampuli, mbinu za kukusanya data na uwasilishaji wa matokeo yake.

### 1.8.1 Uteuzi wa Sampuli

Katika utafiti huu tumeteua diwani mbili za Mberia pekee: *Bara Jingine* (2001) na *Rangi ya Anga* (2014).Vilevile tumeteua mashairi kumi na sita kwa jumla. Kumi na manne kutoka *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na mawili kutoka *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014) yaliyogawanywa katika sehemu mbalimbali. Mashairi haya ni pamoja na: 'Ngao', 'Obasanjo', 'Giza Mbele,' 'Mimi Monika', 'Wanabiashara Barabarani', 'Ni Sumu kwa Watoto', 'Jinamizi', 'Nyeri', 'Matone ya Mvua', 'Kambi ya Malindi', 'Mimi Mto Nairobi', 'Hatutaaga Ndoto', 'Bara Jingine', 'Bwawa la Ithanje', 'Wanda' na 'Rangi ya Anga'. Ili kufaulisha uteuzi huu wa data tumetumia mbinu ya kimaksudi ambapo mtafiti huteua idadi ndogo ya sampuli itakayomwezesha kutimiza mahitaji ya utafiti wake (Orodho, 2005).

### 1.8.2 Ukusanyaji wa Data

Utafiti wetu umefanyika maktabani mahali ambapo tumesoma kazi tofautitofauti za fasihi. Tumesoma pia kwa kina tasnifu ambazo zimeandikwa kuhusu uchambuzi na uhakiki wa kazi mbalimbali za fasihi na hasa ushairi wa Kiswahili. Pia tumesoma diwani zingine za ushairi kama vile: *Mchezo wa Karata* (Mberia, 1997), *Redio na Mwezi* (Mberia, 2005) na *Msimu wa Tisa* (Mberia, 2007). Vilevile tumesoma majarida, magazeti na pia makala katika mitandao ili kuongeza ujuzi na maarifa kuhusiana na mada yetu. Hatimaye tumesoma diwani ya *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014) kwa kina na kubainisha mashairi yanayosheheni mazingira ya kijiografia na pia yale ambayo yanazungumzia kuhusu masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

### 1.8.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Matokeo

Uchanganuzi wa data umeangazia uchunguzi wa athari za mtagusano kati ya jamii na mazingira kupitia utambulishaji wa mandhari ya kijiografia na uainishaji wa masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii na yanavyoathiri mfumo wa ekolojia katika *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014). Tumewasilisha matokeo ya utafiti wetu kwa njia ya maelezo. Tumetoa maelezo kuhusu athari za maingiliano kati ya jamii na mazingira. Vilevile tumetoa maelezo na

ufafanuzi wa jinsi masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa yanavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii katika *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014).

### 1.8.4 Hitimisho

Katika sura hii mambo ya kimsingi kuhusu utafiti kwa jumla yameangaziwa. Kwa mfano, usuli wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni, upeo na yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti. Data ya utafiti ilikusanywa kutoka maktabani, kusoma kutoka mitandaoni na vitabu teule. Katika sura inayofuata tumejadili athari za mtagusano baina ya jamii na mazingira na kuonyesha ni vipi mazingira yanavyoathiriwa na mwingiliano huu wa binadamu.

# SURA YA PILI

# ATHARI ZA MTAGUSANO KATI YA JAMII NA MAZINGIRA

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia athari za mtagusano wa jamii na mazingira. Hii ni kwa sababu mazingira ni kiungo muhimu katika uchunguzi wa kazi yoyote ile ya fasihi. Mazingira hapa ina maana ya vitu ambavyo vinamzunguka binadamu kama vile misitu, mito, milima na mabonde. Mazingira haya ni sehemu ya ekolojia. Ekolojia ni mahusiano baina ya viumbe na mazingira vinamoishi. Kwa hivyo katika sura hii tumejikita katika uchanganuzi wa tungo zenye mandhari ya kijiografia na kuonyesha jinsi ambavyo maingiliano haya ya jamii yanavyoathiri mazingira. Wamitila (2008) anasema kuwa mandhari ya kijiografia huwa ni nguzo muhimu sana katika uchanganuzi wa kazi yoyote ile ya kifasihi na hasa zile ambazo zimeandikwa katika mkondo wa kihalisia. Hii ni kwa sababu kanuni ya ushabihi kweli inaonyesha uhusiano wa karibu kati ya ulimwengu wa kibunifu na ulimwengu halisi kwa kumfanya msomaji aweze kuamini kuwa matukio, mazingira na maingiliano ya wahusika yanayotokea katika ulimwengu huu wa kibunifu ni ya kukubalika. Mberia katika mashairi yake anayatumia mazingira haya ya kijiografia kuonyesha jinsi binadamu anavyoingiliana na mfumo wa ekolojia, suala ambalo linaathiri hali yake ya maisha na hata viumbe vinavyomzingira. Kwa hivyo katika sura hii tumeonyesha jinsi uharibifu huu wa mazingira ya kijiografia kama vile, misitu, mito, mabwawa, mabonde, miinuko, mmomonyoko wa udongo, hali ya hewa, bahari, maziwa na kadharika na hata utunzaji wake unavyoathiri maisha ya binadamu na viumbe vingine.

## 2.1 Uharibifu wa Misitu

Uharibifu wa misitu ni suala tata ambalo linaathiri mfumo wa ekolojia na hatimaye kuathiri mifumo ya kijamii kwa sababu misitu ni rasilimali muhimu katika mchakato mzima wa ekolojia. Katika diwani *Bara Jingine* utungo 'Jinamizi' (Mberia, 2001:55) mwandishi anatuonyesha jinsi ukataji wa miti kiholela unavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii. Binadamu akikata miti sehemu inageuka na kuwa jangwa na matokeo yake ni mimea, wanyama, ndege na binadamu kuathirika. Haya yanajitokeza katika uk. 58 kifungu cha 15 anaposema 'ndimi jangwa ninyimaye mayai, nafaka na maziwa'. Hii ina maana kuwa hakuna mimea inayoweza kukuzwa katika sehemu iliyo jangwa na hatima yake ni wanajamii kukosa chakula cha kutosha. Binadamu anajishughulisha na

harakati hizi za ukataji wa miti ili kupata mashamba ya kulima, upasuaji wa mbao na uchomaji wa makaa. Mtunzi anadokeza haya katika uk.55 kifungu cha 2 anapoonyesha jinsi watu wanatumia mashoka, mapanga na misumeno kuharibu miti. Anairejelea hali hii kama, 'kuchinja miti' ikiwa na maana ya kuangamiza miti yote bila kujali matokeo yake. Anapofanya hivi, matokeo yake ni 'kunyonga chemchemi za mito' ishara ya kuwa mito inakauka, binadamu na wanyama wanaangamia kwa sababu ya ukosefu wa maji. Mtunzi analinganisha uharibifu wa chemchemi hizi za maji na mauti ishara kuwa binadamu asipozilinda anaathiri vizazi vya leo na vijavyo.

Ni bayana kuwa baada ya wanajamii kukata miti, ardhi inaachwa wazi bila hata mti mmoja. Mtunzi anaelezea kuwa inaachwa 'uchi kama mkazi wa kijiji aliyeshambuliwa njiani' (uk. 55 kifungu cha 2). Hapa mtunzi anatumia tashbihi uchi kama mkazi akiwa na maana kuwa, ardhi inaachwa tambarare bila mimea yoyote ya kuifunika. Matokeo yake ni kuongezeka kwa hali ya joto ambayo inaharibu udongo ambao binadamu anautegemea kwa kuzalisha vyakula. Mshairi anadokeza haya katika uk. 55 kifungu cha 5 anaposema kuwa 'kijinga cha jua kiliunguza udongo'. Kauli hii inaonyesha kuwa binadamu anapoharibu udongo anaoutegemea kwa kilimo kupitia kwa ukataji wa miti basi anaathirika kiafya kwani hatapata chakula cha kutosha kinachozalishwa kutokana na udongo huu. Pia kutokana na ukataji wa miti nchi inaachwa 'uchi' hali inayochangia upepo mkali kupeperusha kwa nguvu vumbi jekundu suala ambalo laweza kueneza na kuleta maradhi kwa binadamu. Mwandishi anaonyesha haya katika uk. 56 kifungu cha 5 anaposema kuwa, 'vumbi jekundu lilipaa angani kama wimbo wa matanga'. Ikiwa na maana kuwa udongo ulio na rutuba unabebwa na upepo.

Baada ya wanajamii kukata miti kwa sababu ya shughuli za kilimo ardhi inaachwa wazi na unapojiri msimu wa mvua kubwa udongo wote unabebwa na maji kwani hakuna miti ya kuzuia mmomonyoko huu wa udongo. Hali hii inapotokea mimea kama vile: pojo na mbaazi inashindwa kuhimili dhoruba kali ya mawimbi makuu ya maji na inabebwa yote. Haya yanajitokeza katika uk. 56 kifungu cha 9 wakati mtunzi anasema kuwa, 'mvua iliponyesha pojo na mbaazi zilizokuwa mashambani zilikwama njiani'. Ishara ya kuwa zilibebwa na maji.

Pia kutokana na mvua ya gharika, wanyama kama vile ng'ombe, kondoo na mbuzi wanadhoofika kiafya kwa kukosa malisho ya kutosha. Hali hii ya wanyama na mimea kuathirika inasababishwa na binadamu kuhitilafiana na mfumo wa ekolojia kwa kuharibu misitu. Baadaye anaathirika

kiuchumi kwani pia yeye anategemea mimea hii na wanyama hawa ili kujiendeleza kiuchumi. Mshairi anasema kuwa kutokana na hali hii, binadamu, wanyama, wadudu na ndege wanaathirika kutokana na mvua ya gharika. Analinganisha ng'ombe na majani makavu yanavyoangushwa wakati wa upepo (uk. 57 kifungu cha 13) kuonyesha jinsi ng'ombe hawa wanavyodhoofika kiafya na kufa kwa sababu ya ukosefu wa chakula.

Athari hii ya mafuriko pia inasababisha huzuni na machozi kwa wanakijiji kwani yanasababisha vifo vya wanajamii na hata wanyama ambao wanaangamia kwa sababu ya ukosefu wa chakula. Mtunzi anakiri haya katika uk. 56 kifungu cha 15 anaposema kuwa 'walizikwa watoto, wazee na hatimaye wanyama'

Hali hii ya binadamu kuharibu misitu pia inajitokeza katika hali halisi ya maisha ya binadamu. Kwa mfano Letiwa (2018), anaonyesha jinsi msitu wa Mau nchini Kenya unavyoharibiwa na wakazi wa eneo hili. Wanafanya hivi ili wapate makazi, kuni, mbao na uchomaji wa makaa. Kulingana na Letiwa (2008), shughuli kubwa ambayo inaathiri ekolojia ya msitu huu ni uchomaji wa makaa wakitumia miti ya kiasili. Ni suala la kusikitisha kuona kuwa msitu huu wa Mau ni mojawapo wa misitu ya kiasili ambao umebaki na ulio na chemchemi za maji ambazo zina umuhimu mkubwa katika mfumo wa ekolojia. Athari ya ukataji huu wa miti ni kuwa unasababisha mito iliyoko ndani ya msitu huu wa Mau kukauka. Hali hii inaathiri maisha ya wanajamii kiuchumi kwani wengi huyategemea maji haya kuyanyunyuzia mashamba yao. Pia mifugo wanaoyategemea maji haya wanaangamizwa kwa sababu ya kukauka kwa chemchemi hizi za maji. Jambo hili limepelekea serikali kuwafurusha wakazi hawa ili kuweza kuhifadhi ekolojia. Sayange (2018) anasema kuwa uharibifu wa msitu huu wa Maua umeathiri uhamaji wa wanyama na hasa ndovu kutoka msitu wa Maasai Mara hadi msitu wa Olpusimoru suala ambalo linaathiri shughuli za kitalii ambazo huleta fedha za kigeni na kuinua uchumi wa Kenya.

Katika diwani *Bara Jingine* shairi 'Matone ya Mvua,' msimulizi anaonyesha kuwa hapo awali kabla ya mvua kunyesha binadamu hakuwa na furaha hata kidogo kwa sababu ya vumbi lililokuwa limejaa barabarani. Anaonyesha haya katika uk. 73 kifungu cha 3 anaposema 'vumbi liliwasonya njiani' ishara ya jinsi lilikuwa jingi. Vumbi hili ni hatari kwa afya ya binadamu na hata viumbe vingine kwani linaweza kusababisha magonjwa mbalimbali. Anasisitiza kuwa jamii ikiyatunza mazingira inamoishi basi itaweza kuepukana na baadhi ya magonjwa yanayoweza kuhatarisha maisha yake. Mshairi anaendelea kuonyesha jinsi wanyama waliodhoofika kiafya

kwa sababu ya kukosa chakula kizuri lakini baada ya mvua kunyesha afya zao zinaimarika kwa kupata chakula chenye madini ya kutosha. Haya yanajitokeza katika uk. 73 kifungu cha 3 anaposema:

> Bali leo
> Wana wa kondoo
> Ewee! Watazame uani
> Warukao na kupinda angani
> Kwa joto laini la furaha
> Limewajaa katika damu

Katika kifungu hiki mwandishi anaonyesha jinsi wanyama walivyofurahi na kuchangamka kwa sababu ya kupata malisho mazuri. Anasema kuwa 'joto la furaha liliwajaa katika damu', ishara ya jinsi wanyama kama kuku walivyoimarika kiafya kwa sababu ya kunawiri kwa chakula kama vile mtama na mawele. Mtunzi anamalizia shairi kwa kuisifia mvua na kutumai kuwa haitapotea wala kupusa ili iweze kuwanusuru wanyama na binadamu dhidi ya ukame ambao unasababishwa na jua kali. Anatumia sitiari 'mgeni wa thamani' katika uk. 74 kifungu cha 5 kurejelea mvua inayoleta manufaa mengi kwa jamii. Ni wazi kuwa mwandishi anaielimisha jamii kuhusu umuhimu wa kupanda miti kwani wakifanya hivyo hawataangamia kutokana na janga la njaa na wataweza kujiinua kiuchumi na kijamii.

Katika diwani *Rangi ya Anga* utungo 'Wanda' sehemu ya 5 (Mberia, 2014), mwandishi anaonyesha madhara yanayosababishwa na uharibifu wa misitu na hasa ukataji wa miti kiholela. Athari yake ni kusababisha mafuriko ambayo mtunzi anasema 'yanatiririka kwa fujo' ishara ya jinsi yako mengi kwani miti ambayo inasaidia kuyazuia imeharibiwa. Matokeo ya mafuriko haya ni kubeba mchanga 'mweusi' yaani wenye rutuba na kuacha mchanga 'mwekundu' yaani ambao hauna madini ya kusaidia mimea kukua. Katika uk. 34 kifungu cha 1 mtunzi anasema kuwa yuko na furaha kwa sababu 'majira ya ukarimu na shibe yamefika' ikiwa na maana kuwa msimu wa mvua umejiri lakini pia anahuzunika kutokana na hasara itakayoletwa na mvua hii. Hii ni kwa sababu katika msimu uliopita wanajamii walifurahia mchanga wenye rutuba lakini baada ya mafuriko umebebwa wote hadi mitoni na kuacha 'mgeni mwekundu' yaani mchanga usio na rutuba. Hali hii inaharibu makazi ya wanyama wanaoishi majini kwani baada ya udongo huu kuishia mitoni wanyama wanaoishi humo wanaathirika kwa sababu wanakosa mahali pa kujisitiri. Anaendelea kusema kuwa mito ambayo haikuwa na maji hapo awali sasa 'imekunywa maji na imekinai' (uk. 34 kifungu cha 3) ishara kuwa imefurika hali ambayo inasababisha

maangamizi kwa binadamu na wanyama. Ili kuzuia hali hii wanajamii sharti waelimishwe na kushauriwa dhidi ya kuharibu miti na mimea iliyoko kando ya kingo za mito.

Katika kifungu cha mwisho mtunzi anaonyesha jinsi mafuriko yanayosababishwa na ukataji wa miti yanavyoathiri ekolojia anasema kuwa 'maji yaliyokuwa ya kijani sasa yananguruma huku mgeni mwekundu akingurumisha magogo, mizizi na mizoga' (uk. 35 kifungu cha 4). Katika kauli hii Mberia anaonyesha athari ya mafuriko kwani yanaharibu mimea, kuangamiza wanyama na binadamu. Hali hii inaathiri binadamu kwani anaitegemea mimea hii na wanyama hawa kwa chakula na fedha za kujiinua kiuchumi.

Baada ya hali hii yote, sehemu ya kijiji inaachwa jangwa kisa na maana ni binadamu kukata miti na matokeo yake ni kuwa mito inakauka, wanyama wanakufa, mimea inakauka na binadamu anaachwa akiteseka kwani hawezi kujikimu kiuchumi. Haya yanajitokeza katika uk. 58 kifungu cha 15 anaposema kuwa 'ndimi jangwa ninyongae mito, ninyimae maziwa, nyama na matunda'. Kwa hivyo inajitokeza wazi kuwa binadamu akiharibu misitu na hasa ukataji wa miti anaathiri ekolojia. Kwa mfano mimea inabebwa na maji, wanyama wanaangamia kwa sababu ya kukosa malisho. Pia yeye anaathirika kwa sababu mimea ikiharibiwa na wanyama wafe basi anakosa chakula cha kutosha, anakumbwa na maradhi na hatimaye anaangamia. Hivyo basi binadamu ana jukukumu la kulinda misitu.

Katika diwani *Bara Jingine* shairi 'Matone ya Mvua' (Mberia, 2001), mwandishi pia anaonyesha umuhimu na faida za kutunza misitu. Anaisifu mvua ambayo inaletwa na hali ya binadamu kuyatunza mazingira wanamoishi na hasa upanzi wa miti; anasisitiza kauli hii kwa kurejelea mvua kama 'mashujaa wa uhai' (uk. 73 kifungu cha 1). Vilevile anaonyesha jinsi jamii inavyofaidika kutokana na mvua ambayo inanyesha. Anasema kuwa wanyama, wadudu na ndege waliokuwa wamedhoofika kwa sababu ya ukame hapo awali 'wanatabasamu kwa sababu ya matone ya mvua yanayoleta mazao tele.' (uk. 73 kifungu cha 3). Maana yake ni kuwa mvua hii inasababisha mimea kunawiri na kukua vizuri hali ambayo inampa binadamu na wanyama chakula cha kutosha.

Mwandishi anaonekana kuisifu mvua ambayo anasema inanyesha kwa wakati unaofaa (uk. 73 kifungu cha 1) ishara kuwa imenyesha wakati ambapo binadamu, mimea na wanyama wanaihitaji. Anatumia sitiari 'matone ya uhai' anapoirejelea mvua, ishara ya kuwa isiponyesha

binadamu na wanyama wanaangamia kwa sababu ya kiangazi. Ili kuzuia hali hii ya kiangazi binadamu hana budi kupanda miti kama vile mijakaranda, migunga, mikayaya na mikomo ambayo inavutia mvua. Ikiwa mvua haingenyesha mimea ingekauka na matokeo yake ni binadamu na wanyama kuangamia kwa sababu ya kukosa lishe bora. Kauli hii ya mtunzi inaonyesha umuhimu wa kutunza ekolojia kwani binadamu, wanyama na mimea hutegemeana. Katika uk. 73 kifungu 2 mwandishi anasema kuwa kutokana na mvua kunyesha mimea imeweza ‘kukombolewa kutoka tanzi la simanzi’. Hapa mtunzi anaonyesha jinsi mvua imesababisha mimea kutokauka hali ambayo imewanufaisha wanyama, wadudu na ndege kwa sababu wamepata chakula.

## 2.2 Hali ya Hewa na Ongezeko la Joto

Ongezeko la joto ni hali ya joto kuongezeka kupita hali ya kawaida ambapo viumbe na mimea haiwezi kuistahimili kutokana na gesi zenye sumu zinazotokana na uharibifu wa hewa hali ambayo inachangia mabadiliko ya tabia nchi. Mberia (2001) katika diwani ya *Bara Jingine* shairi ‘Ngao’ anaonyesha jinsi teknolojia anayoivumbua binadamu inavyochangia katika uharibifu wa ukanda wa ozoni hali inayosababisha ongezeko la joto. Katika uk. 59 kifungu cha 2 mtunzi anasema kuwa ‘kemikali jeuri zinatafuna ozoni kama majeshi ya mchwa’ ishara ya jinsi kemikali zinazotolewa kwenye viwanda zinavyoharibu ukanda wa ozoni kwa kiwango kikubwa. Hatima yake ni binadamu kukumbwa na magonjwa ambayo yanatokana na miale mikali ya jua yenye sumu inayoathiri afya yake na kusababisha mauti.

Madhara haya ya miale ya jua yanaathiri maisha ya binadamu, wanyama na hata mimea kwa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanasababishwa na kemikali zenye sumu anazotumia binadamu katika uzalishaji wa bidhaa viwandani. Mwandishi anarejelea uharibifu huu wa ozoni kama ‘janga linalotukodolea macho’ (uk. 59 kifungu cha 2), ishara kuwa wanajamii wanaathirika kwa sababu ya miale hii mikali ya jua. Hali hii inatokea kwa sababu binadamu hajaweka mikakati madhubuti ya kuzuia kemikali zinazotoka viwandani kuathiri hewa na ukanda wa ozoni. Mtunzi anasema kuwa kuna ‘kemikali jeuri ambazo zinaharibu ozoni kama majeshi ya mchwa’ akiashiria jinsi kemikali hizi zinavyoathiri eneo la ozoni na hivyo basi kuachilia miale mikali ya jua ambayo inaathiri viumbe kama vile binadamu na wanyama. Mshairi anaendelea kusema kuwa ikiwa binadamu angekuwa na uwezo wa kuunda ozoni angeirekebisha kwa manufaa yake mwenyewe. (uk. 59 kifungu cha 2), ishara kuwa binadamu

yuko radhi kuyabadilisha maumbile ya kiasili ilmuradi yana faida kwake bila kujali wanyama na mimea ambayo inamzunguka. Hali hii inaonyesha jinsi ambavyo binadamu alivyojawa na tamaa na ubinafsi kwani hafahamu au anafahamu na hajali kuwa viumbe vingine vinayategemea mazingira haya. Mberia pia anaonekana akisifia ukanda wa ozoni kwa sababu unawalinda waja kutokana na miale mikali ya jua licha ya kuwa binadamu ameuharibu. Anaonyesha haya katika uk. 59 kifungu cha 2 anaposema kuwa 'bila uchungu wa malipo ukanda wa ozoni unawakinga binadamu kutokana na miale mikali ya jua'. Maana yake kuwa wanajamii hawalipii chochote ukanda wa ozoni kwani ni wa kiasili.

Anaendelea kuusifu ukanda wa uzoni kwani anakiri kuwa miale hii ya jua ni hatari na hata inaweza kusababisha magonjwa kwa binadamu hali ambayo inaweza hata kusababisha mauti. Anasisitiza haya katika uk. 60 kifungu cha 5 anaposema kuwa 'ukanda wa ozoni unalinda wanadamu kutokana na mauti'. Hii ni ishara kuwa isipokuwa kwa ukanda huu mimea, binadamu na wanyama wangeweza kuathirika. Mwandishi hata hivyo anakashifu na kumsuta binadamu kwa sababu anaendelea kuuharibu. Hali hii inatokea kwa sababu ya uvumbuzi wa teknolojia ya kisasa ambayo binadamu anaitumia katika kuzalisha bidhaa viwandani. Kwa mfano hivi viwanda vinatoa moshi na kemikali zenye sumu ambazo zinaachiliwa hewani kiholela na kuharibu ukanda wa ozoni. Mtunzi anaonyesha haya anaposema kuwa 'tunakulegeza afya' katika uk. 60 kifungu cha mwisho kuonyesha jinsi harakati za wanajamii zinavyoharibu ukanda huu. Matokeo yake ni kuibuka kwa magonjwa mbalimbali na hatimaye kuleta maangamizi kwa binadamu, wanyama na mimea.

Kulingana na Mberia ni wazi kuwa binadamu anapoharibu hewa anaathiri mfumo wa ekolojia na hatimaye mifumo mbalimbali kama vile ya kiuchumi na kijamii. Hili linatokea pale ambapo analazimika kugharamia matibabu ambayo kiini chake ni miale mikali ya jua. Pia anapozalisha bidhaa viwandani kiholela akitumia teknolojia ya kisasa na kuachilia kemikali zenye sumu angani, anaharibu ukanda wa ozoni. Anadokeza haya katika uk. 60 kifungu cha 6 anapoirejelea teknolojia kama 'Ujeuri wa binadamu'. Hatima yake ni kuwa miale hii ya jua inakosa kinga na hivyo basi inaathiri binadamu, wanyama na hata mimea. Binadamu anaathirika kiuchumi kwa sababu anategemea wanyama na mimea kama chakula. Kauli hii inaoana na mhimili wa Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia unaosema kuwa mtunzi huonyesha jinsi utamaduni wa kijamii huchangia katika kuathiri maendeleo ya kiuchumi na kijamii kutokana na mali ya kiasili na

mifumo mipya ya kiteknolojia. Kwa hivyo binadamu akitumia teknolojia ya kisasa kwa mfano katika kuzalisha bidhaa viwandani bila uangalifu anaathiri ekolojia na hatimaye kuathiri maisha yake kutokana na gesi zenye sumu zinazotolewa viwandani.

Katika diwani ya *Rangi ya Anga* shairi 'Wanda' sehemu ya 1 (Mberia, 2014) mwandishi anasema kuwa 'joto linapeperusha bendera' (uk. 28 kifungu cha 1) ishara ya jinsi ongezeko la joto ulimwenguni linavyoathiri maisha ya wanyama, binadamu na hata mimea. Anaonyesha jinsi afya ya binadamu inavyoathirika kutokana na miale mikali ya jua anaposema kuwa 'linakereketa migongo' katika kifungu cha 1 uk. 28. Vilevile anaonyesha jinsi wanyama na wadudu wanavyoangamia kutokana na miale mikali ya jua anaposema, 'tazama mayowe kimya yakibabaisha ndege, mijusi na nyuki'. (uk. 28 kifungu cha 2) ishara ya jinsi viumbe hivi vinavyoathirika kutokana na ongezeko la joto ambalo linaathiri miili yao. Hali hii inachangiwa na binadamu kutopanda miti na kuyaharibu mazingira ya kiasili. Mtunzi anaonyesha jinsi ongezeko la joto ulimwenguni linavyoathiri maisha ya binadamu. Anasema kuwa 'joto linatawala kwa maringo' ishara ya jinsi lilivyoenea na kuangamiza viumbe na mimea. Joto hili limeathiri afya ya binadamu na wanyama kwa sababu hawana mahali pa kujisetiri. Anasisitiza haya katika uk. 28 kifungu cha 1 anaposema:

Linanyanyasa tosi
Na macho
Harara inachokoza kwapa
Na kukereketa migongo

Ongezeko hili la joto duniani linaathiri mimea ambayo inakauka kutokana na jua kali. Mwandishi anaonyesha haya katika kifungu cha 3 uk. 28 anaposema: 'Ewe jua! Mikwaju na mimea walikutenda ovu gani?' Hali hii inaonyesha jinsi binadamu na wanyama wanavyokumbwa na janga la njaa kwani wanaitegemea mikwaju na mimea kama chakula ambayo inakauka kutokana na joto jingi. Joto hili pia linasababisha ndege na wadudu kuangamia kwa sababu hawana mahali pa kujisetiri kutokana na miale mikali inayotokana na jua. Mtunzi anasisitiza haya anapouliza katika kifungu cha 4 uk. 28 'ni ovu gani ndege, wadudu na wanyama wa mito walilotenda mpaka wakaangamia kutokana na joto hili'. Kauli hii inaoana na mhimili wa Nadharia ya Ekolojia unaodai kuwa binadamu anastahili kuhusiana na kuingiliana na mandhari yake kwa njia sahihi bali si kuchangia katika kuyaharibu. Hii ni kwa sababu akifanya hivyo anaathiri viumbe na mimea inayomzunguka. Ongezeko la joto pia linaathiri mfumo wa

ekolojia kwa sababu binadamu anategemea mimea hii kwa chakula na pia anawategemea wanyama hawa kujikimu kiuchumi. Kwa hivyo mimea ikikauka na wanyama kuangamia binadamu hataweza kupiga hatua za kimaendeleo. Ndiposa mtunzi anawafahamisha na kuwashauri wanajamii waweze kupanda miti na kupunguza uchafuzi wa hewa ili kuzuia ongezeko la joto ulimwenguni. Anawaonya kuwa wasipofanya hivyo mimea itanyauka, mito ikauke na hatimaye wanyama na binadamu wataangamia.

Katika kuliangazia suala hili tumeongozwa na mhimili wa nadharia ya Uhalisia unaodai kuwa mwandishi huwasilisha mambo ambayo yanaonekana na kuthibitika katika jamii anamoishi. Kwa mfano, mwandishi anaonyesha jinsi wanyama wanaangamia na mimea kunyauka kutokana na ongezeko la joto duniani. Vilevile kulingana na Mativo (2018, August 7), Kenya ni miongoni mwa nchi duniani ambazo zinakumbwa na hatari ya ongezeko la joto duniani. Ripoti hii imetolewa ambapo kiwango cha joto katika bara la Yuropa kimezidi nyuzi 40. Hali hii kulingana na Mativo (2018) imechangiwa na moto uliochoma misitu na hasa uliochoma misitu katika nchi ya Ugiriki na kuangamiza watu tisini na mmoja. Nchini Kenya hali hii pia imechangiwa na moto ambao ulichoma nyasi, mimea na miti ya kiasili miaka mitatu iliyopita. Suala hili limechangia migogoro na mivutano kati ya wafugaji wa kuhamahama wakipigania malisho ya mifugo wao. Ili kuzuia hali hii ya ongezeko la joto, serikali za nchi ambazo zimeathiriwa zinastahili kupanda miti kwa wingi na kutumia mbinu mwafaka za kuhifadhi gesi zenye sumu.

## 2.3 Uchafuzi wa Mito na Mabwawa

Mito na mabwawa ni rasilimali ambazo zina umuhimu mkubwa katika mchakato mzima wa ekolojia. Hii ni kwa sababu binadamu na wanyama hawawezi kuishi bila kuyategemea maji. Mito na mabwawa pia huwa ni hifadhi na makazi ya baadhi ya viumbe kama vile samaki ambao hutumiwa na binadamu kama chakula. Kwa hivyo binadamu akiharibu mito na mabwawa anaathiri mfumo mzima wa ekolojia kwenye mito na mabwawa. Katika diwani *Bara Jingine* (Mberia, 2001) katika shairi ‘Mimi, Mto Nairobi’ mtunzi anaonyesha jinsi harakati za binadamu zinavyoharibu na kuchafua maji ya mto Nairobi. Mwandishi anasema ‘wananitesa hawa wajeuri’ (uk. 63 kifungu cha 1) ishara ya jinsi wakazi wa mji wanachafua maji ya mto huu na kuhitilafiana na mimea na wanyama ambao wanaishi majini. Uchafuzi huu wa mito unaharibu mfumo wa ekolojia kwa sababu baadhi ya wanyama hutegemea mazingira haya kukua.

Binadamu hana shukrani na hajawajibika kwani anayachafua maji ya mito licha ya kuwa anayategemea kwa matumizi yake ya kila siku. Mtunzi anasisitiza hili kwa kuwarejelea wakazi wa jiji kama 'majirani wasio na shukrani' (uk. 63 kifungu cha 1). Hii ni kwa sababu wanaachilia mafuta na takataka zingine kwenye mito na matokeo yake ni kuangamiza mimea na wanyama ambao wanaishi humo hali inayochangiwa na ukosefu wa hewa ya okisijeni. Wanyama wanaoishi majini wanahitaji hewa ya okisijeni ili waendelee kukua na kuzaana. Lakini wakati hewa hii inapochafuliwa wanaangamia na kutoweka. Mberia pia anaonyesha jinsi wakazi wa jiji wanavyotupa makopo, matairi na takataka ndani ya mto Nairobi. Makopo haya na takataka hizi zinaathiri na kuziba mkondo wa maji jambo ambalo linachangia maji taka kutiririka hadi katika makazi ya binadamu. Matokeo ya hali hii ni magonjwa ambayo yanasababishwa na maji taka. Anaonyesha haya katika uk. 63 kifungu cha 2 anaposema kuwa, 'wananinyonga kwa mafuta na tairi'.

Ni wazi kuwa licha ya kwamba wakazi wa jiji ndio wanaofaidika na maji ya mto Nairobi wanaendelea kuyachafua. Mtunzi anasema katika uk 63 kifungu cha 2 kuwa 'wendawazimu wananiangamiza' ishara ya jinsi wakazi wa Nairobi wanavyoyachafua maji ya mto huu bila kujali. Matokeo yake ni kuibuka kwa maradhi yanayosababishwa na maji machafu yaliyojaa viini vya sumu. Ni bayana kuwa binadamu anapoharibu mazingira yanayomzunguka kwa mfano uharibifu na uchafuzi wa mito, anaathirika kiuchumi. Hii ni kwa sababu anapougua sharti agharamie matibabu. Binadamu pia anahatarisha maisha ya wanyama wengine ambao wanaishi majini kwani anapotupa takataka na kemikali kali kwenye mito, wanyama hawa wanakosa hewa safi au oksijeni na matokeo yake ni maangamizi.

Wanajamii pia wanapojishughulisha na shughuli za kilimo kando ya mito na mabwawa, wanaharibu ekolojia. Kwa mfano, katika diwani *Bara Jingine* (Mberia, 2001) katika shairi 'Bwawa la Ithanje' mwandishi anaonyesha jinsi bwawa hili linavyoharibiwa na maji yake kuchafuliwa na wakazi wa eneo hili ambao wanajishughulisha na shughuli za kilimo kando mwa bwawa lenyewe. Baada ya wakulima kutumia kemikali zenye sumu kunyunyizia mimea katika mashamba yao wanayaelekeza maji haya yenye viini sumu kwenye bwawa. Mwandishi anasisitiza haya anaposema 'mnanikamulia sumu kinywani' (uk. 69 kifungu cha 2) ishara kuwa kemikali zinazotoka kwenye viwanda zinapoelekezwa kwenye maji ya bwawa hili binadamu na wanyama wanaathirika kwa sababu wanayategemea maji haya kwa shughuli zao za kila siku.

Mwandishi anaonyesha masikitiko na machungu kwa kuona jinsi ambavyo 'Bwawa la Ithanje' linavyochafuliwa na wakazi. Anasikitika kwa kuona jinsi ambavyo uzuri wake ulivyoharibiwa na binadamu. Anasema kuwa 'pole Bwawa la Ithanje polepole afya yako inafifia' (uk. 69 kifungu cha 1). Hii ina maana kuwa hapo awali bwawa lenyewe lilikuwa la kuvutia lakini baada ya binadamu kuanza shughuli za kilimo akitumia teknolojia ya kisasa ameharibu na kuyachafua maji ya bwawa hili. Anaonyesha jinsi jamii ilivyolitelekeza bwawa hili licha ya kuwa ndio inayofaidika. Kauli hii anaisisitiza anaposema kuwa, 'bwawa lenyewe limebaki bila daktari au muuguzi' (uk. 69 kifungu cha 1), ishara kuwa hakuna mtu ambaye analijali tena wala kulitunza. Mtunzi anaendelea kuonyesha jinsi wakulima wanaonyunyuzia mashamba maji kutoka bwawa hili wanavyotumia kemikali katika kunyunyuzia mimea yao, kisha wanayaelekeza maji haya yenye sumu kwenye bwawa. Anadokeza haya katika kifungu 2 uk. 69:

Wakulima wanyunyizao maji
Wanakukamulia sumu kinywani

Kutokana na kifungu hiki ni wazi kuwa wakulima wanapoyaelekeza maji yenye sumu kwenye mabwawa, yaani maji yaliyo na kemikali zinazotokana na dawa zinazonyunyuziwa mimea mashambani wanaharibu mfumo wa ekolojia. Hii ni kwa sababu kuna mimea na wanyama ambao wanaishi katika mabwawa haya. Isitoshe, binadamu anayatumia maji yaya haya katika kunyunyizia mimea na hata katika matumizi yake ya nyumbani. Anapofanya hivi anahatarisha maisha yake na pia ya wanyama wanaoyategemea maji yaya haya. Mshairi anaendelea kuonyesha jinsi kemikali zinazotoka viwandani zinavyoelekezwa kwenye bwawa na matokeo yake ni kuchafua maji na kuyafanya hatari kwa matumizi ya binadamu na wanyama. Mtunzi anakiri haya katika kifungu 2 uk. 69 anaposema:

Navyo viwanda vya Limuru
Vinakushambulia mwili
Kama vikosi hatari
Vikishambulia adui
Katika vita vya kemikali.

Katika kifungu hiki mtunzi anamlaumu binadamu kwa sababu ya kukosa mikakati bora ya kuhifadhi takataka na kemikali zinazotoka viwandani kwani anahatarisha maisha yake pamoja na ya mimea na wanyama wanaomzingira. Anaonyesha haya anaposema kuwa 'viwanda vya Limuru vinakushambulia mwili' ishara ya jinsi kemikali zinazotoka katika viwanda hivi vinavyoharibu maji ya bwawa hili. Mtunzi anashauri kuwa ili kuepukana na adha hii, binadamu

hana budi kuibuka na mikakati mwafaka ya kuhifadhi mazingira kutokana na uchafu na kemikali zinazotoka viwandani anamozalishia bidhaa akitumia teknolojia ya kisasa. Mshairi anasikitika kutokana na hali ya kuharibiwa kwa mabwawa ya maji kwani anafahamu kuwa yanapoharibiwa wanajamii wanaangamia kutokana na ukosefu wa chakula cha kutosha kwani wanakosa maji ya kunyunyizia mimea yao. Hii ni kwa sababu maji yaliyochanganyika na viini sumu si salamu kutumika katika kunyunyizia mimea. Pia wanaathirika wakinywa maji yenye viini sumu. Anaonyesha haya anaposema kuwa maji ya bwawa hili ni 'uhai wa familia nzima' (uk. 69 kifungu cha 3) ishara ya kuwa jamii nzima inalitegemea bwawa hili kuzalisha chakula. Kwa hivyo anawaomba na kuwahimiza wanajamii walinde na wahifadhi mabwawa ili kuepuka kuathiri mfumo wa ekolojia. Anasisitiza kauli hii anaposema (katika kifungu 3 uk. 69), 'La! Usife! Ithanje usife! Kwani kifo chako kitakuwa cha familia kubwa'. Anachosisitiza mtunzi katika kifungu hiki ni kuwa wakazi wa eneo hili wanalitegemea bwawa hili kwa maji ya kuinyunyizia mimea na wanatumia teknolojia ya kisasa katika kukuza vyakula vyao. Kwa hivyo maji haya yakiharibiwa kwa kemikali zenye sumu wanajamii wanaathirika kiuchumi. Hii inasababishwa na ukosefu wa maji safi ya kunyunyizia na kuzalisha chakula cha kutosha. Matokeo yake ni maangamizi kutokana na njaa na kutegemea misaada ya chakula kutoka mataifa mengine. Wanyama ambao pia binadamu anawategemea kwa chakula na hata kujikimu kiuchumi wanaathirika na hatimaye kuangamia.

Ni wazi mtunzi anawasihi wanajamii waweze kutunza mabwawa yanayowasaidia katika kupata maji wanayoyatumia katika kilimo na hata mahitaji yao ya kila siku. Mwandishi katika kifungu cha 4 uk. 69 anasisitiza haya anaposema, 'usife! Ithanje dumu'. Mshairi pia anadhamiria kukashifu na kusuta jinsi binadamu anavyohitilafiana na ekolojia kwani anapofanya hivyo anaharibu rasilimali na matokeo yake ni kurudisha maendeleo ya taifa nyuma. Mtunzi anawasuta wakulima na wenye viwanda, ambao wanayaelekeza maji yenye sumu katika mito na mabwawa kwa kusema kuwa 'viwanda vya Limuru vinashambulia mwili' (uk 69 kifungu cha 4) ishara kuwa zinatoa kemikali ambazo zinaharibu maji ya bwawa hili jambo linaloathiri binadamu na wanyama.

Jambo hili la uchafuzi wa mito pia linatokea katika hali halisi maishani. Kwa mfano Mueni (2018) anaonyesha jinsi wakazi wa mji wa Nairobi wanavyouharibu mto Nairobi. Anasema kuwa uchafuzi huu unatokana na uchafu ambao unatoka kwenye mitaa ya mabanda ambayo

imejengwa kando kando ya mto huu na takataka ambazo zinatoka kwenye masoko ambayo yanauzingira. Pia takataka na kemikali zenye sumu kutoka viwandani zinaelekezwa kwenye mto huu. Serikali ya kaunti imeshindwa kuhifadhi takataka hizi kutokana na idadi kubwa ya watu wanaoishi jijini, suala ambalo linachangia wengine kujenga majumba makubwa kando kando ya mto. Ili kuzuia hali hii serikali haina budi kubomoa nyumba zote ambazo zimejengwa kwenye kingo za mto huu ili kuzuia kuendelea kuharibiwa kwa mfumo wa ekolojia.

### 2.4 Milima na Mabonde

Milima na mabonde ni sehemu ya mazingira ambayo hutumika kama hifadhi ya wanyama. Katika sehemu hizi mimea hukua na kustawi vyema suala ambalo linapelekea binadamu na viumbe vingine kupata chakula cha kutosha. Katika diwani *Bara Jingine* (Mberia, 2001) katika shairi 'Nyeri' mwandishi anaonekana akiusifu mji wa Nyeri wenye mabonde na miinuko. Anausifia mji huu anaposema kuwa katika mabonde na miinuko 'kijani kibichi kinatabasamu' (uk, 70 kifungu cha 1) ishara ya jinsi eneo zima linavyong'aa kwa rangi ya kijani kibichi kwani wanajamii hawajaharibu mfumo wa ekolojia. Matokeo yake ni kwamba ndege na wanyama wanayafurahia mazingira haya yenye hewa safi ya okisijeni na chakula tele. Wakulima nao wanapata mavuno mengi ya majani chai, kahawa na ndizi; pia wanapata faida nyingi kutokana na mauzo ya maziwa ya ngo'mbe wa kisasa wanaofugwa katika eneo hili. Anasisitiza haya katika kifungu cha 3 uk. 70 anaposema kuwa 'wakulima wa majani chai na wafugaji wa ng'ombe bila nundu wanafurahia mazao'. Mtunzi anaonyesha jinsi watoto wa sehemu hii walivyoimarika kiafya kutokana na hali ya kupata lishe bora kwa kusema kuwa 'alikutana na watoto wenye nyuso zilizong'aa' (uk. 70 kifungu cha 4), ishara ya kuwa watoto hawa wanapata chakula chenye madini hali ambayo inawazuia kupatwa na maradhi. Mberia pia anaonyesha mji ulio na mabonde na miinuko ambayo imefunikwa na rangi ya kijani kibichi jambo linalowafanya wakazi wa eneo hili waishi kwa furaha na tabasamu. Rangi hii ya kijani kibichi inatokana na juhudi za wakazi hawa kuyatunza mazingira. Hawachangii katika kuyaharibu bali wanashirikiana katika kupanda miti na ndiposa wanafurahia uzuri wa eneo lenyewe. Katika uk. 71 kifungu cha 5 mtunzi anasema wanahimizana kupanda miti kwa kusema 'onyesha mpaka wa shamba kwa miti'. Upanzi huu wa miti unawasaidia wanajamii kupata hewa safi na kuepukana na maradhi ambayo husababishwa na ukosefu wa hewa safi. Pia miti hii inakuwa hifadhi ya wanyama na ndiposa ndege wanafurahia mazingira haya ya kijani kibichi.

Mwandishi anaendelea kuonyesha jinsi wakazi wa eneo hili wanavyopata chakula cha kutosha kutokana na chakula maridhawa kinachozalishwa katika eneo hili. Anasema kuwa wakazi hawa 'wanaridhisha tumbo' (uk. 70 kifungu cha 2), ishara ya kuwa hawakumbani na janga la njaa kwani wanapata chakula cha kutosha. Wanajamii wanaonywa kuwa wasipoyatunza mazingira yao na hasa sehemu za milima na miinuko wataangamizwa na janga la njaa na pia wataathiri viumbe vingine ambao hupata hifadhi katika sehemu hizi. Pia katika sehemu hii anaonyesha jinsi ndege wanavyofurahishwa na mazingira haya ya kijani kibichi. Anadokeza haya katika uk. 70 kifungu 3 anaposema kuwa 'ndege wanaimba na kucheza kwa kufurahia kijani kibichi'. Hii ina maana kuwa ndege hawa wanapata chakula cha kutosha, ambacho kinatokana na jamii kutunza sehemu hizi za miinuko na mabonde na hasa kutokana na upanzi wa miti. Kwa hivyo binadamu akitunza sehemu hizi vizuri atakuwa amehifadhi mfumo wa ekolojia.

Mwandishi anaendelea kuonyesha jinsi mazingira ya mji huu yanavyowanufaisha wakulima. Anasema kuwa wakulima wa mimea ya majani chai, kahawa na mahindi inayokuzwa katika sehemu za miinuko (uk. 70 kifungu cha 3) wanapata mavuno tele. Anachokitilia mkazo hapa ni kuwa ikiwa jamii inatunza sehemu za miinuko na mabonde inaweza kujichumia riziki kwani sehemu hizi huwa na udongo wenye rutuba. Mimea ikikuzwa katika sehemu hizi inanawiri vizuri na wakulima wanapoyauza mazao yao wanapata pesa za kujiinua kiuchumi suala linalochangia maendeleo katika taifa. Mberia anaonyesha jinsi wafugaji wa mji huu wanavyofaidika kutokana na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa wa kisasa kwa kusema kuwa wanafuga ng'ombe ambao hawana nundu na wanapata mazao tele (uk. 70 kifungu cha 3). Hali hii inachangiwa na juhudi za binadamu za kutunza sehemu zenye mabonde na miinuko ambapo ng'ombe hawa wa maziwa wanakulia na matokeo yake ni kwamba wakulima wanapata maziwa ya kutosha wanayoyoanywa na kuimarisha afya zao na hasa za watoto. Pia wanayauza maziwa na kuweza kujiinua kiuchumi.

Mtunzi anasema kuwa 'watoto wa sehemu hii, nyuso zao zinang'ara kutokana na afya nzuri' (uk. 70 kifungu cha 4). Hali hii inatokana na kupata chakula cha kutosha na maziwa yenye viini vinavyosaidia mwili. Watoto wakipata lishe bora wanaweza kujikinga kutokana na maradhi ambayo yanaweza kudhoofisha afya zao. Watoto pia wakiwa na afya nzuri ni furaha kwa jamii kwani ndio tegemeo la kesho. Mtunzi anawasifia wakazi wa eneo hili kwa sababu ya upandaji miti kwenye sehemu hizi za mabonde na miinuko ili kuweza kuvutia mvua zaidi na kuzuia mmomonyoko wa udongo. Anadokeza haya anaposema katika uk. 71 kifungu 5 kuwa matangazo

yamewekwa kwenye milango ya nyumba na vituo vya umma yakiwa na ujumbe kwamba wakaazi wapande miti. Anachosisitiza Mberia katika kauli hii ni kwamba ni wajibu wa wanajamii kuhimizana kupanda miti na hasa katika sehemu hizi za miinuko ili wasiharibu mazingira yao. Wanapofanya hivi wanaweza kuinua hali yao ya kiuchumi na kijamii na ili kuweza kufaulisha jambo hili wanajamii sharti waishi kwa umoja na upendo kama majirani wema. Anadokeza haya katika uk. 71 kifungu cha 5 anaposema kuwa 'ujirani mzuri wa wakazi wa mji huu ndio unaofariji moyo.' Mwandishi anawashauri wanajamii kuwa ni wajibu wao kuyatunza mazingira wanamoishi kwa kupanda miti kwa wingi na hasa sehemu zenye milima na mabonde. Wakifanya hivi wanapata manufaa mengi kwa mfano, chakula cha kutosha, watoto wanakuwa na afya nzuri na wataliendeleza taifa lao mbele kiuchumi. Pia anawahimiza wanajamii sharti washirikiane na wahimizane katika kuhifadhi mazingira kwa mfano kupanda miti kwani ni wajibu wa kila mwanajamii kufanya hivi. Katika kulishughulikia suala hili tumeongozwa na mhimili wa Nadharia ya Uhalisia unaodai kuwa msanii huwasilisha maisha ya jamii kwa uwazi na usahihi kuwasilisha mambo yanayoonekana katika jamii. Mhimili huu umetuwezesha kuelezea mazingira haya halisi ya mji wa Nyeri.

## 2.5 Uhifadhi wa Bahari na Maziwa

Bahari na maziwa ni mazingira ya kiasili ambayo huwa na manufaa mengi kwa jamii na mfumo wote wa ekolojia kwa jumla. Binadamu akitunza bahari na maziwa huweza kujiinua kiuchumi kwa sababu ya rasilimali za kiasili zinazopatikana humo. Lakini vilevile akihitilafiana nayo huweza kuathirika. Katika diwani *Bara Jingine* (Mberia, 2001) katika shairi 'Kambi Malindi' mtunzi anaonyesha mandhari mazuri ya sehemu hii ya Malindi ambapo watu kutoka bara huwa wanavutiwa nayo na kwenda kubarizi kando ya bahari. Anaonyesha haya anaposema katika uk. 79 kifungu cha 1 kuwa walifika wakati wa alasiri ambapo 'jua lilikuwa na upole' ishara kuwa hali ya anga ilikuwa tulivu na shwari. Mtunzi anaonyesha jinsi mandhari haya yanavyoleta umoja na ushirikiano wa kijamii kwani anaonyesha namna watu wanavyoogelea pamoja kwa furaha na kubarizi kwenye upepo mwanana unaovuma kutoka baharini. Haya yanajidhihirisha anaposema kuwa mchana waliogelea pamoja wanaume na wanawake (uk. 79 kifungu cha 4), ishara kuwa waliyafurahia mandhari haya. Mazingira haya ya bahari yanachangia katika kupunguza uchovu wa fikira miongoni mwa wanajamii. Kwani wanapoburudika kwenye maji ya bahari hurejea makwao wakiwa na miili myepesi. Anadokeza haya katika uk. 81 kifungu cha 11

anaposema kuwa ‘baada ya kuvunja kambi walirejea makwao miili ikiwa myepesi’. Ikiwa na maana kuwa hali hii ya kujiburudisha inasaidia katika kunyoosha viungo vya mwili hali inayoimarisha afya miongoni mwa wanajamii.

Mshairi anaonyesha jinsi walivyofika mjini Malindi wakati wa alasiri ambapo walikaribishwa na maji ya bahari kwenye ufukwe (uk. 70 kifungu cha 1). Hapa mtunzi anaonyesha uzuri wa mandhari haya ya Malindi na jinsi wanajamii wanavyoyafurahia. Anaendelea kusema kuwa ‘Walipiga kambi chini ya mti wa mvinje na kukita hema’ (uk. 79 kifungu cha 2). Kauli hii inaonyesha umuhimu wa miti kwani inaweza ikatumiwa kama makazi na kusetiri wanadamu na wanyama. Pia ni kutokana na miti hii ambapo upepo unaotoka baharini unakuwa laini na kuchangamsha miili. Mandhari haya ya baharini yanaboresha mfumo wa ekolojia kwani watu wanapocheza pamoja wanaimarisha umoja na ushirikiano katika jamii. Mberia anatilia kauli hii mkazo (katika uk. 79 kifungu cha 6) anaposema, ‘walipofika Malindi walikimbia na kukimbizana huku wakitoa jasho’. Vilevile anasema kuwa, ‘walicheza mchezo wa kandanda na kuangushana na kujizoa kwenye mchanga wa bahari’. Hali hii inaonyesha jinsi wanajamii wanavyoyafurahia mazingira haya ya ufuoni.

Pia mandhari haya ya Malindi yanawapa nafasi nzuri ya kujumuika kama jamii na kuleta ule utangamano na uhusiano mwema. Isitoshe, anaonyesha jinsi wanajamii wanavyofurahia rasilimali za kiasili. Anasema kuwa walifurahia kuona ‘tone la ardhi linaloishi pekee kwa ujasiri ambalo mara huyeyuka na mara kuimarika’ (uk. 80 kifungu cha 7). Mandhari kama haya yanasaidia kuinua uchumi wa taifa kwani yanawavutia wageni wa kitalii ambao wanachangia pakubwa katika kuendeleza na kuinua uchumi wa taifa. Binadamu akihifadhi ekolojia vizuri anaweza kupata manufaa mengi na kuboresha hali yake ya maisha. Mberia anaonyesha jinsi watoto wanavyofurahia mandhari haya ya bahari wanaposhikana na watu wazima wakishindana katika michezo mbalimbali kwenye mchanga wa bahari (uk. 80 kifungu cha 8).

Mshairi anaendelea kuonyesha jinsi ambavyo walifurahia ufukwe wa bahari kwa kuona mandhari mazuri ndani ya maji. Haya anayadokeza katika uk. 80 kifungu cha 10 anaposema, ‘walifurahia matumbawe mviringo yenye ukubwa kama wa viazi’ ishara ya jinsi mandhari haya yalivutia. Pia wanyama wa baharini kama vile samaki wa aina mbalimbali wanakuwa kivutio kwa watalii na vilevile kutumiwa na binadamu kama chakula. Mwandishi anaonyesha haya katika uk. 81 kifungu cha 10 anaposema ‘waliona samaki wa rangirangi kama vipepeo arusini’.

Ishara ya jinsi samaki hawa walivyo wengi na wakuvutia. Wanajamii wanashauriwa umuhimu wa kutunza mazingira ambamo wanaishi kama vile bahari na maziwa kwani yanawasaidia kujiburudisha baada ya uchovu mwingi wa kazi. Pia ni wajibu wa wanajamii kutunza rasilimali za kiasili kama vile maji ya bahari kwani yanawavutia watalii na kuinua uchumi na maendeleo ya taifa wanapokuja kuzuru maeneo haya. Mtunzi anasisitiza haya anaposema katika uk. 80 kifungu cha 9 kuwa walifurahia ufukwe wa bahari yenye matumbawe duara yanayovutia macho.

Kulingana na Nadharia ya Uhalisia mwandishi wa kazi ya kifasihi husawiri wahusika, matukio na mandhari yanayokubalika, kuonekana na kuaminika katika jamii ya wakati wake. Kwa mfano, Odhiambo (2017), anaonyesha jinsi wavuvi katika sehemu ya ziwa Viktoria wanavyoathirika kutokana na uchafuzi wa ziwa hili. Wavuvi hawa wanahofia kuwa huenda samaki aina ya tilapia wakaangamia kabisa ikiwa uharibifu huu wa ziwa hili hautasitishwa. Wanalaumu taasisi na viwanda ambavyo vinazunguka ziwa hili kwa kuelekeza maji machafu na kemikali zenye sumu ndani ya ziwa. Jambo hili linaathiri samaki ambao wanahamia sehemu nyingine zenye maji safi. Baadhi ya wanabiashara pia wanatupa vifaa vya plastiki na karatasi za sandarusi kwenye ziwa na kuharibu nyavu. Wavuvi hawa wanaathirika kiuchumi kwani tofauti na hapo awali wanawavua samaki wachache ambao wanawauza kwa bei ya juu ambayo wanajamii wengi hawawezi kuimudu.

## 2.6 Mmomonyoko wa Udongo

Ardhi ni rasilimali muhimu katika kuimarisha mchakato mzima wa ekolojia. Hii ni kwa sababu ndiyo sehemu ambayo mimea hukua na wanyama na binadamu hukita makazi yao. Binadamu anapoharibu udongo matokeo yake ni kuangamia kwa mimea ya kiasili pamoja na wanyama. Wanajamii pia wakijihusisha na baadhi ya mbinu kongwe za kilimo zinachangia udongo kupoteza rutuba. Katika diwani *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014) katika shairi ‘Wanda’ (uk. 29 kifungu 6) mwandishi anasema kuwa ‘kilimo kikongwe kimehujumu ardhi’ na matokeo ya kutumia mbinu hizi kongwe za kilimo ni kwamba wakulima wanazalisha chakula haba suala linalosababisha hali ya njaa nchini. Pia wanajamii wanatahadharishwa dhidi ya kufuga idadi kubwa ya mifugo kwa sababu wanasababisha mmomonyoko wa ardhi wanapochimba na kulegeza udongo wakitumia kwato zao. Anaonyesha haya anaposema katika uk. 31 kifungu cha 7 kuwa ‘kikosi cha taya za ng’ombe kinashambulia nyasi changa’ ishara ya kuwa ng’ombe hawa wanaharibu udongo kwani wanakula nyasi zinazoanza kumea na hivyo kuacha udongo wazi.

Mberia anamsuta binadamu kwa sababu ya kuharibu udongo. Anamrejelea binadamu kama 'adui wa maumbile' (uk. 29 kifungu cha 1), ishara kuwa anajihusisha na shughuli za uharibifu wa mchanga wenye rutuba kwa sababu ya tamaa na ubinafsi wake. Anamrejelea binadamu kama 'hasidi ambaye ameyatia mazingira kitanzi,' (uk. 29 kifungu cha 1), ishara ya kuwa ameyaharibu na matokeo yake ni kuathiri maisha yake na hata ya vizazi vya kesho kwa sababu anayategemea mazingira haya kwani ndio yanayozalisha chakula anachokitumia pamoja na viumbe vingine. Mtunzi anaendelea kuonyesha jinsi wanajamii wanavyohujumu ardhi kwa kuchimba mawe yenye thamani. Anasema kuwa 'wanajamii wanavunja miamba wakitumia sepetu ili kupata mawe ya kuundia udongo wa thamani' (uk.29 kifungu cha 2). Ni wazi kuwa binadamu anapofanya hivi anaharibu ardhi ambayo huwa makazi ya wanyama na wadudu. Shughuli hizi za binadamu zinaathiri ekolojia kwa sababu wanyama hawa wanapokosa makazi hatima yao ni kuangamia au kuhama.

Mberia anamsuta binadamu kwani baada ya miti na nyasi kumea anarudi tena na kuikata miti hii huku akifyeka nyasi ili aweze kuchimba mawe ilhali hii miti na nyasi ndizo ambazo zinashikilia udongo usibebwe na maji ya mvua. Anapofanya hivi makazi ya wanyama na wadudu wanaoishi kwenye udongo yanaharibiwa. Isitoshe, wanyama wanakosa malisho kwa sababu ya upungufu wa mvua na ukosefu wa udongo wenye rutuba wa kuzalishia chakula na matokeo yake ni mauti. Haya yanajitokeza katika uk. 29 kifungu cha 3 anaposema kuwa makazi ambayo yalikuwa mazuri yamegeuka na kuwa 'makaburi ya kuzika ndege, wanyama na binadamu' ambao wameangamizwa kwa sababu ya ukosefu wa chakula cha kutosha. Kwa hivyo kutokana na kifungu hiki, binadamu akiingilia mazingira yake, anahatarisha maisha yake na ya viumbe vingine.

Mwandishi pia anawasuta wanajamii kwa sababu ya kujishughulisha na shughuli za kilimo kila mahali. Wanalima kiholela hata kwenye sehemu ambazo hazistahili. Kwa mfano, kwenye kingo za mito, miinuko ya milima na hata kwenye chemchemi za maji ambazo ni nadra kupatikana. Anawakashifu wakulima wanaolima katika sehemu za miinuko kwa sababu hawaweki matuta ili kuweza kuzuia mmomonyoko wa udongo. Anaonyesha haya katika uk. 30 kifungu cha 5 anaposema kuwa 'wanalima kilimo cha lima-hama-lima bila kuheshimu matuta', ishara kuwa hawahifadhi na kutunza ardhi ambayo wanalima. Pia hawajihusishi katika shughuli za kupanda miti kwa minajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo. Anadokeza haya katika uk. 30 kifungu

cha 5 anaposema kuwa hawatilii maanani upanzi wa miche ya miti'. Vilevile vifaa vya kijadi wanavyotumia wanajamii katika shughuli zao za kilimo vinahujumu ardhi na mimea ambayo inatumiwa kama chakula na mifugo kwani wanavitumia vifaa hivi kufyeka mimea ambayo iko kingoni mwa mito, miinuko ya vilima na kwenye chemchemi za maji. Katika uk. 30 kifungu cha 6 anaonyesha haya anaposema kuwa 'hicho kilimo cha jadi kimepotosha panga'. Katika dokezo hili ni wazi kuwa mtunzi anaonyesha jinsi binadamu anavyoharibu ekolojia kwa kujishughulisha na kilimo cha jadi.

Mtunzi anawazindua wanajamii dhidi ya kulima kando kando ya kingo za mito kwani wakifanya hivi wanalegeza udongo na hivyo kuufanya uwe rahisi kumomonyolewa na maji yanayopita kwa kasi kwenye mito. Pia anawatahadharisha wanajamii dhidi ya kulima kwenye sehemu za miinuko kwani wakati wa msimu wa mvua udongo wote wenye rutuba unabebwa na maji hadi kwenye kingo za mito. Anadhihirisha haya katika uk. 32 kifungu cha 8 anaposema kuwa 'ardhi inashindwa kuhimili matone buka ya mvua.' Ili kuzuia hali hii ni vyema wanajamii wahimizwe na washauriwe watumie vifaa na mbinu mwafaka za kilimo ili kuzuia mmomonyoko wa udongo. Hii ni kwa sababu wakitumia mbinu kongwe za kilimo, wanapata mapato duni na pia wanaharibu ardhi yenye rutuba. Anasisitiza kauli hii katika uk. 30 kifungu cha 5 anaposema kuwa wakijihushisha na kilimo cha jadi watapata mazao duni na kuharibu udongo wenye rutuba. Mwandishi katika kifungu hiki anawashauri wanajamii kuwa sharti watumie mbinu mwafaka za kilimo ili wapate mazao tele huku pia wakiepuka uharibifu wa udongo wenye rutuba.

Mwandishi pia anawashauri wanajamii waepuke kutumia mbinu za zamani katika kilimo zinazohujumu udongo kwani matokeo yake ni kuharibu riziki ya vizazi vya kesho. Wanajamii pia wanaonywa dhidi ya kufuga mifugo wengi ambao wanachangia kwa kiwango kikubwa katika uharibifu wa udongo. Anasema kuwa 'kikosi cha taya za ng'ombe hushambulia nyasi changa,' (uk 31 kifungu cha 8) ishara kwamba ng'ombe hawa wanaharibu nyasi ambazo zinaanza kukua. Mshairi anawashauri wanajamii wafuge idadi ya mifugo ambao sehemu fulani ya ekolojia inaweza kuhimili kwa sababu wasipofanya hivyo wanaathiri nyasi na kusababisha mmomonyoko wa udongo. Hali hii inatokea kwa sababu wakati wa msimu wa kiangazi mifugo hawa wanazoa na kula majani ambayo yamo ardhini kwa sababu ya ukosefu wa nyasi na kunyima miti lishe. Hali ambayo inaharibu udongo wenye rutuba. Haya yanajitokeza katika uk.31 kifungu cha 8 anaposema kuwa katika msimu wa kiangazi mifugo wanakula majani yaliyoanguka na kuinyima

miti lishe na matokeo yake ni miti hii kukosa nguvu za kuhimili ardhi. Ni wazi kuwa katika kifungu hiki mwandishi anawaelimisha wanajamii kuwa udongo wa ardhi ukiwa legevu basi wakati wa mvua maji yanaubeba udongo wenye rutuba kwa wepesi. Katika utungo huu 'Wanda' (uk.31) ni wazi kuwa mwandishi anawasuta wanajamii kwa sababu ya kujihusisha na harakati zinazoathiri mfumo wa ekolojia hali ambayo inamwathiri kiuchumi na kijamii. Anawaonya wanajamii dhidi ya kuchimba ardhi wakitafuta madini yenye thamani kwani wanaharibu udongo. Pia anawashauri watumie baadhi ya mbinu za kisasa katika kilimo ili wapate mazao mengi na kuweza kujiinua kiuchumi na waepuke kufuga idadi kubwa ya wanyama ambayo ekolojia haiwezi kustahimili.

Katika diwani *Rangi ya Anga* utungo 'Wanda' sehemu ya 8 (Mberia, 2014) mwandishi anahuzinika jinsi nyasi zilizofunika ardhi zimeharibiwa na binadamu na kuacha ardhi ikiwa wazi. Anaonyesha haya anaposema kuwa 'nyasi za kuezeka mapaa zilifunika ardhi kwa ukunjufu na kuhimili afya ya udongo' (uk. 38 kifungu cha 1). Ishara kuwa zilikuwa hapo awali lakini zimekatwa na kuharibiwa na binadamu. Pia anakashifu ukataji wa miti kiholela kwani ni jambo ambalo limesababisha chemchemi za mito kukauka. Msimulizi katika kifungu cha kwanza cha shairi anaanza kwa kuonyesha jinsi anavyohuzunika na kusikitika kwa sababu nyasi zilizofunika ardhi zimekatwa zote na binadamu. Anadokeza kauli hii katika uk.38 kifungu cha 1 anaposema kuwa 'miaka ya jana  nyasi za kuezeka mapaa zilifunika ardhi kwa ukunjufu. Hali hii inaonyesha jinsi binadamu anavyohujumu mfumo wa ekolojia kwa manufaa yake mwenyewe. Hii ni kwa sababu baada ya kukata nyasi ardhi inaachwa wazi na udongo unakosa nguvu za kuhimili mvua ya gharika. Mwandishi anadokeza haya katika uk. 38 kifungu cha 1 anaposema kuwa afya ya udongo imeathiriwa baada ya binadamu kukata nyasi. Ni wazi kuwa katika kifungu hiki mtunzi anaonyesha jinsi nyasi zinasaidia katika kuhifadhi udongo wenye rutuba lakini baada ya binadamu kuzikata ardhi inabakia wazi.

Mberia anaonyesha kuwa hapo miaka ya nyuma hungeweza kuona kwekwe za miiba na hata mimea yenye ncha kali. Haya yanajitokeza katika uk. 38 kifungu cha 2 anaposema kuwa 'miaka ya nyuma kwekwe za miba-miba na vimea vyenye ncha kali zilikosa nafasi ya masakini'. Lakini hali hii inaonekana kwa sasa kwa sababu nyasi ambazo zinaleta uzuri wa kijani kibichi na kuzuia mmomonyoko wa udongo zimeng'olewa na binadamu. Hapa mshairi anaonyesha jinsi harakati za binadamu zinavyoathiri uzuri wa mazingira ambao unaletwa na rangi ya kijani kibichi na jinsi

udongo ulivyoharibiwa na shughuli za binadamu. Anadai kuwa hapo awali udongo ambao umeharibiwa ulikuwa hifadhi ya ndege ambapo waliojenga viota na kuwalea makinda wao humo (uk.39 kifungu cha 4) Lakini baada ya binadamu kuharibu makazi haya ndege hawa wanaangamia. Hapa mwandishi anawaonya wanajamii dhidi ya kuharibu ekolojia kwani wakifanya hivyo wanaathiri maisha ya wanyama wengine. Pia wanapoyaharibu mazingira wanaathiri maisha yao kiuchumi kwani ndege hawa, wanawavutia watalii suala ambalo linainua uchumi wa taifa.

Msimulizi anamsuta binadamu kwa kung'oa miti iliyokuwa inang'aa kwa kijani kibichi na kuacha udongo umedhoofika bila mihimili ya kuuzuia usibebwe na maji ya mvua. Katika uk. 39 kifungu cha 4 mtunzi anasema kuwa 'moyo wake umeudhika kwa sababu ya kingo changamfu za mito kuharibiwa'. Anaendelea kuonyesha jinsi mito ambayo walikuwa wanaogelea na kujiburudisha wakiwa watoto ilivyokauka na kujazwa na udongo kwa sababu ya binadamu kuharibu ardhi. Anasisitiza kauli hii katika uk. 40 kifungu cha 6 anaposema kuwa 'mto Thanantu walikochezea kwa kupiga makambi na mbizi sasa umeharibiwa na mmomonyoko wa udongo'.

Mtunzi anaonyesha jinsi watoto wanavyofurahia mazingira ya kiasili kwani ni katika mazingira kama haya wanajifunza mbinu kama za kuogelea na kukuza umoja na ushikamano na kuzuia kujihusisha na uhalifu. Pia anausifu mto huu wa Thanantu kwani unahifadhi baadhi ya wanyama wanaoishi majini. Haya yanajitokeza anaposema katika uk. 40 kifungu cha 4 kuwa mto huu ulikuwa 'makazi ya shangwe kwa wanyama, ndege, wadudu na mimea'. Lakini kutokana na shughuli za binadamu umechafuliwa na mmomonyoko wa udongo suala ambalo limechangia kuangamizwa kwa wanyama hawa. Anadokeza haya katika uk. 39 kifungu cha 4 anaposema kuwa 'magofu ya udongo yamesimama kwa fahari,' ishara ya jinsi udongo huu ulivyojikita ndani ya mto. Hali hii inaathiri ekolojia kwani binadamu hutegemea wanyama hawa kwa chakula kama vile samaki ambao huwa na madini ambayo husaidia kukua kwa ubongo wa binadamu.

Mberia anaendelea kuonyesha jinsi binadamu anavyoharibu makazi ya wanyama, wadudu na ndege kwani baadhi ya viumbe hawa wanakufa kwa sababu ya kukosa mahali pa kujisetiri kutokana na jua kali baada ya udongo ambao ndio makazi yao kuharibiwa. Anadokeza haya katika uk. 40 kifungu cha 5 anaposema 'wadudu kama vile nyungunyungu wanaangamia kwa jua kwa sababu udongo wanaotumia kujengea makazi ili kuweza kujizuia na maadui umeharibiwa.' Ni wazi kuwa kutokana na kifungu hiki kabla ya binadamu kuhitilafiana na makazi haya,

wadudu na ndege walikuwa na makazi ambayo waliweza kujisitiri kutokana na miale ya jua na wanyama wengine hatari. Lakini baada ya binadamu kuharibu ekolojia wadudu hawa wanaachwa kuangamia. Mtunzi anawashauri wanajamii kuwa ni wajibu wao kuhifadhi na kutunza viumbe vinaomzingira. Katika kifungu cha mwisho mtunzi anaonyesha jinsi ukulima wa kiholela katika sehemu za miinuko na ufugaji wa wanyama wengi wanaoathiri udongo kwa kwato zao hasa wanapokwenda kunywa maji mitoni unavyoathiri kingo za mito na matokeo yake ni mmomonyoko wa udongo ambao unachafua maji na kuharibu makazi ya wanyama wanaoishi majini. Udongo huu pia hubeba madini yenye sumu kali ambayo inahatarisha maisha ya wanyama hawa wa majini. Anaonyesha haya katika uk.40 kifungu cha 6 anaposema kuwa mto Thanantu umeharibiwa kutokana na 'mikono hasiri na kwato za ufugaji shakiri,' ishara ya kwamba umeharibiwa na binadamu kukata miti inayozuia mmomonyoko wa udongo na kuwafuga wanyama ambao wanahujumu ardhi kutokana na kwato na matokeo yake ni kwamba wakati wa msimu wa mvua mchanga huu unabebwa na kuelekezwa kwenye mito.

Katika sehemu hii ni wazi kuwa mtunzi anawashauri wanajamii wasihitilafiane na ekolojia. Anawashauri wanajamii wasikate nyasi zinazosaidia kukinga ardhi kwa 'bidii na ujasiri' (uk.38 kifungu cha 2), ishara kuwa zinasaidia kuhimili udongo usibebwe na maji ya mvua. Pia anawatahadharisha wanajamii dhidi ya kukata miti ya kiasili ovyoovyo kama vile: miringa, migunga na mikoma (uk. 39 kifungu cha 4) inayosaidia kuzuia mmomonyoko wa udongo kwani mizizi yake hushikilia udongo usibebwe na maji ya mvua. Katika kuliangazia hili suala tumeongozwa na mhimili wa Nadharia ya Uhalisia unaodai kuwa msanii huwasilisha mambo yanayoonekana katika jamii anamoishi. Kwa mfano, mwandishi ameonyesha jinsi binadamu anasababisha mmomonyoko wa udongo kwa kulima kando kando ya mito. Vilevile Waithera (2018), anazungumzia jinsi mporomoko wa ardhi ulivyowakumba wakazi wa kaunti ya Murang'a nchini Kenya. Wakazi hawa walikumbwa na hatari kwa sababu ya mvua kubwa ilionyesha sehemu hii. Nyumba nyingi ambazo zilijengwa katika sehemu za miinuko ziliporomoka kwa sababbu udongo haukuweza kuhimili uzito wa nyumba hizi. Kulingana na wataalamu wa Jiolojia madhara haya yanasababishwa na binadamu kulima maeneo makubwa, kufyeka mimea na uharibifu wa misitu hali ambayo hulegeza udongo na kukosa nguvu za kuhimili idadi kubwa ya nyumba zinazojengwa. Athari ya shughuli hizi ni kwamba hakuna miti ambayo ina mizizi mirefu ya kushikilia udongo pamoja wakati wa mvua kubwa katika eneo hili

la Murang'a. Kwa hivyo kunaponyesha wanyama na binadamu wanaangamizwa kutokana na mporomoko huu wa ardhi.

Waithera (2018) anaendelea kusema kuwa Kulingana na shirika la kuhifadhi mazingira la National Environment Management Authority (NEMA) hali hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na harakati za wanajamii za kuharibu misitu ili wapate ardhi ya kilimo. Pia ongezeko la watu katika eneo hili la Murang'a limechangia mashamba kugawanywa katika vijisehemu vidogo vidogo na kuongezea udongo uzito wa kuhifadhi idadi hii kubwa ya watu kwa sababu ardhi ikigawanywa katika sehemu ndogo ndogo udongo huwa mwepesi na legevu. Ili kuzuia hali kama hii ni sharti wanajamii waepuke kufyeka mimea ya kiasili na wapande miti kwa wingi ili kuboresha mshikamano wa udongo na kuzui mporomoko wa ardhi.

## 2.7 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia athari ya mtagusano kati ya jamii na mazingira. Mberia amedhihirisha jinsi binadamu na viumbe vingine vinavyoathirika baada ya jamii kuharibu mazingira ambamo inaishi. Kwa mfano, tumeonyesha jinsi uharibifu wa misitu kwa shughuli za kilimo, upasuaji wa mbao na uchomaji wa makaa unavyoathiri ekolojia. Kutokana na uharibifu huu wanyama wanakosa hifadhi na kuangamia kutokana na ukosefu wa lishe. Mito pia inakauka na kuathiri wanajamii kwani maji haya ndiyo yanayotumiwa kuzalisha nguvu za umeme zinazotumiwa kuzalisha bidhaa viwandani. Pia tumedhihirisha jinsi binadamu anavyoharibu ekolojia kupitia ulimaji wa kando kando ya mito na mabwawa na vilevile kwenye miinuko na mabonde. Anapofanya hivi anasababisha mmomonyoko wa ardhi wakati wa msimu wa mvua. Udongo huu unaishia kwenye mito na kuangamiza wanyama wanaoishi majini kwa kukosa hewa safi ya okisijeni. Binadamu pia anaharibu hali ya hewa na ukanda wa ozoni kupitia uzalishaji wa bidhaa viwandani hali inayosababisha ongezeko la joto duniani. Ni wazi kuwa katika shughuli hizi zote binadamu anaharibu mfumo wa ekolojia anaoutegemea yeye pamoja na mimea na wanyama. Mberia anawasuta, na kuwakashifu wanajamii kwa sababu ya kuharibu mazingira. Hata hivyo, anawaelimisha na kuwashauri kuwa ni jukumu lao la kuyalinda na kuyatunza mazingira wanamoishi ili kuhifadhi ekolojia. Hili ni muhimu kwa sababu wanyama, mimea na pia binadamu hutegemeana.

# SURA YA TATU

# ATHARI ZA MASUALA YA KIJAMII KWENYE MFUMO WA EKOLOJIA JAMII

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia na kuonyesha jinsi masuala ya kijamii yanavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii. Hii ni kwa sababu kulingana ns Bronfenbrener (1989) ekolojia jamii ni dhana pana ambayo pia hujumuisha mahusiano, upatano na maingiliano kati ya binadamu na mwenzake. Kwa hivyo tofauti na sura iliyotangulia ambapo tulishugulikia athari ya mtagusano kati ya jamii na mazingira, katika sura hii tumeshughulikia mahusiano baina ya binadamu na binadamu mwenzake na jinsi yanavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii. Tumenuia kuhoji kuwa maingiliano haya ya binadamu na binadamu mwenzake huweza kuathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa njia nyingi kwani jamii hubadilikabadilika kulingana na jinsi binadamu anavyojiendeleza kimaisha. Masuala ya kijamii ambayo tumeyashughulikia na kuonyesha jinsi yanavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii ni pamoja na: ufuska, dawa za kulevya, mimba na ndoa za mapema, ubaguzi wa kijinsia ukeketaji wa mtoto wa kike na teknolojia ya kisasa.

## 3.1 Ufuska

Ufuska ni hali ya wanajamii kujihusisha na uasherati au uzinzi nje ya ndoa. Suala hili linaathiri mahusiano baina ya wanajamii kwani husababisha migogoro katika ndoa na ueneaji wa maradhi kama vile UKIMWI. Katika diwani *Bara jingine* shairi 'Giza Mbele' (Mberia, 2001) mtunzi anaonyesha jinsi wanafunzi wa kike wanavyojiingiza katika mapenzi ya kiholela wangali bado shuleni. Kando na wao kwenda shuleni, hawapati elimu kama jamii inavyotarajia kwani baada ya kushinda na walimu wao mchana kutwa, jioni magari ya kifahari yanawangoja nje ya lango la shule na kuwapeleka sehemu za burudani. Mtunzi anaonyesha haya (uk.26 kifungu cha 3) anaposema kuwa 'karibu na lango la shule kuna benzi jekundu limewasubiri kama chatu' ikiwa na maana kuwa wanawangoja kwa hamu na ghamu ili wajihusishe kimapenzi nao.

Ni wazi kuwa katika kifungu hiki wanaowabeba wanafunzi hawa wa kike hadi maeneo ya burudani ni matajiri ambao kwa hakika wako na mali. Haya yanajitokeza (uk. 26 kifungu cha 3) mtunzi anaposema kuwa katika lango la shule benzi jekundu linawangoja kwenye lango ishara ya kuwa wao ni matajiri. Baadhi yao wanatumia nafasi waliyonayo katika jamii na mali

walionayo kuwahadaa wasichana hawa kimapenzi kwani wengi wao wanatoka katika familia ambazo hazijiwezi kiuchumi. Mwandishi anadokeza haya katika uk. 26 kifungu cha 4 anaposema wanafunzi hawa 'wanaongozwa na umasikini nyumbani,' ishara ya kuwa hali ngumu ya maisha ndiyo inawafanya kushawishiwa haraka kwa madai ya kupewa mapenzi na hawa matajiri.

Mshairi anaonyesha uozo ulioko katika jamii kwani watu hawaiheshimu tena asasi ya ndoa. Badala ya matajiri hawa kuwaelekeza wasichana hawa wa shule ili wakue katika misingi ya kimaadili ndio wanaochangia katika kuporomosha maadili. Hali hii ni kinyume na siku za kale pale ambapo wazee walionekana kama kielelezo cha jamii na taasisi za ndoa zilikuwa zinaheshimiwa sana. Lakini kutokana na uigaji wa utamaduni wa kigeni na mifumo mipya ya kiteknolojia mifumo ya kijamii imebadilika na wazee wanajihusisha kimapenzi na wasichana wadogo kwa kuwahadaa kimapenzi kupitia pesa. Wasichana hawa wa shule wanajiingiza katika mapenzi na wazee walio na mali kwa sababu ya kutojua kwani bado wao ni wadogo. Haya yanajitokeza (uk.26 kifungu cha 4) mwandishi anaposema wanahadaiwa kwa 'kutojua akili,' ishara kuwa hawajui madhara ya kujihusisha na aina hii ya mapenzi ambayo yanachangiwa na hali ngumu ya kiuchumi.

Kwa hivyo ni bayana kuwa wasichana wa shule wanajihusisha kimapenzi na wazee kwa sababu ya kutojua athari yake na umasikini unaowakumba nyumbani. Baadhi ya wazazi huwachochea wana wao kujiingiza katika mapenzi ya aina hii ili wapate riziki. Mtunzi anaendelea kuonyesha athari ya mahusiano haya anaposema kuwa baada ya wanafunzi hawa kujihusisha kimapenzi matokeo yake ni mimba za mapema na hatimaye wanaacha shule. Mtunzi anasisitiza haya anaposema katika uk. 27 kifungu cha 7 kuwa 'katika udongo kunachipuka mche kwenye sare ya shule,' ishara ya kuwa wasichana hawa wanapata mimba. Kauli hii ya mtunzi inawakashifu wanaume ambao wanakatisha masomo ya wanafunzi wa kike kwa kuwapachika mimba. Anachora taswira ya wanaume ambao hawana hisia wala huruma kwani hawajali mustakabali wa watoto hawa kwani katika uk. 27 kifungu cha 6 mtunzi anasema 'wanaachwa wameanguka kama maziwa yaliyomwagika,' ikiwa na maana kuwa wameharibiwa maisha yao machanga.

Kwa upande mwingine wazazi wanaachwa kwenye njia panda wasijue la kufanya baada ya watoto wao kupachikwa mimba na kuacha masomo. Pia wanaachwa na uchungu kwani wanakumbana na dhiki nyingi wakati wa kuwasomesha wakiwa na matarajio kuwa watakuja kuinusuru familia yao baada ya kupata elimu. Mwandishi anadokeza haya katika uk. 27 kifungu

cha 8 anaposema kuwa wazazi wanachomwa na maswali mengi akilini wakijiuliza ni nani aliwapachika wana wao mimba baada ya kuwasomesha kwa dhiki. Ni wazi kuwa watoto wa kike wakijihusisha na mapenzi wangali bado shuleni wanaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwani wanapopata watoto wanaacha masomo na kuanza ulezi. Wengi wao huwa hawana uwezo wa kuwatimizia watoto hawa mahitaji yao ya kimsingi kama vile chakula na mavazi na huishia kujiingiza katika uhalifu, ukahaba na matumizi ya dawa za kulevya ili waweze kujikimu kimaisha. Watoto hawa wanapokosa chakula na mavazi wanakumbwa na maradhi kwa sababu ya ukosefu wa lishe bora na matokeo yake ni jamii kukosa nguvu kazi za kuzalisha rasilimali zitakazotumiwa na binadamu na viumbe vingine.

Ni wazi kuwa mtunzi anaikashifu jamii na hasa wazee walio na mali kwa kuwahadaa watoto wa shule na kujihusisha kimapenzi nao bila kujali maisha yao ya baadaye. Mwandishi anasema katika uk 26 kifungu cha 4 kuwa wakitoka shuleni huwa wanangojewa ‘Kama windo katika mtego wa hayawani.’ Pia mwandishi anawashauri walimu na wazazi kuwa ni jukumu lao kuwaongoza na kuwalea wana wao kwa kufuata maadili ya kijamii na kuwa kielelezo chema. Vilevile anawashauri wanafunzi wa kike wajihadhari kujihusisha kimapenzi kiholela kwani watapata mimba za mapema na hata magonjwa kama vile UKIMWI na hatima yao ni kuacha masomo na kuwa mzigo kwa jamii. Wanafunzi hawa wakikosa elimu wanaathiri usawa wa mfumo wa ekolojia kwa sababu jamii ndiyo inawategemea katika uongozi wa kesho na shughuli za kuzalisha mali wakitumia teknolojia ya kisasa ambayo inahitaji elimu. Pia wanaathiri mfumo wa kijamii kwa sababu wakipata mimba za mapema wanakuwa wazazi wangali wachanga na hawana uwezo wa kujikimu kimaisha na matokeo yake ni kuwategemea wazazi ambao hata wao hawajiwezi kiuchumi. Kauli hii inaoana na mhimili wa Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia unaodai kuwa maendeleo katika jamii huathiriwa na vitu au viumbe ambavyo vinamzingira binadamu kwa mfano wazazi, marafiki na taasisi za elimu.

## 3.2 Dawa za Kulevya

Dawa za kulevya na pombe ni tatizo la kijamii linaloathiri mfumo wa ekolojia jamii. Matumizi yake huathiri maisha ya mtu binafsi, familia na jamii kwa jumla. Wazazi wanakosa kuwajibikia familia zao kwa sababu ya kujihusisha na unywaji wa pombe kiholela. Wanakosa muda wa kuzungumza na kuwashauri wana wao. Katika diwani *Bara Jingine*, shairi ‘Ni Sumu kwa Watoto’ (Mberia, 2001) mwandishi anawakashifu baadhi ya wazazi kwa sababu ya kuwapa

wana wao matumaini ambayo hayana mwelekeo. Haya yanajitokeza katika uk 49 kifungu cha 1 mtunzi anaposema kuwa 'wazazi wanahatarisha watoto kwa ndoto zao leweshi,' ishara kuwa masuala wanayozungumzia na kuwapa watoto wao hayana manufaa.

Mtunzi anawashauri wazazi watenge muda wao na kuwaelekeza watoto kuhusu maadili na mienendo mizuri. Hii ni kwa sababu wazazi ni kiungo muhimu katika jamii na hasa mzazi wa kiume ambaye kulingana na utamaduni wa mwafrika ndiye kiongozi wa familia. Lakini mzazi akijihusisha na unywaji wa pombe anaharibu uhusiano uliopo kati yake na familia yake. Mtunzi anadokeza haya katika uk. 49 kifungu cha 1 anaposema kuwa 'wazazi wasijenge ukuta baina ya watoto wao,' ikiwa na maana kuwa wawe na uhusiano wa karibu na watoto ili waweze kuwaelekeza. Anachosisitiza Mberia katika kauli hii ni kuwa mzazi anastahili kuwa karibu na watoto wake ili aweze kuwashauri na kuwaelekeza. Hii ni kwa sababu watoto hawa ndio viongozi watakaoshikilia na kuiongoza jamii katika siku za usoni. Lakini wasipofanya hivyo, familia zinavunjika na wanaoumia ni watoto kwani hawana watu wa kuwaelekeza, kuwaongoza na hata kuwatimizia mahitaji yao ya kila siku.

Wazazi wengi hukosa muda wa kuzungumza na wana wao kwa sababu muda wao mwingi wanautumia katika sehemu za burudani wakibugia mtindi. Mtunzi anadokeza haya katika uk 49 kifungu cha 3 anaposema kuwa wazazi wanatenganishwa na watoto wao kwa 'mazoea ya daima ya kunywa moja baridi' ikiwa na maana kuwa wamezoea na wanatumia muda wao mwingi wakinywa pombe na kusahau kuwaelekeza wana wao. Wazazi wanashauriwa kuwa sharti wajaribu kutenga muda wao na kuwazungumzia watoto wao. Hii ni kwa sababu wasipofanya hivyo wanapotoka kimaadili na wanafunzwa na marafiki kama anavyosema Bronfenbrenner (1989) kuwa maisha ya wanajamii huweza kuathiriwa na watu walio mbali kidogo nao kama vile marafiki.

Mwandishi pia anawakashifu wazazi ambao baada ya kutoka kazini hawaendi nyumbani moja kwa moja bali wanaingia kwenye klabu na kunywa pombe hadi saa nane za usiku. Anasema kuwa hali hii inasambaratisha mfumo wa kifamilia kwani akirejea saa nane za usiku anawakuta watoto wamelala na hivyo basi kukosa muda wa kuzungumza nao. Mtunzi anadokeza haya katika uk. 49 kifungu cha 3 anaposema 'wazazi wanarejea nyumbani saa nane usiku baada ya kutoka kwenye vilabu'. Anachosisitiza mtunzi katika kauli hii ni kuwa wazazi lazima watenge muda wa kukaa na kuzungumza na watoto wao. Wasipofanya hivyo watoto hawa wataelekezwa

na marafiki zao na huenda wasielekezwe inavyopasa na kujikuta wameingizwa katika uhalifu au matumizi ya dawa za kulevya.

Mtunzi anaendelea kuwasuta wazazi kwa kuwapa wana wao pesa nyingi kupindukia eti ni ishara ya mapenzi. Haya yanajitokeza katika uk. 50 kifungu cha 5 mtunzi anaposema 'wazazi wanawajeruhi watoto kwa kuliwaza kwa pesa' na wakifanya hivi watoto hawa wanapata hela nyingi wanazozitumia katika kununua sigara na kujihusisha na ulevi. Mtunzi anasisitiza kauli hii katika uk. 50 kifungu cha 5 anaposema 'watoto wakipata pesa chungu nzima zinawafikisha kwenye sigara na ulevi'. Hali hii ni hatari kwani wakijiingiza katika ulevi maadili yao yanaporomoka. Wanadhoofika kiafya hivi kwamba hawawezi kujifanyia kazi na matokeo yake nikurejesha maendeleo ya taifa nyuma kwani taifa linakosa nguvu kazi za kuzalisha rasilimali viwandani.

Ni bayana kuwa ikiwa wazazi hawana uhusiano na mazungumzo na wana wao kwa sababu ya kujihusisha na ulevi basi wanaathiri mfumo wa ekolojoia jamii baina ya binadamu na binadamu mwenzake. Hii ni kwa sababu wazazi sharti wawaelekeze watoto wao kwani ndio tegemeo la kuendeleza taifa kiuchumi na kijamii katika siku zijazo. Lakini wazazi wakijihusisha na ulevi na kukosa muda wa kuwaelekeza watoto wao, wanaelekezwa vibaya na watu wanaowazunguka kama marafiki na huenda wasielekezwe vizuri. Bronfenbrenner (1989) anasema kuwa maisha ya wanajamii yanaweza kuathiriwa na watu wa familia au watu wa mbali kidogo kama vile marafiki na walimu. Kwa hivyo watoto hawa wasipoelekezwa vizuri wanaishia kujiingiza katika uhalifu na kuathiri mtagusano na mwingiliano mwema baina ya wanajamii. Pia vijana hawa wakijiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya wanaathirika kiafya na kukosa nguvu za kufanya kazi. Hali hii inaathiri mfumo wa ekolojia kwani viumbe vingine vinategemea rasilimali kama vile chakula kinachozalishwa na nguvu kazi ya vijana. Vijana hawa pia wakitumia dawa za kulevya jamii inagharamikia matibabu kwa kutumia hela nyingi kuwatibu fedha ambazo zingetumika kwa mfano kuzalisha vyakula ambavyo vingetumika na wanajamii na wanyama wengine kwa jumla.

### 3.3 Mimba na Ndoa za Mapema

Mimba na ndoa za mapema inarejelea hali ambapo watoto wa kike wanapata mimba wangali wachanga na hatimaye wanaozwa kabla hawajamaliza masomo yao. Ni suala la kusikitisha kuwa taasisi kama vile shule ambazo zimepewa majukumu ya kuwasomesha na kuwaelekeza

wanafunzi zinageuka na kuwa vituo vya dhuluma za kimapenzi. Watu waliopewa majukumu ya kuziongoza taasisi hizi wanatumia nafasi na vyeo vyao kuwadhulumu wanafunzi wa kike kimapenzi. Katika diwani *Bara Jingine* (Mberia, 2001) katika shairi 'Flora na Wenzake,' mwandishi anaonyesha namna mwalimu mkuu anawahadaa wanafunzi wafike shuleni mapema kwa shughuli za masomo. Lakini inabainika kuwa yeye hufanya hivyo ili apate nafasi ya kujihusisha kimapenzi na wanafunzi wake wa kike. Mshairi anadokeza haya katika uk. 33 kifungu cha 4 anaposema kuwa 'darasa la nane limejaa wanafunzi kama jinsi ambavyo mwalimu mkuu alivyokuwa ameagiza'. Mwalimu mkuu hakuwa anasema hivi akiwa na nia ya kuwasomesha wanafunzi mbali ni apate nafasi ya kujihusisha kimapenzi nao.

Mtunzi anawakashifu viongozi wa shule na hasa walimu wakuu kwa sababu ya kujihusisha kimapenzi na wanafunzi wao wa kike. Mwandishi anaonyesha haya katika uk. 33 kifungu cha 5 anaposema kuwa 'ofisini mwalimu mkuu anatupa macho kama mburukenge na miali kama ya nyegere,' ishara ya jinsi anawatamani wasichana hawa kimapenzi. Mwalimu mkuu anawahadaa wanafunzi kuwa wafike mapema shuleni ili awafunze lakini ukweli ni kwamba anaongozwa na tamaa na ubinafsi na ndiposa hajali mustakabali wao. Haya yanajitokeza katika uk. 36 kifungu cha 15 mtunzi anaposema kuwa 'jua humkuta Mwalimu Mkuu shuleni' akiwangoja wanafunzi ili ajihusishe nao kimapenzi. Hali hii inaonyesha uozo ulioko katika jamii ya kisasa pale ambapo suala la heshima kati ya wazee na vijana limetupwa katika kaburi la sahau. Kwa hivyo ni jambo la fedheha na la kuhuzunisha kuona kuwa watu waliopewa majukumu na jamii ya kulinda watoto wao, ndio wanaowaharibu kimaadili.

Mwandishi anawakashifu walimu hawa ambao wanawapachika wasichana wa shule mimba na kuwaharibia maisha yao ya baadaye. Anadokeza haya katika uk. 35 kifungu cha 11 anaposema kuwa 'sare ya Flora inapanda pole pole na kukataa kushuka' ishara ya kuwa tayari yu mjamzito na matokeo yake ni kuacha masomo. Mtunzi analikashifu jambo hili kwani wasichana hawa hukumbana na hali ngumu ya kuwalea watoto ambao hawana baba na hatimaye wanajiingiza katika uhalifu ili waweze kukidhi mahitaji yao ya kimsingi. Pia watoto hawa wanalelewa katika mandhari ya familia isiyo na msingi suala ambalo linaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa njia hasi kwa sababu watoto hawa wanakosa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, mavazi na makazi. Watoto ambao wamelelewa na wazazi wote wawili aghalabu huweza kupata mahitaji haya ikilinganishwa na wanaolelewa na mzazi mmoja. Bronfenbrenner (1989) anasema kuwa

familia ni mojawapo ya kigezo kinachoathiri mfumo wa ekolojia. Katika mifumo ambapo familia ni thabiti, taifa huweza kushuhudia maendeleo faafu ya kiuchumi na kijamii.

Mtunzi pia anawakashifu wazazi kwa sababu ya kutowajibika na kuwaelekeza watoto wao. Wazazi wengi wanawaachia walimu majukumu ya ulezi na kusahau kuwa ni wajibu wao kama wazazi kuwalea wana wao ili waweze kufahamu changamoto wanazokumbana nazo na kuwashauri. Hii ni kwa sababu wazazi wanagutukia kuwa watoto wao wamepachikwa mimba na kupotoka kimaadili baada ya athari kuonekana. Mtunzi anasisitiza haya katika uk. 36 kifungu cha 16 anaposema kuwa wazazi ndio sasa wameelewa maana ya Mwalimu Mkuu kusema kuwa 'watoto wafike mapema shuleni'. Katika dokezo hili ni wazi kuwa wazazi na walezi wanagundua kuwa mwalimu mkuu alikuwa anajihusisha kimapenzi na wana wao lakini tayari wamepachikwa mimba na madhara yashatokea. Mwandishi anaonyesha haya katika uk. 35 kifungu cha 12 anaposema kuwa, Flora ni mja mzito. Kauli hii 'Ilimchoma nyanya mlezi kama mishale yenye sumu,' ishara ya jinsi alivyokumbwa na uchungu kwani hakutarajia kadhia kama hii kutoka kwa mwalimu mkuu.

Mberia pia anaonyesha utepetevu wa taasisi ambazo zimepewa majukumu ya kuwalinda na kuwatunza wanafunzi lakini badala yake zinageuka na kuwa vituo vya dhuluma za kimapenzi. Tunaarifiwa katika uk. 35 kifungu cha 16 kuwa nusu ya wasichana katika darasa la nane walikuwa wamefunzwa 'utu- uzima', ishara kuwa mwalimu mkuu alikuwa amejihusisha nao kimapenzi. Walimu wakuu ambao wanajihusisha kimapenzi na wanafunzi wa kike wanawaharibia maisha yao kwani wanapoacha masomo wanajihusisha na uhalifu ili waweze kujikimu kimaisha hali ambayo inaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu jamii inastahili kuishi kwa amani bila migogoro na mivutano. Hii ni kwa sababu jamii ikikumbwa na migogoro huathiri maendeleo ya taifa kwani uzalishaji wa rasilimali kama vile chakula kinachotumiwa na viumbe vingine hautawezekana na matokeo yake ni viumbe hivi kuangamia kutokana na njaa. Wazazi pia wanakashifiwa kwa sababu ya kuzembea katika majukumu yao ya kuwaelekeza wana wao. Wanaachia walimu majukumu ya ulezi badala ya kuwaelekeza watoto wao. Hata hivyo anawashauri kuwa ni vyema wafahamu hali ya watoto wao hata kama wako shuleni .

Katika shairi *Rangi ya anga* sehemu ya 6 (Mberia, 2014) mwandishi anaonyesha jinsi wazazi wanavyowaoza watoto wao wa kike wangali wadogo ili wazazi waweze kujikimu kimaisha. Haya yanajitokeza katika uk 8 kifungu cha 1 pale ambapo mzazi anamwambia mtoto wake wa

kike wa miaka kumi na minne aolewe na Mzee Mali ili awazimie moto wa umaskini ikiwa na maana kuwa wazazi wanawaona watoto hawa kama chombo cha kujikimu kiuchumi. Pia kauli hii inaonyesha jinsi wazazi wanavyowatumia watoto wao wa kike kama vyombo vya kuchumia mali. Wazazi wanawalazimisha watoto wao kuacha shule ili waweze kuolewa na wazee wenye mali ili kujiauni kutoka kwenye lindi la umaskini. Wazazi wanapofanya hivi wanayaharibu maisha ya watoto hawa kwani wana haki ya kuendelea na masomo ili waendeleze mifumo ya kijamii katika siku zijazo. Wazee hawa wanaongozwa na utamaduni potovu ambao unamwona mtoto msichana kama chombo cha kujitajirisha. Utamaduni wa aina hii haumthamini mtoto wa kike hata kidogo. Mtunzi anaendelea kukashifu mila na tamaduni ambazo zinakwamiza binadamu kuendelea mbele kiuchumi na kijamii. Hii ni kwa sababu wasichana hawa wanapokatishiwa masomo yao na kujihusisha na ndoa za mapema wanapitia maisha magumu ya kuwa walezi bado wakiwa wachanga badala ya kuendelea na masomo ili wapate ujuzi wa kuendesha uchumi wa nchi.

Msimulizi pia anawakashifu wazazi kwa sababu ya ubinafsi na tamaa ya mali bila kujali mustakabali wa watoto wao.Wanaona ng’ombe na mbuzi wanaowapata kama mahari ni muhimu kuliko maisha ya watoto hawa. Haya yanajitokeza katika uk. 8 kifungu cha 1 pale mzazi anamuuliza mtoto wake wa kike ‘mbona usiolewe ili tupate mahari ya ng’ombe na mbuzi?’ Mtunzi anawashauri wazazi kuwa ni jukumu lao kuona wana wao wamesoma badala ya kuwaoza mapema kwani wakifanya hivyo wanahitilafiana na maisha yao ya baadaye. Wazee wakioa wasichana wachanga ni ishara ya jinsi mfumo wa ekolojia jamii ulivyoathirika kwa sababu mahusiano kama haya si ya heshima bali ni ya kidhuluma na unyanyasaji. Kwa hivyo mtunzi anasisitiza kuwa jamii sharti ielimishwe kuhusu tamaduni ambazo zimepitwa na wakati na wazazi wanaopatikana wakiwaoza mabinti zao wachukuliwe hatua kali za kisheria kwani ni haki ya kila mtoto kupata elimu. Hii ni kwa sababu wasichana hawa wakiozwa wangali bado na umri mdogo hawana uwezo wa kufikiria na kujiamulia baadhi ya masuala katika jamii kwani hawajakomaa kimawazo. Pia pindi wanapoolewa mapema wanakuwa wazazi wachanga na kupewa majukumu ya kifamilia masuala ambayo hawayafahamu. Vilevile wasichana hawa huishia kupata idadi kubwa ya watoto ambao hawawezi kuwakimu kimaisha. Hali hii pia hutokea kwa sababu hawana maarifa yoyote kuhusu mbinu za upangaji uzazi na wakati ambapo jamii inapata watoto wengi ambao ekolojia haiwezi kustahamili inaathirika kwa kukosa mahitaji ya kimsingi kama vile: mavazi, chakula na makazi.

Ili kuepukana na adha hii ya ndoa za mapema ambazo zinaathiri mfumo wa ekolojia jamii zinastahili kupigwa marufuku na wazazi wanaozitekeleza wachukuliwe hatua kali za kisheria. Hali hii ya watoto wadogo kuozwa kwa wazee walio na mali inajidhihirisha katika maisha halisi. Kwa mfano, kulingana na Chuma (2018, August 4) anaelezea jinsi msichana wa miaka minane alivyoozwa kwa mwanamume wa makamo katika eneo la Baringo nchi Kenya ili wazazi wapate ng'ombe na mbuzi kama mahari. Baada ya msichana huyu kukosa kupata mtoto alifukuzwa na wazazi wake wakumuoza kwa mwanamume mwingine. Suala kama hili linaathiri ekolojia jamii kwa sababu mtoto kama huyu anaingizwa katika mfumo wa ndoa ilhali hawezi kujilisha wala kujivisha.

Mwandishi vilevile anaonyesha uozo uliopo katika vyuo vikuu. Anaonyesha jinsi taasisi hizi zimegeuka na kuwa vituo vya kuwadhulumu wanafunzi wa kike. Baadhi ya wahadhiri wanajihusisha kimapenzi na wanafunzi na hata watoto wadogo na baada ya kuwapachika mimba wanawatelekeza. Mtunzi anadokeza haya katika uk. 9 kifungu cha 2 anaposema kuwa 'alisikia profesa akijigamba jinsi alivyomchumbia msichana wa miaka kumi na mitatu'. Kauli hii inadhihirisha jinsi mifumo ya kijamii ilivyobadilika kwani badala ya taasisi kama hizi kuwaelekeza watoto wadogo zinawanyanyasa kimapenzi. Hali hii inasababishwa na upotofu wa maadili unaoletwa na uigaji wa utamaduni wa kigeni ambao unaletwa na mifumo mipya ya kiteknolojia kama vile simu na mitandao. Ni hali ya kusikitisha kuona kwamba badala ya taasisi za elimu zitumike kuendeleza maarifa ya kiuchumi na kijamii zinatumika kama vituo vya kuporomosha maadili.

Ni suala la kusikitisha kuona waliosoma wakiharibu maisha ya wasichana wadogo kwa kuwakatishia masomo na hatima yao ni kujiingiza katika uhalifu suala ambalo linaathiri kuwepo kwa mazingira mazuri ya kufanyia kazi na hasa mijini. Matokeo yake ni taifa kushindwa kuzalisha rasilimali zinazotumiwa na binadamu na viumbe vingine. Waliosoma wanastahili kuwa katika mstari wa mbele katika kutetea haki za watoto hawa kwa sababu wamesoma na wanaelewa madhara ya kutomsomesha mtoto wa kike. Msimulizi pia anawakashifu na kuwasuta wanawake ambao wamesoma na kuelimika. Badala ya kupigania haki za mtoto wa kike wasiozwe kwa lazima, wanasema kuwa sharti utamaduni uheshimiwe na lazima waozwe kwani ni desturi na kanuni za kitamaduni. Mtunzi anadokeza haya katika uk 10 kifungu cha 4 anaposema:

Profesa wa kike
Mwenye shahada ya uzamili
Ateteapo viini vya matende, akibeua
Hiyo si taasubi ni desturi
Hizo si nyanyaso ni kanuni za kijadi
Hizo si dhuluma ni kaida za utamaduni

Katika sehemu hii ni wazi kuwa mwandishi anaonyesha jinsi mifumo ya ekolojia jamii inavyoathiriwa na mimba za mapema na ndoa za lazima. Anawakashifu wazee wanaowaoza wasichana wao wakiwa wangali wachanga ili wapate mali. Pia anawasuta baadhi ya wasomi ambao wanategemewa na jamii kulinda haki za watoto lakini ndio wako katika mstari wa kwanza kuzikiuka. Masuala haya yanatokea katika hali halisi ya maisha. Kwa mfano, kulingana na Aineah (2018, August 2) anaelezea jinsi mwanafunzi mmoja wa kike katika Chuo Kikuu kimoja nchini Kenya alivyokiri kujihusisha kimapenzi na mhadhiri wake ili aweze kupata alama za juu katika mtihani. Mwanafunzi huyu anakiri kuwa baada ya mahusiano haya alipata mimba kisha akaiavya. Mambo kama haya yanaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu uavyaji wa mimba ni suala la kikatili ambalo linapunguza idadi ya wanajamii katika taifa husika na hivyo basi kuathiri nguvu kazi za kuzalisha mali. Isitoshe, kitendo cha kuavya mimba ni hatari hivi kwamba mhusika huenda aage dunia au alemazwe kiafya na kukosa nguvu za kujitafutia mahitaji ya kimsingi kama vile chakula na mavazi. Matokeo yake ni kutegemea wanajamii wengine ambao pia wanataabika katika kujitafutia riziki.

## 3.4 Ubaguzi wa Kijinsia

Jamii ikimbagua mwanamke katika hali ya kurithi mali ya jamii ni suala ambalo linarudisha maendeleo ya taifa nyuma na kuathiri mfumo wa ekolojia jamii. Katika shairi *Rangi ya Anga* sehemu ya 2 (Mberia, 2014) mtunzi anaonyesha jinsi utamaduni unavyomtweza mwanamke kwa kumnyima haki ya kurithi mali na hasa ardhi. Haya yanajitokeza katika uk. 3 kifungu cha 4 mtunzi anaposema kuwa ‘kulingana na ibara za kitamaduni mwanamke hastahili kurithi mashamba’. Hata hivyo wanawake wanajaribu kupigania haki ya usawa na wanaume ila hawafui dafu. Mwandishi anadokeza haya katika uk. 3 kifungu cha 1 anaposema ‘damu inatiririka mwanamke akipigania haki za usawa’ ishara ya jinsi anavyokazania kuona kwamba amepata haki yake ya kurithi . Kitendo cha kumnyima ardhi mwanamke kinaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu hii ardhi ndio binadamu anatumia kuzalisha chakula anachotumia kujiinua kiuchumi. Kwa mfano tendo la kuwanyima wajane haki ya kurithi ardhi kwa minajili ya kuwa

utamaduni hauruhusu linaathiri maisha ya watoto walioachiwa wajane hawa. Maisha ya watoto hawa yanabadilika kwa sababu walezi hawa wanaachwa bila chochote cha kuwalisha, kuwavisha na kuwaelimisha. Hatima ya watoto hawa ni kujiingiza katika uhalifu, matumizi ya dawa za kulevya na ukahaba ili kuweza kujikimu kimaisha. Mtunzi anakashifu mila hizi na tamaduni kwa sababu zinamkandamiza mwanamke ambaye jamii inamtegemea katika maendeleo ya taifa. Wanawake wanapojaribu kupigania haki zao za usawa wanakumbana na pingamizi nyingi kwa sababu hawana nguvu kama wenzao wa kiume. Mtunzi anasema kuwa hata wanakumbana na kichapo. Haya yanajitokeza katika uk.2 kifungu cha 1 anaposema:

Kwamba kuwa navyo mkononi
Ni mpini wa upanga mkali
Mkononi mwa mwanamume
Na kiganja cha mwanamke
Kinapoishiwa na stahamala
Hushika makali ya bapa
Ikatiririka damu bila hatia.

Kwa hivyo mtunzi anasisitiza kuwa jamii ikumbatie mabadiliko na kuwapa wanawake haki sawa na wanaume ili kuendeleza mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu hawa wawili wanategemeana na kusaidiana katika kuboresha maisha ya jamii.

Mwandishi pia anakashifu jinsi mwanamke anavyodhalilishwa na kubezwa kwa sababu ya kujifungua mtoto wa kike ilhali mwanamume anajiondolea lawama. Hali hii inaathiri mahusiano katika jamii na kuathiri mfumo wa ekolojia jamii hivi kwamba wanawake wanatengwa na jamii na kunyimwa nafasi ya kuchangia katika maendeleo ya taifa. Matokeo yake ni taifa kukosa nguvu kazi ambazo zinazalisha rasilimali ambazo zinatumiwa na wanajamii na viumbe vingine kwani wanaume pekee hawawezi kufaulisha jambo hili. Katika shairi *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014) sehemu ya 4 uk. 6 kifungu cha 1 mtunzi anasisitiza haya anaposema 'mwanamume anampiga mwanamke kwa kosa lisilostahimilika la kuwazaa watoto wa kike badala ya watoto wastahiki'. Katika dokezo hili mtunzi anaionya jamii dhidi ya kuwabagua watoto wa kike na kuwaona kama wasio na thamani. Anaishauri jamii kuwa watoto hawa wote ni sawa na ni wajibu wa jamii kuwapa nafasi sawa ya kujiendeleza kijamii na kiuchumi kwani jamii isipofanya hivyo maendeleo ya taifa hayawezi kuendelezwa na wanaume pekee bila kuwashirikisha wanawake na matokeo yake ni wanajamii kushindwa kujimudu kimaisha suala ambalo linaathiri mfumo wa ekolojia jamii.

Mwandishi pia anawakashifu wazazi wa kiume kwa kuwabeza na kuwalaumu wenzao wa kike kwa sababu ya kuzaa watoto wa kike. Mwanamume anajiondolea lawama na kumlaumu mwanamke. Vilevile jamii inamtweza mwanamke ambaye amejifungua mtoto wa kike. Mshairi anasema kuwa mzazi wa kike ananyoshewa kidole kila mahali anapokwenda kwa sababu ya kujifungua watoto wa kike. Haya yanajitokeza katika uk. 6 kifungu cha 1 anaposema 'anadharauliwa sokoni na kudhalilishwa nyumbani'. Kwa hivyo akidhalilishwa sokoni anashindwa kufanya biashara ili kuwatunza na kuwalisha watoto wake hali ambayo inaathiri ekolojia jamii. Anachosisitiza tunzi ni kwamba wanaume wasiwadharau wanawake kwa sababu ya kujifungua mtoto wa kike kwani hata wao wana wajibu mkubwa katika kuboresha mifumo ya ekolojia jamii. Anawaonya wanaume dhidi ya kuwabeza, kuwakemea na hata kuwapiga wanawake kwa sababu jamii haitapiga hatua kiuchumi na kijamii suala ambalo linaathiri mfumo wa ekolojia jamii. Kwa hivyo ni sharti jamii iwakumbatie watoto wao ikiwa ni wa kiume au wa kike kwani wote wana mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa.

Mwandishi anaikashifu jamii kwa sababu ya kumbagua mtoto wa kike kielimu hali inayoathiri mfumo wa ekolojia jamii kwani vijana wote, wa kike na wa kiume, wana mchango mkubwa katika kuendesha maendeleo ya taifa. Katika shairi 'Rangi ya Anga' sehemu ya 10 (Mberia, 2014) mwandishi anaonyesha kuwa baada ya vijana kujihusisha kimapenzi wakiwa bado shuleni vijana wa kike ndio wanaathirika kwa kuacha masomo. Katika uk. 13 kifungu cha 2 mtunzi anaonyesha haya anaposema, 'baada ya wawili kushiriki mapenzi mmoja anaendelea na masomo na kukusanya vyeti vya maana na kupata kazi nzuri.'

Anachosisitiza mtunzi katika dokezo hili ni kwamba huku mtoto wa kike akikosa kuendelea na masomo yake kwa sababu ya mimba, mwenzake wa kiume anaendelea na masomo na kupata vyeti ambavyo vinamsaidia kupata kazi na hivyo basi kuweza kujiendeleza kimaisha. Vijana wa kike wanaathirika kimasomo kwani hawapewi nafasi sawa ya kupata elimu kama wenzao wa kiume na matokeo yake ni kukosa mahitaji ya kimsingi kama vile: mavazi, chakula na makazi jambo ambalo linamshurutisha kujiingiza katika ukahaba ili aweze kujiinua kiuchumi hali ambayo inazorotesha maendeleo ya taifa.

Mshairi pia anazikashifu taasisi za elimu kwa sababu ya kuweka kanuni ambazo zinamwathiri mtoto wa kike pindi anapopata mimba kwani ndiye anafukuzwa shuleni na wa kiume anaendelea na masomo yake. Haya yanajitokeza katika uk. 14 kifungu cha 3 anaposema kuwa 'Halmashauri

ya Shule ilinukuu kanuni za Wizara na kuangusha shoka lenye makali,' ishara kuwa mtoto wa kike anafukuzwa shuleni kwa sababu ya mimba. Huu ni ubaguzi wa kijinsia ambao unaendelezwa katika jamii na kuathiri mfumo wa ekolojia jamii kwani wanajamii hawapewi nafasi sawa ya kujiendeleza kimaisha. Mtoto wa kike anabaki kumtegemea mwenzake wa kiume ili aweze kupata mahitaji ya kimsingi. Kwa hivyo jamii inapomtelekeza mtoto wa kike na kuacha masomo, anaishia mijini kule ambako anajihusisha na biashara ya ukahaba ili aweze kujikimu kimaisha. Mtunzi anaonyesha haya katika uk 14 kifungu cha 5 anaposema:

> Leo mijini
> Akibeba njaa kama saratani ya tumbo
> Na kuvaa umaskini kama joho la miiba
> Akitegea na kuchunguza magari yapitayo
> Na kulenga shabaha yanayochochea ndoto.

Katika kifungu hiki ni wazi kuwa mtunzi anaonyesha jinsi mfumo wa ekolojia jamii ulivyoathiriwa hivi kwamba wasichana wa shule wanajihusisha na ukahaba ili waweze kujikimu kimaisha. Hali hii inatokea ili waweze kuwalisha watoto wao. Haya yanajitokeza katika uk. 15 kifungu cha 4 anaposema kuwa 'ahimili maisha ya huzuni ya mama na kunusuru uhai wa mtoto asiyejua baba'. Kwa hivyo ni bayana kuwa msimulizi anakashifu jamii kwa sababu ya kumtenga mtoto wa kike. Anasisitiza kuwa mtoto wa kike na wa kiume wanastahili kupewa nafasi sawa ya kujiendeleza kimaisha la si hivyo inaathiri mfumo wa ekolojia jamii pale ambapo mtoto wa kike akikosa namna ya kujitegemea kiuchumi na kujihusisha na ukahaba anaathiri maendeleo ya taifa na kuporomosha maadili katika jamii. Isitoshe, katika karne hii ya ishirini na moja elimu imekuwa muhimu kwa sababu ya teknolojia ambayo binadamu anaendelea kuivumbua kila kuchao. Teknolojia hii inatumika katika kuzalisha vyakula viwandani na katika shughuli za kilimo cha kisasa. Kwa hivyo mtoto wa kike akinyimwa elimu jamii itakuwa na upungufu wa maarifa haya, hali itakayochangia upungufu wa uzalishaji wa bidhaa za kimsingi kama vile chakula na mavazi. Mtunzi anaishauri jamii kuwa impe mtoto wa kike nafasi sawa na yule wa kiume ili kusawazisha mfumo wa ekolojia jamii.

### 3.5 Ukeketaji wa Mtoto wa Kike

Kitendo cha jamii cha kumkeketa mtoto wa kike ni kitendo ambacho hakistahili kutumiwa kama kigezo cha kupima utu uzima. Hii ni kwa sababu jamii inapofanya hivi inamnyima heshima na hadhi yake. Chuma (2018, August 4) anaonyesha jinsi msichana wa miaka minane katika

sehemu ya Baringo alivyokeketwa na kisha kuozwa ili wazazi wake wapate mali. Katika shairi 'Rangi ya Anga' sehemu 3 (Mberia, 2014), mtunzi anaonyesha jinsi kitendo hiki kinavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii. Wasichana hawa wanakeketwa wakiwa wangali shuleni na hatima yao ni kuozwa mapema kwani kulingana na utamaduni, msichana akisha keketwa basi amehitimu umri wa kuozwa na wanaokataa wanatengwa na wazazi na jamii kwa jumla. Haya yanajitokeza katika uk 5 kifungu cha 1 mtunzi anaposema wazazi hawataki kuwa karibu na 'waasi' ikiwa na maana ya kwamba wanaokataa kukeketwa ili waozwe wanatengwa na familia zao.

Mwandishi anawakashifu baadhi ya wazazi ambao wanawakeketa watoto wao na baadaye wanawaoza ili wapate mali. Mtoto wa kike ambaye hajakeketwa anatengwa na jamii kwani anaonekana kama mtu ambaye hajakamilika na hawezi akaolewa. Mtunzi anadokeza haya katika uk. 5 kifungu cha 1 anaposema kuwa msichana ambaye amekataa kukeketwa jamii inamuona kuwa 'hadhi yake imeingia doa,' ishara ya kuwa hastahiki katika jamii. Kutengwa huku kunaathiri mfumo wa ekolojia jamii. Wanajamii wanastahili kuishi pamoja bila mivutano na migogoro kwani inakwamiza maendeleo ya taifa. Hakuna jamii inayoweza kupiga hatua mbele kukiwa na mivutano kwani kila mwanajamii ana nafasi na jukumu la kuchangia maendeleo katika nchi yake yatakayomfaidi pamoja na viumbe vingine. Wasichana pia wanapokeketwa huwa wanaathirika kiafya na hasa katika maisha ya kisasa ambapo kuna ugonjwa wa ukimwi. Wasichana hawa wakipatwa na ugonjwa wa ukimwi wanadhoofika kiafya kwani wengi wao hutoka katika familia ambazo hazijiwezi kiuchumi.Wanaishia kuwategemea jamaa zao ambao pia hawajiwezi kiuchumi. Hali hii inaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu jamii inapokosa nguvu kazi maendeleo ya taifa yanalemazwa.

Mtunzi kadhalika, anawakashifu wasanii ambao wanaimba nyimbo za kumdhalilisha msichana ambaye hajakeketwa. Anadokeza haya katika uk 6 kifungu cha 2 anaposema kuna wasanii ambao wamefungwa pingu za mila na wanatunga nyimbo sumbufu kama mpupu wakilalamika kuwa mtoto wa kike kukataa kukeketwa ni kwenda kinyume na utamaduni wa jamii. Katika dokezo hili mtunzi anakashifu utamaduni huu wa kukeketa mtoto wa kike kwani ni mila ambazo zimepitwa na wakati na zinaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwani wasichana hawa baada ya kukeketwa huwa wanaolewa na kuwa wazazi wakiwa wachanga na kushindwa kuwalisha na kuwavisha watoto wao. Matokeo yake ni watoto hawa kudhoofika kiafya na kukumbwa na magonjwa yanayosababishwa na ukosefu wa chakula cha kutosha na chenye madini

yanayosaidia miili. Pia wengi wao huishia kujifungua watoto wengi ambao ekolojia haiwezi kustahamili kwa sababu hawana maarifa kuhusu mbinu za upangaji wa uzazi. Isitoshe, huweza kukumbana na athari za kiafya wakati wa kukeketwa kwani wengine hufanyiwa vibaya. Vilevile hukumbwa na matatizo wakati wa kujifungua suala ambalo linaweza hata kusababisha kifo. Moore (2008) anasema kwamba wakati ambapo wanawake wanakandamizwa na utamaduni uliopitwa na wakati ekolojia na mazingira pia huathiriwa kwa sababu wanawake wana mchango mkubwa katika kuendeleza mfumo wa ekolojia na maendeleo ya jamii kwa jumla.

### 3.6 Teknolojia ya Kisasa

Ni wazi kuwa kutokana na mifumo ya teknolojia ya kisasa mifumo ya ekolojia jamii imeathirika. Vijana wanaiga mila na desturi za kigeni bila kufahamu madhara yake. Katika utungo *Rangi ya Anga* sehemu ya 8 (Mberia, 2014), mshairi anaonyesha jinsi vijana walivyoathiriwa na teknolojia ya kisasa. Anakashifu filamu ambazo zinaonyesha picha za ponografia kwa vijana. Anadokeza haya anaposema katika uk 11 kifungu cha 1 kuwa baada ya sinema za vita, shujaa wa kiume anajiganga machovu ya vita na mhusika wa kike huku vijana wakifurahia. Filamu hizi zinawapotosha vijana kimaadili wanapotazama vijana wenzao wakijihusisha kimapenzi hadharani. Ni bayana kuwa kupitia kwa filamu hizi vijana wanaiga utamaduni wa kigeni kwa mfano mapenzi ya jinsia moja, jambo ambalo linaathiri vijana kisaikolojia na kuwalemaza katika mahusiano yao ya kawaida na jinsia tofauti. Hali hii inaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu vijana wanapojihusisha katika mapenzi ya jinsia moja hawataweza kuwa na familia zao katika siku zijazo. Hivyo vizazi vya kesho ambavyo jamii inavitegemea katika kuendeleza maendeleo ya taifa vitaadimika. Kauli ambayo inaoana na mhimili wa Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia unaosema kuwa tabia na utamaduni wa jamii huchangia katika kuathiri maendeleo ya kijamii na kiuchumi kutokana na mifumo mipya ya kiteknolojia. Jamii inahimizwa iweze kujiepusha na utamaduni wa kigeni ambao unachangia kuporomoka kwa maadili na inahimizwa kuiga tabia ambazo zitaisaidia kujiendeleza kiuchumi. Vilevile vijana wanapotazama filamu hizi zinawachochea katika hali ya kujihusisha kimapenzi wangali bado wako shuleni na hatima yake ni vijana wa kike wanaoathirika kwani ndio wanaoacha masomo.

Hata hivyo mataifa ya Kiafrika yanayokumbatia mfumo wa kiteknolojia yanaimarisha mfumo wa ekolojia jamii. Haya yanajitokeza katika shairi *Bara Jingine* (Mberia, 2001) katika uk. 12 kifungu cha 2 anapodokeza kuwa ‘njia ya safari itamulikwa ikiwa cheche za sayansi

zitahimizwa,' ikiwa na maana kuwa maisha ya wanajamii yataboreshwa ikiwa watatilia maanani sayansi ya kisasa. Kupitia uvumbuzi huu wa teknolojia mpya jamii imeweza kugundua dawa za magonjwa kama vile malaria na ukambi. Anadokeza haya katika uk. 12 kifungu cha 2 anaposema kuwa kupitia teknolojia watagundua 'makombora dhidi ya malaria na ukambi' ishara kuwa watapata dawa ya kutibu magonjwa haya. Magojwa haya ni hatari kwani yanarudisha maisha ya jamii nyuma. Jamii ikidhoofika kiafya, nguvu kazi zinazotumika kuendeleza uchumi wa taifa zinafifia. Viumbe wengine ambao pia humtegemea binadamu wanaathirika.

Wakulima nao wakitumia teknolojia ya kisasa katika shughuli za kilimo wanaongeza idadi ya chakula wanachozalisha. Haya yanajitokeza katika diwani ya *Bara Jingine* (Mberia, 2001) katika shairi 'Bara Jingine' uk. 13 kifungu cha 2 anaposema 'wakulima wakitumia almasi ya bioteknolojia wataimba nyimbo za mavuno mazuri,' ishara kuwa watapata chakula tele. Ni wazi kuwa katika dokezi hili mwandishi anasisitiza matumizi ya bioteknolojia katika uzalishaji wa chakula. Mataifa yanayoendelea yakikumbatia mfumo huu yataepukana na suala la njaa ambalo huangamiza wananchi wake kwa kiwango kikubwa na yataweza kuimarisha mfumo wa ekolojia jamii

## 3.7 Hitimisho

Katika sura hii tumechunguza jinsi masuala ya kijamii yanavyoathiri mfumo wa ekoloji jamii na hatimaye matokeo yake kwa wanajamii. Kutokana na mashairi ambayo tumeyachunguza ni wazi kuwa utamaduni wa wanajamii una mchango mkubwa katika kuathiri mfumo wa ekolojia jamii. Hii ni kwa sababu kuna makundi mawili ya watu yaliyo na mitazamo tofauti kuhusu mila na tamaduni za jamii. Pia tumechunguza jinsi mifumo ya elimu, malezi, ndoa na teknolojia inavyoathiri mifumo ya ekolojia jamii Matokeo ya uchunguzi huu ni kuwa watoto wanaotelekezwa na wazazi wao huishia kukosa bidhaa za kimsingi kama vile chakula na malezi. Watoto ambao huathirika na hali hii ni wale wanalelewa katika familia ambazo hazina misingi thabiti. Pia mtoto wa kike anapobaguliwa na jamii kielimu usawa wa mfumo wa ekolojia jamii unaathiriwa. Takriban mashairi yote yanazungumzia kuhusu utamaduni, ulezi, elimu na teknolojia ya kisasa na jinsi zinavyoathiri mahusiano ya kijamii. Katika kuchunguza tungo hizi tumeongozwa na madhumuni ya utafiti wetu pamoja na mihimili ya Nadharia ya Uhalisia na ya Mfumo wa Ekolojia.

# SURA YA NNE

## ATHARI ZA MASUALA YA KIUCHUMI NA KISIASA KWENYE MFUMO WA EKOLOJIA JAMII

### 4.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia athari za masuala ya kiuchumi na kisiasa kwenye mfumo wa ekolojia jamii. Masuala haya tumeyaangazia kwa pamoja kwani yana uhusiano na mwingiliano wa karibu. Hii ni kwa sababu aghalabu viongozi wengi wa kisiasa ndio hutunga sheria ambazo huathiri mifumo ya kiuchumi na hatimaye kuathiri mifumo ya ekolojia jamii. Taifa ambalo lina mfumo wa kisiasa ulio imara mifumo yake ya kiuchumi huwa thabiti. Vilevile taifa linapokuwa na mfumo dhaifu wa kisiasa mifumo yake ya kiuchumi vilevile huwa dhaifu. Bronfenbrenner (1989) anasema kuwa mfumo wa ekolojia jamii huathiriwa na masuala ya kisiasa na kiuchumi. Kwa hivyo katika sura hii tumeshughulikia masuala kama vile: ukosefu wa kazi, ufisadi, hali ya umasikini na uongozi mbaya na kuonyesha jinsi yanavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii.

### 4.1 Ukosefu wa Kazi

Vijana wengi katika mataifa yanayoendelea wanakumbana na uhaba wa kazi. Wengi wanatoroka mashambani na kwenda mijini kusaka riziki. Lakini ukweli ni kwamba wanapokosa kazi kama walivyotarajia wanajiingiza katika biashara kama vile ukahaba. Katika diwani *Bara Jingine* Mberia (2001: 37) katika shairi ‘Mimi Monika’, katika kifungu cha 1 uk. 37 mtunzi anasema ‘kama nyuki ameanguka katika bakuli la maji’ ishara kuwa wasichana wanaingia mjini wakiwa na matumaini ya kupata kazi lakini kinyume na matarajio yao wanazikosa nafasi za kazi na kujiingiza katika biashara ya ukahaba ili waweze kujichumia riziki yao ya kila siku. Vijana hawa si eti wanaifurahia kazi hii lakini wanashurutishwa na hali ngumu ya maisha. Mtunzi anadokeza haya katika uk. 37 kifungu cha 2 anaposema, ‘kwa kipindi cha zaidi ya miaka kumi amekuwa akiuhudumia ulimwengu kwa tabasamu chungu’. Hata hivyo hana budi kwani hali ya maisha imekuwa ngumu. Mtunzi anawakilisha hali ya vijana wengi katika jamii na hasa wa kike ambao wanashurutishwa kujiingiza katika biashara ya ukahaba kutokana na ukosefu wa kazi na hawana namna nyingine yoyote ile ya kujiendeleza kimaisha. Wanakumbana na matatizo chungu nzima wakijaribu kujichumia mtaji wao.

Mwandishi anasema kuwa wanavumilia kugugunwa na baridi ya usiku na kulala nje wakati giza linapoingia mradi tu waweze kujipatia riziki (uk. 39 kifungu cha 1). Kazi hii inamdhalilisha na kumtweza mwanamke kwani ananyimwa heshima katika jamii na kuonekana kama kiumbe kisicho na maana. Mtunzi anadokeza haya katika uk. 37 kifungu cha 4 anaposema ‘kama mlango wa umma ameguswa na viganja milioni na kama jumba la mikutano ametembelewa na halaiki ya watu’. Kauli hii inaonyesha ametumiwa na watu wengi sana kimapenzi. Mtunzi anasema biashara hii hata huhatarisha maisha ya wahusika. Baadhi yao hata hukumbana na mauti kutoka kwa wateja wao ambao hukataa kuwalipa baada ya kuwahudumia. Wengine wanadhulumiwa na kuuawa na askari wa kigeni wanaokuja kwa meli na kutua bandarini. Mshairi anadokeza haya katika uk. 40 kifungu cha 14 anaposema kuwa marafiki ambao walikuwa wanasaidiana sasa wametulia ardhini wakiwa hawana matumaini kwa sababu ya askari wauaji wakishuka kisiwani ishara ya kwamba wameweza kuuawa.

Msimulizi anaendelea kuonyesha jinsi hali ya uchumi ilivyo ngumu hivi kwamba vijana wanaotoka mashambani na kwenda jijini kujichumia riziki wanakosa riziki. Hii ndio moja wapo ya sababu yao kujihusisha na biashara hii ya ukahaba. Mtunzi anadokeza haya katika uk. 38 kifungu 8 anaposema kwamba ‘wakiwa mjini walichokora mapipa ya taka na kupigania kama majibwa mabaki ya chakula’. Kauli hii inaonyesha wazi kuwa vijana hawa wanateseka kwa sababu hawawezi kujikimu kiuchumi. Hawawezi kujilisha kwani wanang’ang’ania chakula ambacho kimetupwa kwenye mapipa ya takataka. Ni suala la kusikitisha kuona kuwa hata baada ya taifa kujinyakulia uhuru haliwezi kuwashibisha raia wake linawaacha watafute chakula katika mapipa ya taka. Suala hili linaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu taifa lazima liweze kuwalisha wananchi wake ili wapate nguvu kazi za kuendeleza taifa mbele kiuchumi. Pia wanyama ambao wanawategemea binadamu kuwalisha wanaathirika na taifa linarudi nyuma kimaendeleo.

Mtunzi anaendelea kuonyesha jinsi wasichana hawa wanavyotembea mjini usiku wakiwa nusu uchi ili kuweza kuwavutia wateja wao. Anadokeza haya katika uk. 39 kifungu cha 10 anaposema wanatembea ‘tambarare kifuani,’ ishara kuwa wanatembea huku vifua vikiwa wazi. Baadhi ya wasichana hawa huwa na umri mdogo lakini wanalazimishwa na hali ngumu za kimaisha kushiriki kimapenzi na wazee wanaowazidi kiumri. Haya yanajitokeza katika uk. 39 kifungu cha 9 anaposema ‘alianza utotoni aliposikia sauti yenye upara ikimuita’. Hali hii inaonyesha jinsi hali

ngumu ya kiuchumi inavyoathiri mifumo ya kijamii hivi kwamba wazee ambao wanaheshimika katika jamii wanashiriki mapenzi na wasichana wadogo kinyume na matarajio ya kijamii. Baadhi ya wasichana hawa huambukizwa maradhi kama vile UKIMWI suala ambalo huathiri afya zao. Baadaye wanashindwa hata kufanya kazi yoyote ya kujikimu kimaisha na wanaishia kuwategemea jamaa zao ambao pia hawajiwezi kiuchumi. Kwa hivyo ni wajibu wa serikali kuweza kubuni nafasi za kazi kwa vijana ili waweze kujiinua kiuchumi na kujitegemea kimaisha. Pia vijana wanapopata kazi inasaidia kupunguza hali ya uhalifu nchini na biashara haramu kama vile ya ukahaba. Hii ni kwa sababu mambo haya yanaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa kuathiri mahusiano baina ya wanajamii. Kutokana na hali hii hakuna wawekezaji ambao wanaweza kuekeza katika nchi ambayo haina usalama. Matokeo yake ni taifa kukosa malighafi na uwezo wa kugharamia mahitaji yake ya kimsingi kama vile chakula, makazi, mavazi na huduma za afya suala ambalo linaathiri binadamu na viumbe vingine.

Kulingana na Nadharia ya Uhalisia mtunzi huwasilisha masuala ambayo yanatendeka katika jamii anamoishi. Kwa mfano Kamau (2018, August 3), anaonyesha jinsi wasichana wa mji wa Thika nchini Kenya wanavyojihusisha na ukahaba ili wapate mahitaji yao ya kimsingi. Anasema kwamba wasichana hawa hata ‘huwakopesha’ wateja wao ambao huwalipa mwisho wa mwezi. Hali hii inaonyesha jinsi ukosefu wa kazi unavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii hivi kwamba binadamu anashiriki biashara haramu na ya kushusha hadhi mradi apate chakula, makazi na mavazi. Isitoshe, wengi wa wasichana hawa huambukizwa magonjwa kama vile UKIMWI na kudhoofika kiafya na kukosa nguvu kazi za kuzalisha rasilimali zinazomsaidia binadamu na viumbe vingine.

Katika diwani Bara Jingine (Mberia, 2001) katika shairi ‘Wanabiashara Barabarani’, mwandishi anaishauri jamii isiwe na mtazamo hasi dhidi ya wasichana wanaofanya biashara ya ukahaba mijini kwani baadhi yao wanashurutishwa na hali ngumu za maisha. Haya yanajitokeza katika uk. 43 kifungu cha 1 anaposema ‘wahubiri wasiwatusi wale ambao wamesimama pembeni mwa barabara macho yao yakitangaza nia imara’. Ikiwa na maana kuwa wasiwadhalilishe wanaofanya kazi ya ukahaba. Hii ni kwa sababu hawana njia nyingine ya kujichumia pato ila kushiriki katika biashara hii kwa sababu ya ukosefu wa kazi na wanahitaji kutimiza mahitaji yao ya kila siku. Mshairi anaishauri jamii isiwatusi na kuwabeza bali wanastahili kuelekezwa na kusaidiwa kupata njia nyingine mbadala za kujichumia riziki ili waweze kuboresha mfumo wa ekolojia jamii.

Msimulizi anawakashifu wahubiri ambao wanawakashifu wasichana wanaojihusisha na ukahaba badala ya kuwaongoza kimaadili na kuwasaidia kupata kazi nyingine mbadala. Haya yanajitokeza katika uk.43 kifungu cha I anaposema kuwa mhubiri ahubiri bila kuwatusi wale ambao wako katika barabara za miji. Anachosisitiza mtunzi katika kauli hii ni kuwa wanaofanya biashara hii ni binadamu kama watu wengine ila hali ngumu za kimaisha zinawasukuma katika kufanya kazi hii mradi waweze kupata chakula na mavazi. Mtunzi anaendelea kusema kuwa wanaofanya kazi ya ukahaba si kwamba wanaifurahia kazi hii kama wale wanafanya kazi ofisini wala si eti wana akili pungufu ila ni ukosefu wa kazi unaowafanya kujiingiza katika ukahaba. Anadokeza hili katika uk. 43 kifungu cha 1 anaposema kuwa 'hawana moto au akili pungufu kuliko wanaofanya kazi ofisini'. Hapa mtunzi anaonyesha tofauti za kiuchumi kati ya matajiri na masikini katika jamii. Watu ambao ni matajiri wanafanya kazi zenye hadhi ya juu ilhali masikini wanafanya kazi ambazo zinawadhalilisha na za kuwabeza kama vile za ukahaba. Hali hii inaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu mahusiano haya kati ya matajiri na masikini huwa yanakumbwa na migogoro na mivutano. Kwa mfano, hali ya usalama inazorota kwani wanajamii ambao hawajiwezi kiuchumi wanawahangaisha mabwanyenye kwa kuwaibia mali zao hali inayoleta mikwaruzano katika jamii. Ili kuzuia hali hii ni sharti taifa ligawe rasilimali zake kwa njia ya uwazi ili kuhakikisha kuwa kila mwanajamii anapata haki yake na anaweza kujilisha na kujivisha badala ya kutumia njia haramu kama ukahaba ili kujichumia riziki.

Isitoshe mshairi anaikashifu jamii kwa sababu ya kuwatelekeza wanajamii wake na kukataa kuwapa mwelekeo katika maisha na ndiposa wanajiingiza katika kazi za aibu kama za ukahaba. Mwandishi anadokeza haya katika uk.43 kifungu cha 1 anaposema kuwa 'wanaoshiriki ukahaba ni wale ambao wameangushwa njiani na mwendo wa jamii' ishara ya kuwa jamii imewatelekeza na haijali mustakabali wao. Kulingana na dokezo hili ni vyema jamii iwaelekeze hasa vijana umuhimu wa kuwa na maadili mema na kuwaongoza katika kuangazia njia nyingine za kujichumia riziki ili waweze kuepuka kujiingiza katika biashara hizi haramu. .

### 4.2 Ufisadi

Ufisadi ni suala ambalo linaathiri mfumo wa ekolojia jamii. Hii ni kwa sababu mali ya umma ikinyakuliwa kama vile ardhi, wanajamii wanakosa sehemu za kukuza chakula na kujenga makazi. Wanajamii pamoja na wanyama wanaathirika kwa sababu wanakosa chakula na makazi. Matokeo yake ni viumbe hivi kuangamia na hivyo basi kuathiri ekolojia jamii. Katika diwani

*Bara Jingine* (Mberia, 2001) katika shairi 'Wanabiashara Barabarani', mwandishi anawakashifu watu ambao wanatumia njia za mkato kuweza kujitajirisha. Anasisitiza haya katika uk. 44 kifungu cha 2 anaposema 'ni matarajio hatari kusafiria njia ya mkato' ikiwa na maana wanatumia njia za ufisadi kujichumia mali bila kuwajali watu. Wafisadi hawa ndio wanaathiri mifumo ya ekolojia jamii pale ambapo pana matajiri wachache na masikini wengi katika taifa.

Mtunzi anawakashifu wale ambao walizembea chuoni ndio wako mstari wa mbele kupora mali ya umma kwa kutumia njia za mikato na kuishia kuwa matajiri. Haya yanajitokeza katika uk. 44 kifungu cha 2 anaposema kuwa 'walioepuka jasho darasani na maktabani' ndio wako na mali waliyoyapata kupitia njia ya ufisadi. Hali hii inazima ndoto na kuwatamausha vijana ambao wanakazana na masomo shuleni. Kwa sababu baada ya kutia bidii masomoni, matokeo yake ni hali ngumu za maisha hivi kwamba wanakosa namna za kujitegemea. Hali hii inaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu vijana ambao ni tegemeo la kuendeleza uchumi wa taifa katika siku zijazo wanatamauka na kuanza kujihusisha na njia za mkato kujipatia riziki kama wenzao waliowatangulia. Uchumi wa taifa unalemazwa kwa sababu vijana wana mchango mkubwa katika kuzalisha rasilimali za taifa. Kwa mfano vijana wanapoenda shuleni wanapata maarifa ya kuzalisha chakula wakitumia teknolojia ya kisasa hali ambayo itanufaisha jamii kwa jumla.

Mtunzi anakashifu unafiki wa viongozi wa kidini kwa sababu hawaoni maovu ambayo yanafanywa na viongozi wafisadi ambao wanaporomosha mifumo ya kiuchumi bali wanawasuta na kuwatusi vijana ambao wanajihusisha na biashara ya ukahaba bila kufahamu kuwa wanaofanya biashara hii ni kutokana na hali ngumu ya maisha kwani rasilimali za taifa zimeporwa. Mtunzi anadokeza haya katika uk.43 kifungu cha 2 anaposema kuwa baadhi yao wamekata tamaa 'wakijaribu kutafuta mti wa kukamata' ikiwa na maana kuwa wanajaribu kutafuta njia za kujichumia riziki lakini rasilimali nyingi zimo mikononi mwa wachache waliozipata kwa nja ya ufisadi.

### 4.3 Hali ya Umasikini

Umasikini ni suala ambalo linaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu binadamu anapokosa fedha za kujichumia mahitaji ya kimsingi kama vile chakula na mavazi anaishia kuathirika kiafya na kukosa nguvu za kusaidia viumbe vingine vinavyomtegemea. Katika diwani *Bara Jingine* (Mberia, 2001) katika shairi 'Hatutaaga Ndoto,' mwandishi anaonyesha jinsi hali ngumu

za kiuchumi zinavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii. Anaonyesha jinsi hali ya umasikini imekumba jamii hivi kwamba hata watoto wanaangamizwa na magonjwa kama vile ukambi na kifaduro. Mberia anadokeza haya katika uk. 5 kifungu cha pili anaposema kuwa ‘watoto wanatembea vijijini wakitafunwa njiani na ukambi au kifaduro’. Watoto hawa wanakumbana na maradhi haya kwa sababu wazazi wao hawajiwezi kiuchumi kuwapa watoto wao lishe bora. Hali hii inaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu watoto ni kiungo muhimu katika kuendeleza kizazi katika jamii. Wengi wa watoto hawa wanaangamia kutokana na magonjwa ambayo yangezuilika ikiwa wazazi wao wangekuwa na uwezo wa kuwapa chakula chenye madini yanayosaidia mwili.

Kutokana na uchochole ambao umeikumba jamii, wazazi pia wanashindwa kuwapa watoto wao elimu ndiposa mtunzi katika uk. 4 kifungu cha 1 anasema kuwa ‘sumu ya kutojua imefunika kijiji’ ishara kuwa wanakijiji hawajaelimika. Suala hili la wanajamii kutopata elimu linaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu linachangia katika kudidimiza maendeleo ya taifa kwa sababu elimu ni nguzo muhimu katika kuendesha taifa lolote lile kiuchumi na hasa katika kipindi hiki cha utandawazi kwani wanajamii wanahitaji maarifa ya kuzalisha bidhaa za kimsingi zinazotumiwa na binadamu na viumbe wengine wanaomzingira.

Mtunzi pia analalamikia kuzorota kwa uchumi kunakosababishwa na ongezeko la matumizi mabaya ya mali ya umma. Anadokeza haya katika uk. 4 kifungu cha 1 anaposema kuwa ‘kichaa cha ufisadi kimesambaa mithili ya viini vya kichocho’. Anachosisitiza mtunzi katika dokezo hili ni kuwa matumizi mabaya ya mali ya umma yamekita mizizi na hasa katika mataifa yanayoendelea suala ambalo linakwamiza maendeleo ya taifa kiuchumi. Hii ndiyo sababu suala la utabaka linajidhihirisha katika jamii. Ni wazi kuwa katika jamii kuna matajiri wachache na masikini wengi. Walio masikini aghalabu wanajihusisha na uhalifu ili waweze kujikimu kimaisha. Kiasi kikubwa cha masikini hawa huwa ni vijana ambao hawana kazi. Wanapojihusisha na uhalifu wa kuwaibia matajiri, wao huishia gerezani au makaburini. Hali hii inaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu vijana hawa ndio wanaotegemewa na jamii katika kuendesha shughuli za taifa katika siku zijazo.

Mtunzi pia anawakashifu wafanyi biashara wa kigeni ambao wanakuja kufanya biashara katika mataifa yanayoendelea kwa sababu ya kuwadhulumu kiuchumi. Haya yanajitokeza katika uk 4 kifungu cha 1 anaposema ‘Brettons Woods na wenza wanatunyonya damu mithili kupe milioni’

ikiwa na maana kuwa  wafanyi biashara hawa wanawanunulia wenyeji bidhaa zao kwa bei ya chini kisha kwenda kuuza kwa bei ya juu katika mataifa yao na kuwaacha wenyeji katika umasikini hali ambayo inaathiri mifumo ya kiuchumi katika mataifa yanayoendelea. Mataifa haya yanaachwa yakiwa ombaomba kwa sababu rasilimali yanazozalisha haziwezi kuwasaidia kujikimu kimaisha.

Mwandishi pia anawakashifu viongozi ambao wanajitajirisha kutokana na kupora mali ya umma. Wanawanyanyasa na kuwadhulumu wanajamii hali ambayo inakwamiza maendeleo ya taifa na matokeo yake ni kuwafanya wenyeji wawe kama watumwa katika nchi yao. Mtunzi anadokeza haya katika uk. 4 kifungu cha 1 anaposema kuwa 'mazimwi wajeuri wametuzungusha seng'enge kama motokaa ya vita'. Kutokana na kauli hii ni wazi kuwa viongozi ambao jamii inawapa nafasi ya kulinda mali yao ndio wako mstari wa mbele kuyapora na kuyamaliza. Wanapofanya hivi wanaharibia vizazi vya kesho mtaji kwa sababu ya tamaa na ubinafsi wao. Ubinafsi huu unaathiri mfumo wa kiekolojia hivi kwamba vizazi vya kesho vinataabika kwa sababu ya kukosa mahitaji muhimu kama vile chakula na makazi kwa sababu waliotangulia waliyafyonza mali yote.

Hata hivyo mtunzi anaipa jamii matumaini kwa kusema kuwa kuna siku inayokuja ambapo watoto hawataathiriwa na magonjwa kwani jamii itakuwa imepiga hatua ya kiteknolojia katika sekta ya matibabu. Pia anasema kuwa kutokana na teknolojia mpya waafrika wataweza kuboresha kilimo wakitumia teknolojia ya kisasa hali ambayo itawainua kiuchumi na kuwaondolea fedheha ya kuombaomba katika mataifa yaliyoendelea. Anadokeza haya (katika uk.5) anaposema kuwa 'teknolojia ya kilimo itabusu mashamba yazae kiazi kikuu kuliko Afrika' ikiwa na maana kuwa kupitia kwa teknolojia Afrika itazalisha chakula kingi na kuepuka adha ya njaa suala ambalo litaboresha mfumo wa ekolojia jamii. Kwa hivyo ni wazi kuwa kutokana na kifungu hiki mataifa ya nchi zinazoendelea zikikumbatia mifumo mipya ya kiteknolojia yataweza kupata chakula cha kutosha hali ambayo itaimarisha afya nzuri kwa wakazi wake na kuboresha mfumo wa ekolojia jamii. Biko (2018, June 18) anasema kuwa mataifa mengi ya Kiafrika na hasa Kenya yanakumbwa na janga la njaa kwa sababu ya kutotumia teknolojia ya kisasa katika kilimo biashara. Anasema kuwa mojawapo ya changamoto kubwa inayowakumba wakulima wadogowadogo ni ukosefu wa vifaa vya kisasa vinavyowasaidia kuzalisha chakula kingi na kuboresha hali ya maisha. Anawahimiza wakulima watumie hata simu za mikono ili

kupata habari kwenye mitandao kuhusu mbinu mpya za kilimo, soko la bidhaa zao, na utaratibu wa matumizi ya pesa baada ya kuuza mazao yao. Wakifanya hivi wataweza kuboresha mfumo wa ekolojia kwani binadamu na wanyama wengine watapata chakula cha kutosha.

Katika shairi *Rangi ya Anga* sehemu ya 16 (Mberia, 2014), mtunzi anaonyesha jinsi wasichana wa shule wanavyolazimika kuacha masomo hasa wakati wa hedhi kwa sababu hawawezi kumudu kununua visodo kutokana na hali ngumu ya kiuchumi. Haya yanajitokeza katika uk. 25 kifungu cha 6 anaposema kuwa 'kila wakati wa hedhi anaifanya nyumbani ngome' ikiwa na maana kuwa wakati wa hedhi hahudhurii masomo shuleni. Hii ni kutokana na umasikini uliokithiri mipaka katika jamii wanamotoka hivi kwamba hawawezi kumudu hela za kununua visodo. Wanafunzi hawa wakikosa kwenda shuleni wanaishia kujihusisha na uhalifu kama vile wizi, ukahaba na matumizi ya dawa za kulevya suala ambalo linaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwani wanasababisha migogoro na migongano katika jamii.

Ukosefu wa visodo pia unasababisha wanafunzi hawa kutomakinika darasani wakati wa masomo kwa sababu ya kuona aibu mbele ya wanafunzi wenzao. Mtunzi anasisitiza haya katika uk. 24 kifungu cha 2 anaposema kuwa 'baada ya kuulizwa swali na mwalimu alisimama kwa ujasiri na kugundua wanafunzi wengine wakimcheka kisa na maana sare ya shule ilikuwa na baka loevu.' Katika dokezo hili Mberia anaonyesha jinsi wanafunzi hawa wa kike wanavyotaabika na kudhihakiwa na wenzao pindi wanaposhuhudia hedhi kwani hawana visodo vya kujisteri. Ni suala la kukatisha tamaa kuona kuwa wanajamii wengi hawawezi kumudu visodo kwa watoto wao wa kike kwa sababu ya umasikini. Wanafunzi hawa wanakaa nyumbani bila kuhudhuria masomo kwa sababu ya aibu waliokumbana nayo shuleni. Mtunzi anadokeza haya katika uk 25 anaposema:

> Kwa siku mbili zilizofuatana
> Msichana aliyechomwa na aibu
> Mwana wa wazazi wasiojiweza
> Aliogelea katika majonzi nyumbani
> Wazo la kuonana tena na wenza shuleni
> Likawa latisha kama jinamizi.

Kutokana na kifungu hiki ni wazi kuwa wanafunzi wengi wa kike na hasa katika mataifa yanayoendelea wanaacha masomo kwa sababu ya umasikini hivi kwamba hawawezi wakamudu visodo. Jambo hili linaathiri mfumo ekolojia jamii kwani baadhi yao huishia kuolewa wakiwa

bado na umri mdogo. Mtunzi anaishauri jamii ihakikishe kuwa mtoto wa kike haachi masomo kwa sababu ya hedhi. Hii ni kwa sababu mwanafunzi huyu ana mchango mkubwa katika kuendeleza maendeleo ya taifa kwa mfano kuzalisha chakula viwandani na mashambani akitumia maarifa ya teknolojia ya kisasa ambayo yanahitaji elimu. Kwa hivyo ni jukumu la serikali kuona kwamba wanafunzi hawa wanabaki shuleni na kuendelea na masomo kama wenzao wa kiume na kupata nafasi sawa katika jamii. Hii ndio sababu Wizara ya Vijana na Jinsia nchi Kenya imeeanzisha mradi wa kuwapa wasichana wa shule visodo ili kuhakikisha kuwa wanaendelea na masomo. (Nyaundi, 2017).

## 4.4 Uongozi Mbaya

Katika utungo *Bara Jingine* (Mberia, 2001) mtunzi anawapa waafrika matumaini ya kupata bara jipya ambalo limeendelea kiuchumi. Anadokeza haya katika uk. 10 kifungu cha 1 anaposema 'ndoto yake ni tamu kama asali kuhusu bara jipya' ishara kuwa ana matumaini kuwa bara la Afrika litabadilika kiuchumi na kisiasa katika siku zijazo. Hata hivyo anawalaumu wanasiasa kwa sababu ya kulemaza maendeleo ya taifa. Anawashutumu viongozi kama vile wabunge kwa sababu baada ya wao kupewa nafasi ya kuwawakilisha wananchi waliowachagua wanatumia nafasi hiyo kujitajirisha bila kujali maslahi ya waliowachagua. Mtunzi anawarejelea wabunge hawa 'kama genge la nzige' (uk. 10 kifungu cha 1), ishara ya kwamba wanavamia mali ya umma na kufilisi hazina ya kitaifa. Wanaoumia katika mchakato huu ni wananchi ambao waliwachagua wakiwa na matumaini kuwa watawaletea rasilimali za kitaifa. Lakini kinaya ni kwamba viongozi hawa wanatumia vyeo hivi na mamlaka walionayo kupora mali ya umma. Matokeo yake ni kuathiri maisha ya baadaye ya jamii na viumbe vingine vinayotegemea rasilimali hizi suala linaloathiri mfumo wa ekolojia jamii.

Mshairi pia anawalaumu wanasiasa hawa kwa sababu badala ya askari wa taifa kuwalinda wananchi wa kawaida wanawalinda viongozi hawa wakiwa ikuluni. Haya yanajitokeza katika uk. 10 kifungu cha 1 anaposema kuwa 'usalama wa taifa unalinda mamba wa ikulu' ikiwa na maana kuwa viongozi dhalimu walio serikalini ndio wanalindwa na askari huku wananchi wakiachwa bila usalama hali ambayo inahatarisha maisha yao ilhali ni wajibu wa serikali kulinda maisha ya wananchi wake. Ukosefu huu wa usalama unaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu wananchi hawawezi kufanya kazi katika mandhari ambayo si salama. Matokeo yake ni kuwaacha wananchi wakiangamia kutokana na ukosefu wa vyakula, mavazi na makazi.

Wananchi wengi pia wanapoteza maisha yao kutokana na magenge ambayo yanajihusisha na uhalifu. Wanajamii wakiangamizwa na vikundi hivi haramu nchi inakosa nguvu kazi za kuendeleza taifa mbele kiuchumi. Wananchi wengi ambao wanajaribu kupinga uongozi huu wanaishia kwenye jela kwa makosa ambayo hawajatenda. Anadokeza haya katika uk. 10 kifungu cha 1 anaposema kuwa Vizuizi na jela zinakuwa vinu'.

Suala la ubadhirifu wa mali ya umma linaathiri maisha ya kijamii. Mtunzi anasema kuwa viongozi hawa ambao wamepewa majukumu ya kulinda mali ya umma wanayageuza na kuyafanya mali yao ya kibinafsi. Mberia anadokeza haya katika uk. 11 kifungu cha 1 anaposema kuwa 'ufisadi unanyesha kutoka juu kama sumu' ishara ya jinsi viongozi hawa wanafuja mali ya umma. Wananchi ambao wanatumia nguvu nyingi katika kuzalisha mali, wanaishia kuwa masikini ombaomba kwa sababu hawapati faida zozote katika rasilimali wanazozalisha. Ukabila ambao pia husababishwa na wanasiasa huathiri mfumo wa ekolojia jamii. Hii ni kwa sababu wanasiasa wanawabagua wananchi kwa misingi ya kikabila hasa katika misimu ya uchaguzi hali inayo sababisha chuki miongoni mwa wanajamii na kuathiri maendeleo ya taifa. Haya yanajitokeza katika uk. 11 kifungu cha 1 mtunzi anaposema kuwa 'ukabila unakuwa kama ukungu unaoshambulia macho'. Wanasiasa hawa wanafanya hivi kwa sababu ya manufaa yao wenyewe lakini hawajali maisha ya baadaye ya wananchi waliowachagua. Ni wazi kuwa ukabila huu unaathiri hali ya mahusiano miongoni mwa wanajamii na hivyo basi kukwamiza juhudi za kuzalisha rasilimali zinazotumiwa na binadamu na wanyama kwa jumla.

Wanasiasa wanapowabagua wanajamii kwa misingi ya kikabila aghalabu huweza kutokea vita vya kikabila kama vilivyotokea mwaka wa 2007 nchini Kenya na madhara yake ni mengi kwani wakati jamii zinapopigana taifa haliwezi kuendelea mbele kiuchumi kwani hakuna wawekezaji wa kigeni wanaoweza kuekeza katika nchi ambayo inakumbwa na vita. Vilevile wanajamii wakiuana taifa linakosa watu wa kufanya kazi suala ambalo linazorotesha mfumo wa ekolojia jamii kwani wanajamii hawa ndio wanazalisha mali na kutunza viumbe vingine. Suala la kusikitisha ni kwamba wanasiasa hawa mara nyingi wanawatumia vijana ambao hawana kazi kuzusha ghasia kwa malipo duni. Hali hii hutokea hasa wakati wa uchaguzi pale ambapo wanasiasa wanawatumia vijana kuleta fujo wakiwa na nia ya kuwatisha na kuwatia uoga wapizani wao. Ni wazi kuwa vijana wengi huangamia katika vita hivi na jamii inakosa wafanyakazi wa kuendeleza shughuli za kijamii na kiuchumi kama vile uzalishaji wa chakula na

bidhaa za kimsingi katika viwanda. Kwa hivyo kutokana na utungo huu ni wazi kuwa viongozi wa kisiasa wana mchango mkubwa katika kufaulisha mfumo wa ekolojia kwani ndio huwa wamepewa majukumu ya kutunga sheria na kugawa rasilimali za nchi ili kukidhi mahitaji ya wanajamii kama vile elimu, barabara, huduma za afya, makazi na vyakula.

Mtunzi anawakashifu viongozi ambao baada ya kuchaguliwa na wananchi kazi yao ni kukaa kwenye maofisi na kufyonza mali ya umma. Mtunzi anawarejelea kama 'swila waliofura shingo' uk. 11 kifungu cha 2. Hali hii inawatamausha wananchi na wanakuwa na mtazamo hasi na kuathiri mahusiano kati ya watawala na watawaliwa. Viongozi hawa wanapora mali ya umma iliyotengewa maendeleo ya nchi kama vile ujenzi wa barabara, ununuzi wa pembejeo, huduma za afya na kuishia kuzitumia fedha hizi katika misimu ya kampeni. Hali hii inaathiri ekolojia jamii kwa sababu wakulima wakikosa pembejeo watakosa kujihusisha na shughuli za kilimo na taifa halitapata chakula cha kutosha. Isitoshe, barabara zikiwa bovu wakulima hawataweza kusafirisha bidhaa zao sokoni. Pia mwandishi anawalaumu viongozi hawa kwa kulindwa na idadi kubwa ya askari na kuwaacha wananchi wengine bila usalama wa kutosha. Anawarejelea askari hawa kama 'bakora ya kudumishia miungu-wa- kinamo' ikiwa na maana ndio wanawalinda ikuluni. Wanasiasa hawa pia wanawagawanya wananchi kwa misingi ya kikabila na matokeo yake ni chuki na vita, hali ambayo inaathiri mahusiano baina ya wanajamii na hivyo basi kuathiri mfumo wa ekolojia jamii.

Katika diwani *Bara Jingine* utungo 'Obasanjo' (Mberia 2001) mwandishi anamsifu aliyekuwa raisi wa Nigeria Obasanjo kwa sababu ya kujiuzulu mamlakani kwa hiari yake tofauti na viongozi wengine wa bara Afrika. Anadokeza haya katika uk. 17 kifungu cha 2 anaposema kuwa kitendo cha Obasanjo kujiuzulu mamlakani kilikuwa na 'ladha kama matone ya asali' ikiwa na maana kuwa kilikuwa kitendo kilichoenziwa na kufurahisha wengi. Hii ni kwa sababu viongozi wengi wa kiafrika hukatalia mamlakani hata baada ya kipindi chao cha kuhudumu kukamilika. Haya yanajitokeza katika uk. 17 kifungu cha 5 anaposema kuwa katika bara Afrika 'kuna wapandao vitini na hawashuki. Wengine hata hubadilisha katiba mradi kipindi chao cha kusalia mamlakani kiongezwe. Kauli hii inaoana na mhimili wa Nadharia ya Uhalisia unaodai kuwa mtunzi huwasilisha mambo yanayoonekana katika jamii anayoishi. Kwa mfano, rais wa Rwanda Paul Kagame alishinikiza kubadilishwa kwa katiba ili kuongeza kipindi chake cha kuhudumu kama rais. Clement (2015, December, 17). Anasema huenda Kagame akawa rais wa Rwanda

hadi mwaka wa 2034. Hii ni ishara ya tamaa na ubinafsi ambao umewakumba viongozi hasa wa kiafrika. Wanaposhurutishwa washuke mamlakani wanatumia bunduki na vyombo vya dola. Mtunzi anasisitiza haya katika uk 17 kifungu cha 3 anaposema kuwa Obasanjo alikuwa na bunduki iliyojaa mauti ya kufyatua Izraeli lakini hakufanya hivyo kama jinsi viongozi wengine wa kiafrika hufanya.

Rais wa Uganda Yoweri Museveni amekatilia mamlakani na hata kubadilisha sheria ili kuongeza kipindi chake cha kuhudumu kama rais. Kulingana na Gazeti la *The Standard* (Khafafa 2018, August 28) uongozi wa Museveni ulimdhulumu na kumnyanyasa mbunge wa eneo bunge la Kyadondo Mashariki almaarufu Bobi Wine kwa kumtia kizimbani na kumfungulia mashtaka ya kosa la jinai kwa sababu ya kukosoa utawala wake. Hali hii inaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu vijana ambao wana nguvu na maarifa ya kisasa ya kuzalisha mali na kuendeleza nchi kiuchumi na kisiasa wananyimwa nafasi. Matokeo yake ni jamii kukosa mahitaji ya kimsingi kama vile huduma za afya na chakula. Viongozi hawa wanasababisha vita katika taifa na mara nyingi huathiri maendeleo ya taifa kwa sababu hakuna wawekezaji wa kigeni wanaoweza kuwekeza rasilimali zao katika taifa ambalo linakumbwa na misukosuko ya kivita. Matokeo ya hali hii ni taifa kubaki nyuma kiuchumi. Hii ni kwa sababu wawekezaji hawa husaidia katika kuimarisha mbinu za kilimo, teknolojia ya kisasa na uzalishaji wa mali kupitia kwa viwanda ambavyo vinabuni nafasi za kazi kwa vijana. Lakini wakisusia kuwekeza kwa sababu ya vita vya wenyeji basi mfumo wa ekolojia jamii unaathirika kwa sababu wananchi wa taifa husika hawatapata chakula cha kutosha na hata bidhaa za kimsingi zinazozalishwa katika viwanda zinakuwa nadra.

Isitoshe, nchi ikiwa haina uthabiti wa kisiasa bei ya vyakula na gharama za maisha hupanda kwani sehemu zingine hazifikiki kwa sababu ya uhasama wa kisiasa. Kwa mfano katika uchaguzi wa 2017 nchini Kenya bei za bidhaa za kimsingi kama vile unga zilipanda katika maeneo ya Kisumu kwa sababu wanabiashara hawangefika maeneo hayo kwa sababu ya kuhofia maisha yao. Matokeo yake ni kwamba wakazi walikosa chakula cha kutosha na huduma zingine za kiafya suala linalowaathiri pamoja na viumbe wanaowazingira.

Wanasiasa pia wanapowachochea wanajamii kupigana mradi wasalie mamlakani wananchi wanateseka kwa sababu ya kukosa huduma za kimsingi kama vile matibabu na elimu. Mwandishi anaonyesha haya katika uk 18 kifungu cha 6 anaposema kuwa viongozi wa kiafrika

hawashuki mamlakani isipokuwa ‘cheche za fataki zilipuliwe na askari chini ya makalio yao’. Hali hii inatokea katika hali halisi barani Afrika. Kwa mfano mwaka wa 2018 aliyekuwa rais wa Zimbabwe aling’atuliwa mamlakani na jeshi la nchi hiyo baada ya kuhudumu kama rais kwa takribani miaka thelathini na minane.

Katika mchakato huu wa vita vya wenyewe kwa wenyewe, wanaoathirika sana ni watoto na wanawake kama ilivyoshuhudiwa katika taifa la Sudan Kusini wakati aliyekuwa naibu wa rais wa nchi hii Riek Machar alipojaribu kupindua uongozi wa rais Kiir. Wakati wa vita hivi, watoto wengi hukumbwa na maradhi kama vile utapia mlo, ukambi na kipindupindu. Magonjwa haya yote yanasababishwa na ukosefu wa chakula chenye madini, ukosefu wa maji safi na hali duni ya makazi. Hali hii inaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu watoto hawa ndio tegemeo la taifa katika siku zijazo. Iwapo taifa halitalinda watoto wake linaathirika kiuchumi.

Wanawake pia huathirika kwa kiasi kikubwa katika vita hivi, kwani baadhi yao hubakwa, kuuawa na hata kuambukizwa magonjwa kama vile UKIMWI. Wengine hupachikwa hata mimba na hawa wabakaji, suala ambalo husababisha maumivu ya kisaikolojia na kushindwa kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya jamii. Pia baadhi yao huachwa na vilema vya kudumu. Hali hii inaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu wengi wao hushindwa kuwalea watoto wao kwani huwa wamelemazwa viungo vya mwili. Wanawake wengi pia wanaachwa wajane hasa baada ya waume wao kuuawa katika vita, na kuachiwa mzigo wa kuwalea watoto peke yao. Baadhi ya watoto huachwa mayatima hasa baada ya wazazi wao wote kuuliwa. Hatima ya watoto hawa ni kukosa elimu kwani hawana watu wa kuwalipia karo. Baadaye wanaishia kurandaranda mitaani. Wengine wanajihusisha na uhalifu mijini kama vile wizi wa kimabavu, uuzaji wa dawa za kulevya na hata kujihusisha na ukahaba ili waweze kujichumia riziki. Mambo haya yote yanaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu watoto hawa wanastahili kuelimishwa, kulishwa na kuvishwa kwani ndio tegemeo la taifa katika siku zijazo.

Mtunzi anawashauri viongozi wa kiafrika waige mfano wa Obasanjo bali wasikatalie mamlakani na kusababisha vita na mauti miongoni mwa wanajamii ambao hawana hatia. Anadokeza haya katika uk. 17 kifungu cha 4 anapomsifu Obasanjo kwa sababu ya kuteremka kutoka kiti cha enzi bila ujanja, ishara ya kwamba hakushurutishwa kujiuzulu mamlakani bali alijiuzulu yeye mwenyewe.

### 4.5 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia jinsi masuala ya kiuchumi na kisiasa yanavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii. Tumebainisha wazi kuwa masuala haya yameathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa kiwango kikubwa. Tungo ambazo zinajihusisha na masuala haya zimechangia pakubwa katika kuonyesha masuala kama vile: ufisadi, umasikini, vita vya kikabila, utabaka, uongozi mbaya miongoni mwa mengine na jinsi ambavyo yanaathiri mifumo ya ekolojia jamii. Masuala haya ya kiuchumi na kisiasa yanaingiliana kwa kiasi kikubwa kwani viongozi ambao wamechaguliwa na wananchi ndio aghalabu hushikilia na kuongoza mifumo ya kiuchumi na nyenzo za kuzalisha mali katika jamii. Siasa mbaya katika jamii huchangia katika kurudisha maendeleo ya jamii nyuma na kuhujumu mfumo wa ekolojia jamii ilhali siasa nzuri ambazo zinaendeshwa kwa njia inayofaa zinaboresha mfumo wa ekolojia jamii. Utafiti wetu umeongozwa na mihimili ya Nadharia ya Uhalisia ambapo msanii huwasilisha maisha ya jamii kwa uwazi na usahihi na kuwasilisha mambo ambayo yanaonekana katika jamii anamoishi. Mhimili huu umetuongoza katika kuangazia masuala halisi ya kiuchumi na kisiasa yanayotokea katika mataifa ya Afrika na yanayoathiri mfumo wa ekolojia jamii. Pia tumeongozwa na mihimili ya Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia ambapo maisha ya jamii huathiriwa na vitu au viumbe ambavyo vinamzingira binadamu. Mhimili huu umetuongoza katika kuangazia kwa mfano jinsi wanasiasa wanavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia muhtasari wa mambo tuliyoyatafitia, Matokeo ya utafiti wetu na mapendekezo kwa tafiti zingine kuhusu kazi za kifasihi zinazoangazia athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia. Madhumuni yetu makuu katika utafiti huu yalikuwa kuangazia athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia kupitia utambulishaji wa mandhari ya kijiografia na uwasilishaji wa maudhui ya kijamii, kiuchumi na kisiasa katika diwani *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014). Utafiti umeshughulikia athari za mtagusano wa jamii na mazingira. Vilevile tumeachangazia athari za masuala ya kijamii katika mfumo wa ekolojia jamii. Aidha tumebainisha athari za masuala ya kiuchumi na kisiasa kwenye mfumo wa ekolojia jamii. Ili kufaulisha haya tumeongozwa na Nadharia ya Uhalisia na Nadharia ya Mfumo wa Ekolojia.

## 5.1 Matokeo ya Utafiti

Utafiti wetu ulijikita katika kuchunguza athari za mtagusano kati ya jamii na mazingira kupitia ubainishaji wa mandhari ya kijiografia. Aidha utafiti umechunguza namna masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa yanavyoathiri mfumo wa ekolojia jamii kupitia ubainishaji wa maudhui katika diwani ya *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014). Katika uchunguzi wetu imebainika kuwa matatizo mengi ambayo hukumba wanajamii yanasababishwa na wanajamii wenyewe. Tumebaini kuwa wanajamii kwa mfano wakiharibu misitu huwa wanaharibu mfumo wa ekolojia. Wanapokata miti kwa sababu ya shughuli za kilimo na za kiuchumi kama vile uchomaji wa makaa na upasuaji wa mbao, wanaathiri makazi ya wanyama ambao huishi misituni. Pia inachangia katika hali ya ukame nchini, kwa sababu miti hii huwa inavutia mvua ambayo husaidia wanyama na mimea. Mvua ikikosekana matokeo yake ni nchi kugeuka na kuwa jangwa. Wanajamii wanakumbwa na njaa na kuathirika kiafya kwa sababu hawana chakula cha kutosha. Mberia amedhihirisha hali hii kupita kwa mazingira ya kijiografia katika diwani ya *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga*. Kwa hivyo ni jukumu la wanajamii wote kutunza misitu na hasa ile ya kiasili ili kuzuia taifa kugeuka jangwa. Wanajamii lazima waelimishwe na washauriwe kuhusu umuhimu wa kupanda miti.

Vilevile utafiti huu umebainisha maudhui ya teknolojia mpya na athari zake. Kwa mfano, imebainika kuwa wanajamii wanaojihusisha na shughuli za kilimo kandokando ya mito na mabwawa wanayaelekeza maji yenye kemikali kali kwenye mito baada ya kunyunyizia mimea yao wakitumia teknolojia ya kisasa. Kemikali hizi zenye sumu zinawaua viumbe ambao wanaishi majini kwani wanakosa hewa safi ya okisijeni. Pia baadhi ya wakulima hawa wanavikita viwanda vyao kando kando ya mito na kuyaelekeza maji taka na kemikali zenye sumu zinazotumika katika viwanda hivi kwenye mito. Madhara yake ni kwamba viumbe vinavyoishi majini vinaangamizwa. Hali hii inaathiri mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu baadhi ya wanajamii wanategemea maji haya katika shughuli za kila siku kama vile kupika, kuoga na kuosha. Isitoshe, baadhi ya wanajamii hutegemea baadhi viumbe wanaoishi katika mito hii kama chakula. Ili kuepukana na madhara haya, wananchi sharti waelimishwe kuhusu athari za kulima kandokando ya chemichemi za maji. Serikali lazima pia iweke sera madhubuti kuhusu viwanda vinavyokitwa kandokando ya mito na wamiliki wa viwanda hivi watumie njia mbadala za kutupa taka.

Utafiti huu pia umedhihirisha kuwa binadamu anapotumia teknolojia ya kisasa wakati anazalisha bidhaa viwandani anahitilafiana na mfumo wa ekolojia. Kwa mfano moshi unaotoka kwenye viwanda hivi unaharibu hali ya hewa na kemikali pia zinazotoka viwandani zinaharibu ukanda wa ozoni. Moshi huu unaharibu hewa inayotumiwa na wanyama, binadamu na hata mimea. Wanyama na binadamu wakikosa hewa safi wanakumbwa na maradhi mbalimbali. Kemikali hizi zinaharibu ukanda wa ozoni hali ambayo inachangia ongezeko la joto duniani. Madhara yake ni kusababisha magonjwa ya ngozi yanayotokana na miale mikali ya jua. Baadhi ya mimea vilevile haiwezi kustahamili joto hili na hatima yake ni kukauka na kuangamia na kuacha wanyama na binadamu bila chakula hali ambayo inaathiri afya zao. Ili kuzuia hali kama hii serikali lazima iweke mikakati na sera madhubuti wakati wa kuanzisha viwanda ili kuhakikisha kuwa hazitoi kemikali kali na zenye sumu ambazo zinaweza kuhitilafiana na mfumo wa ekolojia.

Utafiti huu vile vile umebainisha maudhui ya utamaduni uliopitwa na wakati. Kwa mfano, katika jamii ambazo bado zinashikilia utamaduni wa kumuoza msichana angali bado mdogo zinaathiri mfumo wa ekolojia jamii. Wasichana hawa hupewa majukumu ya uzazi ambayo hawawezi kuyatekeleza vyema. Wengi wao wanaachiwa majukumu ya kuwalisha na kuwavisha watoto wao, hali ambayo inawawia vigumu kiuchumi. Matokeo yake ni kwamba watoto hawa

wanakumbwa na maradhi yanayosababishwa na ukosefu wa lishe bora kwa sababu wazazi wao hawana nguvu za kiuchumi za kuwalisha chakula chenye madini yanayosaidia miili. Pia wazazi hawa wachanga hawana maarifa yoyote kuhusu upangaji uzazi na wanaishia kuzaa watoto ambao ekolojia haiwezi ikastahamili. Matokeo yake ni taifa kurudi nyuma kiuchumi na kijamii kwa sababu watoto hawa ndio wanaotegemewa na taifa katika siku zijazo. Uchunguzi huu pia umebainisha kuwa ubaguzi wa kijinsia na hasa katika taasisi za elimu unaathiri mfumo wa ekolojia jamii. Hii ni kwa sababu wakati jamii inamwelimisha mtoto wa kiume na kumnyima mtoto wa kike elimu, taifa linarudi nyuma kimaendeleo. Hii ni kwa sababu wanawake pia wana mchango mkubwa katika kuendeleza uchumi wa taifa. Elimu ni muhimu sana kwa kila mwanajamii na hasa wakati huu wa uvumbuzi wa teknolojia ya kisasa. Kwa mfano, katika viwanda, shughuli za kilimo na biashara zinahitaji nguvu kazi na ujuzi wa hali ya juu ili kwa mfano kuzalisha chakula kinachotumiwa na wanyama na binadamu na bidhaa zingine za kimsingi. Kwa hivyo jamii ikimnyima mtoto wa kike elimu, inapungukiwa na kuwepo kwa nyenzo za kuendeleza taifa kiuchumi. Kwa hivyo jamii inashauriwa iwaelimishe watoto wote ili kuweza kukabiliana na matatizo ya kiuchumi na kijamii yanayoyakumba mataifa yanayoendelea.

Aidha utafiti huu umebainisha maudhui kuhusu mchango wa vijana katika jamii. Kwa mfano, utafiti umebaini kuwa matatizo mengi ambayo yanawakumba vijana yanatokana na hali ngumu ya kiuchumi. Imebainika kuwa vijana wengi hujihusisha na uhalifu kama vile wizi wa kimabavu, uuzaji wa dawa za kulevya na hata biashara ya ukahaba ili waweze kujikimu kimaisha. Hali hii inasababishwa na ukosefu wa kazi miongoni mwa vijana. Wanaojihusisha na uhalifu huishia kuuawa, kufungwa gerezani na hata wengine kudhoofika kiafya na kulemaa. Ni bayana kuwa taifa lolote lile likitelekeza vijana, wengi huishia kujiunga na vikundi haramu ili wajichumie riziki. Hatima yake ni ukosefu wa usalama na hasa mijini kwani wengi huishia kukaa katika mitaa ya mabanda. Hakuna wawekezaji ambao wanaweza kuwekeza rasilimali zao katika taifa ambalo halina usalama. Jambo hili linachangia uhaba wa uzalishaji wa bidhaa za kimsingi kama vile chakula na mavazi. Vilevile huduma kama vile za kimatibabu na kielimu zinalemazwa. Matokeo yake ni jamii kuathirika kiafya na kukosa nguvu kazi za kuzalisha mali. Pia viumbe vingine ambavyo vinamtegemea binadamu vinaathirika kiafya kwa sababu vinakosa chakula cha kutosha.

Utafiti huu vilevile umebainisha maudhui ya uongozi. Kwa mfano utafiti umebaini kuwa viongozi wa kisiasa wana mchango mkubwa sana katika kuathiri mfumo wa ekolojia jamii. Viongozi hawa huchaguliwa na wananchi ili waweze kulinda rasilimali za taifa. Lakini baadhi yao wanajihusisha na unyakuzi wa mali ya umma, suala ambalo linarudisha maendeleo ya taifa nyuma. Imebainika kuwa viongozi wanaokatalia mamlakani hata baada ya kipindi chao cha kuhudumu kumalizika wanaathiri mfumo wa ekolojia jamii. Wengi husababisha vita vya wenyewe kwa wenyewe na taifa linakosa amani na utulivu suala ambalo huathiri wawekezaji wa kigeni. Vijana ndio aghalabu huhusishwa na vita hivi kutokana na tamaa na ubinafsi wa viongozi. Taifa linapokumbwa na vita wanaoathirika sana ni watoto na wanawake. Wanawake wengi huachwa wajane baada ya waume wao kuuawa kwenye vita na watoto wanaachwa mayatima. Watoto hawa wanaishia kurandaranda mitaani kwa sababu wazazi wao hawawezi kuwalisha, kuwavisha na kuwaelimisha. Wanabakia kuwa wakimbizi katika nchi yao. Vita hivi vinaathiri mfumo wa kiekolojia kwa sababu watoto ambao wanawategemea wazazi wao kwa chakula na mavazi wanaachwa wakijitafutia wenyewe.

## 5.2 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti wetu umeangazia athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia kupitia utambulishaji wa mandhari ya kijiografia na uwasilishaji wa maudhui ya kijamii, kiuchumi na kisiasa katika ushairi wa Mberia *Bara Jingine* na *Rangi ya Anga.* Tunapendekeza kuwa tafiti wa baadaye ziweze kuangazia athari za mtagusano wa jamii na ekolojia kupitia utambulishaji wa mandhari ya kihistoria ambayo hatukuangazia katika utafiti wetu. Aidha tafiti za siku za usoni zinaweza zikatumia Nadharia ya Kisosholojia kuangazia athari za masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kwenye mfumo wa ekolojia jamii katika ushairi wa Kiswahili. Hii ni kwa sababu nadharia hii inazungumzia kuhusu mahusiano baina ya wanajamii na athari zake. Vilevile katika utafiti wetu tumejikita katika ushairi wa Mberia. Kwa hivyo tafiti za baadaye zinaweza kuangazia kazi za kishairi za waandishi wengine na kuzilinganisha na ushairi wa Mberia. Aidha tafiti za baadaye zinaweza kuangazia athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia katika kazi zingine za kifasihi kama vile tamthilia na hadithi fupi.

## 5.3 Hitimisho

Kulingana na madhumuni yetu ni bayana kuwa athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia zinajidhihirisha wazi kupitia utambulishaji wa mandhari ya kijiografia na uwasilishaji wa maudhui ya kijamii, kiuchumi na kisiasa katika *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Rangi ya Anga* (Mberia, 2014). Diwani hizi zinasheheni mandhari na maudhui ambayo yanaonyesha jinsi mfumo wa ekolojia jamii unavyoathiriwa na shughuli za wanajamii. Utafiti huu pia umedhihirisha kuwa maisha na mifumo ya kijamii huathirika na kubadilika wakati binadamu anaharibu ekolojia.

## MAREJELEO


Abdalla, A. (1972). *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.

Aineah, A. (2018). 'How lectures prey their students'. *Standard Digital.* Makala kutoka *hhttps://standard.co.ke.* August, 4.

Bertoncini, E. (2010). "Some Remarks on Kithaka wa Mberia Poetry". *Swahili Forum* 17: 91-103 Makala kutoka *hhttps://scholar.google.com.*

Biko, R. (2018). 'Experts call for use of tecknology in Agriculture.' *The Standard.* Makala kutoka *hhttps://www. standard.co.ke*. June, 18.

Bronfenbrenner, U. (1989). *Ecological System Theory*. London: Greenwich Limited.

Bronfenbrenner, U. na Ceci, J. (1994). 'Nature & Nurture Reconceptualized in Development Perspective': A Biosecological. Psychological Review101,568-586.

Bronfenbrenner, U. (2005). *Making Human Being Human*. *Bioecological Perspectives on Human Development*. London: Sage Publications Limited.

Chuma, A. (2018). 'How ten year- old girl was married to three different men'. *Citizen Digital*. Makala kutoka *hhttps://www. Citizen.co.ke*. August, 4.

Claser, M. (2002). *Human & Nature Interaction in the Anthropocene*. *Potential of Social-Ecological systems Analysis.* Makala kutoka *hhtp://www.oekm.de.*

Clement, U. (2015). 'Rwanda vote on constitution changes'. Makala kutoka *https://www. reuters.com.* December, 17.

Crutzen, P. (2008). Geology of Mankind. The Anthropocene. Nature 415: 23. Makala kutoka *hhtp://www.oekm.de*.

Gicuku, M. (2011). "Usawiri wa Maudhui ya Ndoa katika Ushairi wa Euphrase Kezilahabi Kithaka wa Mberia." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta (haijachapishwa).

Gromov, M. D. (2006). “The Question of Kiswahili Style Again? Of Kithaka wa Mberia” *Swahili Forum* 69: 109-126.

Harries, L. (1962). *Swahili Poetry*. London: Oxford University Press.

Hegel, G. W. (1971). *Introduction to Aesthetics*. Clarendon: Oxford University Press.

Kamau, A. (2018). ‘Makongeni where customers ‘chew’ hookers on credit’. *The Standard*. Makala kutoka *hhttps://www.standard.co.ke.* August, 3

Kanyua, M. G. (2013). “Mtindo unavyoendeleza Maudhui katika *Natala*”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi.* Nairobi: Heinmann Education Books.

Kezilahabi, E. (2008). *Dhifa*. Nairobi: Vide – Muwa Publishers Limited.

Khafafa, L. (2018). ‘Bobi Wine: Uganda’s new political senstention’. *The Standard* Makala kutoka *hhttps://www.standard. co.ke.* August, 28

Kibaru, C. (2016). “Taashira ya Mazingira katika Ushairi wa Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (haijachapishwa).

King’ei, K. na Kemoli, A. (2001). *Taaluma za Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

Kobia, J. (2007). ‘Tumbombele Mla Misitu,’ katika Mbatiah, M. (mh) uk. 137- 153. Nairobi: Focus Publishers Limited.

Kombo, K. na Tromp, A. (2006). *Proposal and Thesis Writing. An Introduction.* Nairobi: Pauline Publishers Limited.

Krebs, C. (1978). *Ecology. The Experimental Analysis of Distribution and Abundance*. New York. Herper Limited.

Letiwa, P. (2018). ‘Charcoal trade, logging wiping out Mau Forest. *Daily Nation*. Makala kutoka *https://www.nation.co.ke*. May, 6

Lukacs, G. (1963). *The Meaning of Contemporary Realism* London: Merlin Publishers.

Mativo, S. (2018). 'Kenya world posses looming danger of high temperature'. *Citizen Digital*. Makala kutoka *https://www.citizen.co.ke*. August 7

Mberia, K. (1997). *Mchezo wa Karata*. Nairobi: Marimba Publishers Limited.

____________(1997). *Natala*. Nairobi: Marimba Publishers Limited.

____________(2001). *Kifo Kisimani.* Nairobi: Marimba Publishers Limited.

____________(2001). *Bara Jingine*. Nairobi: Marimba Publishers Limited.

____________(2004). *Maua Kwenye Jua La Asubuhi*. Nairobi: Marimba Publishers Limited.

____________(2005). *Redio na Mwezi*. Nairobi: Marimba Publishers Limited.

____________(2007). *Msimiu wa Tisa*. Nairobi: Marimba Publishers Limited.

____________(2014). *Rangi ya Anga.* Nairobi: Marimba Publishers Limited.

Mbogo, E. (2002). *Bustani ya Edeni.* Dar es Salaam: MPB Enterprises.

Mcdougal, L. (2009). *American Literature.* New York: Houghton Mifflin Publishing Company.

Mogeni, M. (2015). "Fani na Maudhui katika Mashairi ya Magazetini ya Taifa Leo". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (haijachapishwa).

Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Momanyi, C. (2009). *Nakuruto*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Moore, N. (2008). 'Eco/ feminism, non- violence, and the future of feminism'. *International Feminism* J Pol, 10(3),282-298.

Mueni, J. (2018). 'Cleaning Nairobi River needs proactive approach'. *The Standard*, Makala kutoka *hhttps://www.standard.co.ke*. April, 9.

Mwangi, J. (2013). "Uhalisia na Uhalisia Ajabu katika Riwaya Mpya". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Nabeta, S. na Ongutte, R. (2014). 'Literary environmentalism: An ecocritique of Kiswahili Literature'. *International Journal of Ecology and Ecosolution* vol. 1(2), pp. 29-41, August 2014 Review.

Nasimiyu, M. (2016). "Athari ya Mazingira ya Kihistoria na Kijamii katika Uwasilishaji wa Maudhui katika Diwani ya Dhifa." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (haijachapishwa).

Ngari, A. (1998). "Utetezi wa Haki za Wanyonge katika Diwani ya Mchezo wa Karata". Tasnifu ya Elimu (sanaa). Chuo Kikuu cha Nairobi. (haijachapishwa).

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustana College.

Nyambura, A. (2014). "Matumizi ya Kinaya katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia". Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta (haijachapishwa).

Nyaundi, L. (2017). 'Gender ministry takes over sanitary pads distribution to schools girls'. *The Star.* Makala kutoka *hhttps://star.co.ke*. October, 6.

Nzuki, P. (2003). "Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Odhiambo, H. (2017). 'Fishermen blame pollution for Lake Victoria fish decline'. *The Standard*. Makala kutoka *https://www.standard.co.ke*. January, 9.

Odum, E. (1971). *Fundamentals of Ecology*. Philadelphia. Third Edition. Makala kutoka *https://www.researchgate.net*.

Ongarora, S.M. (2017). 'Contempranity of Themes in Kithaka wa Mberia Poetry'. *International Journal of Science, Arts and Commerce* Vol 2. 1, March 2017.

Orodho, A. (2005). *Elements of Education and Social Science Research Methods.* Nairobi: Masola Publishers Limited.

Raffel, B. (1984). *How to Read a Poem*. New York: Penguin Publishers. Report. Vol. 2, No.1.

Sabula, A. M (2014). 'Nafasi ya Wanawake katika Uhifadhi wa Mazingira katika Riwaya ya Nakuruto: Mtazamo wa Fasihi ya Ufeministi wa Ekolojia'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (haijachapishwa).

Sayange, G. (2018). 'New twist in Mau Forest evictions'. *Daily Nation* Makala kutoka *https://www.nation.co.ke*. August, 6.

Waithera, A. (2018). 'Earth Moves, cracks opens and land slides in Murang'a'. *The Star*. Makala kutoka *https://www.the star. co.ke*. May, 26.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers.

____________(2003). *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Vide – Muwa Publishers Limited.

___________(2008). *Msimu wa Vipepeo.* Nairobi: Vide – Muwa Publishers Limited.

____________(2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide – Muwa Publishers Limited.

Warutere, P. (2018, March 7). 'Why Kenyans should be serious about Protecting forest'. *Daily Nation.* Makala kutoka; *hhttps://www.nation.co.ke*

Waweru, G. (2014). "Uhakiki wa Fani katika Tamthilia za Mberia". Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Egerton (haijachapishwa).